Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Nne - Tarehe 18 Aprili, 2005**

*(Ulianza Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mkutano wa Kumi na Tisa unaendelea baada ya mapumziko ya mwisho wa wiki.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Siyo muda muafaka usimwi-*interrupt* Spika wakati anazungumza na Wabunge. Hiki ni Kikao cha Nne cha Mkutano wa Kumi na Tisa sasa kikao kinaanza, Katibu endelea.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 45

**Madai Mbalimbali ya Walimu**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa kauli mbalimbali za kusisitiza kulipa madai ya walimu na kwa kuwa baadhi ya walimu wakiwemo wa Wilaya ya Liwale, bado wanaendelea kusumbuka kwa kucheleweshwa kwa madai yao:

(a) Je, ni walimu wangapi na kiasi gani cha fedha kimelipwa kwa madai hayo hadi sasa na kati ya hao ni wangapi wa Wilaya ya Liwale?

(b) Je, Serikali itahakikisha kuimaliza kero hiyo ya walimu nchini ndani ya awamu hii ya uongozi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalile, Mbunge wa Jimbo la Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikitoa kauli za kusisitiza kulipa madai ya walimu. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati akijibu swali namba 1 la tarehe 12 Aprili, 2005 hapa Bungeni, Serikali imelipa jumla ya Sh.9,844,254,602/80 kwa ajili ya walimu 36,258 ambao madai yao yalihakikiwa na kuthibitika kuwa ni halali. Kuhusu madai ya walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, walimu 210 waliwasilisha madai ya jumla ya shilingi 108,321,160/=. Madai yaliyothibitika kuwa ni halali ni ya walimu 128 ambao tayari wamelipwa jumla ya shilingi 65,434,225/=. Walimu hao wote 128 wamekwishalipwa madai yao, isipokuwa mwalimu mmoja aliyefariki dunia ambaye hundi yake itakabidhiwa kwa ndugu za marehemu kwa kufuata taratibu za urithi. Madai ya Walimu 82 yalikataliwa na Serikali na kwa maana hiyo, hawatalipwa madai yao.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika sehemu (a) hapo juu Serikali ya Awamu ya Tatu, bado ina dhamira ya kumaliza kabisa kero hii na ndiyo maana imeweza kulipa madai ambayo yamehakikiwa tayari. Aidha ili kuepuka matatizo hayo kutokujirudia tena Serikali imekwishatoa maagizo kwa Halmashauri zote nchini kuwa Watumishi hasa walimu, wasihamishwe kama hakuna fedha za uhamisho.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inashughulikia madai kwa watumishi wote wa Halmashauri na siyo walimu peke yao.

Aidha Serikali inazidi kuzisisitiza Halmashauri kujiepusha na ulimbikizaji wa madeni usio wa lazima. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Je, hali ikoje nchini kote kuhusu madai hayo ya walimu?

(b) Sijui kama unaelewa kwamba madai haya unayozungumzia ni ya kuanzia mwaka 2000 tu mpaka sasa hivi. Wale walimu waliokuwa na madai kabla ya mwaka 2000 mpaka hivi sasa hawajalipwa. Je, Serikali ina utaratibu gani kwa walimu hao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya madai ya walimu ilivyo nchini kote, naomba tu nirudie niliyoyasema. Zoezi la kuhakiki madai haya lilikwishafanyika na wale waliostahili kulipwa wamelipwa. Lakini lazima niseme kwamba ili mradi madai yale ambayo yaliafikiwa yakaonekana hayana uhalali, tushirikiane wote kujaribu

kulieleza jambo hili kwa sababu ni letu wote. Malipo yanafanywa lakini kwa taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu ambao madai yao ni ya kabla mwaka 2000, jambo hili lilishawahi kuulizwa na likaelezwa. Wote mtakumbuka Serikali ilifanya juhudi sana kuhakikisha madai yote yawe yamelipwa ifikapo mwaka 2000 kwa madai yote ya siku za nyuma. Kazi hiyo, ilifanyika na madai yalilipwa mpaka mwaka 2001 Serikali ilikuwa bado inaendelea kumalizia madeni ya nyuma. Ninaloweza kusema kama bado watu wanadai madai ya nyuma baada ya kuwa malipo yamefanyika, mimi nadhani tusaidiane tu, wanaweza kuwasilisha madai yao kunakohusika, juhudi ziendelezwe kuona kama wanastahili kulipwa au hapana. *(Makofi)*

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya walimu ambao hawakulipwa au madai yao hayakuhakikiwa ni kwa sababu fedha zao ziliibiwa kwa kusaidiana na Watumishi wa Halmashauri pamoja na Watumishi wa Wizara ya Fedha. Je, Serikali inasemaje kuhusu haya madai ambayo walimu hawakulipwa lakini si kwa sababu ya kosa lao bali fedha ziliibiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishasema kwamba kwa wale wote ambao madai yao yamehakikiwa na kuonekana ni halali, fedha zimelipwa na kama bado kwa maana hao litakuwa ni zoezi tu la kuendeleza kuhakikisha limekamilika. Kama upo wizi uliokuwa umefanywa kati ya Halmashauri na Wizara ya Fedha nadhani suala hilo ni wazi maana ni la kisheria na Serikali haiwezi kumnyima mtumishi ambaye madai yake yamehakikiwa kwa sababu ya wizi. Serikali itatekeleza wajibu wake lakini kwa upande mwingine Serikali vile vile itawabana wahusika kuhakikisha na wao wanapata wanachostahili. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa walimu 104 wa Mtwara Vijijini waliitwa na Halmashauri kuja kuchukua *cheque* zao walipokuja walikuta *cheque* za walimu 4 tu, walimu 100 wote *cheque* hakuna ni kwa nini na wale 100 wameshalipwa au bado mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Hali hiyo, ilijitokeza Mtwara na kwa ufuatiliaji mzuri wa Mheshimiwa Namkulala alinipigia simu na mimi niliondoka mwenyewe kwenda kwa Mhasibu Mkuu akasimamia jambo hilo likatekelezwa na walimu wote wamelipwa na Mheshimiwa Namkulala juzi amethibitisha hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 46

**Mgogoro wa Mpaka Kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hatma ya mgogoro wa mpaka uliodumu kwa muda mrefu kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge, uliachwa mikononi mwa Serikali na kwa kuwa Serikali iliahidi kutoa maelekezo ya mpaka huo mnamo mwezi Septemba, 2004 lakini haikufanya hivyo.

(a) Je, ni lini kazi hiyo itatekelezwa kama Serikali ilivyoahidi?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya maeneo mengi nchini yenye migogoro ya mipaka kwa muda mrefu na kuwaacha viongozi na wananchi wa maeneo hayo wakizozana bila Serikali kuchukua hatua za haraka za kupunguza na viongozi na wananchi wa maeneo hayo na kutoa maelekezo ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli upo mgogoro wa mpaka wa muda mrefu kati ya Wilaya ya Manyoni upande wa Mkoa wa Singida na Wilaya ya Sikonge Mkoani Tabora. Kwa muda mrefu jitihada zimekuwa zikifanywa na mamlaka mbalimbali kushughulikia mgogoro huo zikishirikiana na wananchi, wataalam kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika kukamilisha zoezi hili mwaka jana 2004 tulikubaliana likamilike kabla ya tarehe 31 Julai, 2004.

Hata hivyo, kufuatia majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kazi hii iliahirishwa na itafanywa kabla ya kumalizika mwaka wa fedha 2004/2005.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna maeneo mengine hapa nchini yenye migogoro ya mipaka licha ya mgogoro wa Wilaya mbili hizi nilizozitaja na ofisi yangu kwa kushirikia na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mikoa inaendelea kuyashughulikia. Kwa mfano mgogoro uliokuwepo kati ya Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara na Wilaya ya Kondoa Mkoani Dodoma umefanyiwa kazi na umemalizika. Aidha, mgogoro kati ya Wilaya ya Biharamulo Mkoani Kagera na Bukombe Mkoani Shinyanga umekwishafanyiwa kazi na wataalam kwa kushirikiana na Mikoa husika na maagizo yametolewa na ofisi yangu baada ya kukutana na viongozi wa Mikoa na Waheshimiwa Wabunge wa Biharamulo na Bukombe. Maagizo yangu naomba kurudia ni kwamba maelekezo ya mpaka kati ya Bukombe na Biharamulo ni kama yalivyo katika *GN.* Na. 27 ya tarehe 27/1/1961.

Tangazo hilo la Serikali Na. 27/1961 linaonyesha wazi kwamba mpaka kati ya Mkoa wa Shinyanga na Kagera haujawahi kubadilishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la kujirudia rudia kwa migogoro ya mipaka na njia iliyoonekana ni muafaka ni ushirikishwaji wa wahusika wote katika eneo linalibishaniwa na baada ya kukubaliwa basi utaratibu wa kutekelezwa unafuata. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize swali. Lakini vile vile naomba nimshukuru Mheshimiwa Said Nkumba kwa kuikumbusha Serikali juu ya kushughulikia hili tatizo la mpaka.

Kwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aliwahi kutoa kauli kwamba kijiji kinachogombewa cha Kalangali kipo Sikonge na katika kitabu kilichotolewa na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi mwaka jana, kuna kitabu kilitolewa kikionyesha kila Wilaya na Vijiji vyake na katika hicho kitabu Kijiji cha Kalangali ambacho ndiyo kinachogombewa kilionyesha kiko Manyoni.

Je, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, atakuwa tayari kupitia hicho ili aweze kubadilisha kauli yake kwamba kile kijiji kirudi Wilaya ya Manyoni. (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iwvata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema kwa niaba ya Waziri naomba tuliahidi Bunge lako kwamba tutapata nafasi ya kwenda kuangalia hali halisi ilivyo katika mgogoro kati ya Manyoni na Sikonge na mimi nadhani baada hapo ndipo hatua nyingine za kurekebisha kauli ya Serikali zitafuata. Kwa sasa naomba tu tushirikiane na Mheshimiwa Iwvatta ili tulimalize.

Na. 47

**Mfuko wa Huduma za Jamii - *TASAF***

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE (K.n.y. MHE. FATMA SAID ALI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa Huduma za Jamii *(TASAF)* umeendelezwa hadi kufikia Wilaya 40 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na kwamba umeonyesha mafanikio makubwa.

(a) Je, ni sababu gani/zipi zilizocheleweshaujenzi wa soko la Makadara Jimboni Mlandege?

(b) Je, ni lini mfuko huo utaanza kwa awamu ya pili Tanzania Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y.WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Soko la Makadara Jimboni Mlandege, Unguja, halikuingizwa katika mpango wa kujengwa kwa fedha za *TASAF* kwa kuwa wananchi hawakutoa kipaumbele kwa soko hilo wakati wa pembukizi shirikishi jamii. Vivyo hivyo kama wananchi wataendelea kutoa kipaumbele kwa miradi mingine na siyo soko hilo, *TASAF* itakuwa haina uwezo wa kuwalazimisha kutekeleza wasichokuwa wamekiona ni kipaumbele kwao.

Kama inavyofahamika programu ya *TASAF* inatekelezwa kwa kuzingatia ushirikishwaji wa wananchi, kwani hubaini matatizo wenyewe na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yao, kwa kuandaa mipango shirikishi na kuweka kipaumbele katika utekelezaji kulingana na uwezo walionao. Hii ina maana kitakachotekelezwa ni kile wananchi walichoamua wenyewe. *(Makofi)*

(b) Kufuatilia mafanikio katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* katika Wilaya 40 za Tanzania Bara na kwenye Visiwa vya Pemba na Unguja kwa upande wa Zanzibar Serikali iliamua kuwa awamu ya pili ya *TASAF* ambayo itatekelezwa katika Halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa zote za Tanzania Bara na kwenye Visiwa vya Pemba na Unguja Tanzania Zanzibar.

Maandalizi ya awamu ya pili ya *TASAF* yalianza mwaka 2003 yakisimamiwa na timu maalum ya maandalizi iliyoundwa na Serikali ikijumuisha wajumbe toka Tanzania Bara na Zanzibar. Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Dunia iliridhia na kupitisha mradi wa awamu ya pili *TASAF* tarehe 30 Novemba, 2004. Benki ya Dunia imeidhinisha kiasi kiasi cha dola za Kimarekani milioni moja na hamsini elfu. Awamu ya Pili ya *TASAF* itahusika zaidi na ngazi ya jamii na itakuwa na sehemu kuu mbili, ambazo ni Mfuko wa Taifa wa Kijiji na Mfuko wa kuimarisha uwezo. Mfuko wa Taifa wa Kijiji umetengewa dola za Kimarekani milioni mia moja na ishirini na kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kuimarisha uwezo ni dola za Kimarekani milioni 30.

Kipindi cha utekelezaji ni miaka mitano yaani, kuanzia mwaka 2005 hadi 2009. Uzinduzi wa awamu ya pili ya *TASAF* unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Mei 2005. Utekelezaji wa awamu ya pili ya *TASAF* utaanza baada ya uzinduzi huo kwa nchi

nzima. Kwa kuwa Serikali imekubali kuandaa semina juu ya jambo hili kwa Waheshimiwa Wabunge katika mkutano huu naomba kuthibitisha kwamba semina hiyo, itafanyika na maswali yote ambayo mlitarajia kuniuliza leo naomba muyaweke. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa, tunakubaliana na wewe maswali kwa Wizara ya Fedha.

Na. 48

***Unit Trust of Tanzania***

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Sheria ya Udhamini Na. 375 ya Sheria za Tanzania imewezesha kuwepo kwa *UTT* na miongoni mwa malengo ya sasa ya *UTT* ni pamoja na kuanzisha na kuendesha mipango ya uwekezaji wa pamoja ili kufikia malengo ya dhamana:-

(a) Je, kuna kanuni au utaratibu wowote uliowekwa wa kuhakikisha kuwa wana jamii maskini hasa wale wa vijijini wanafaidika na mpango huo?

(b) Je, kuna malengo yoyote ya uwezeshaji yenye manufaa yanayoandaliwa katika mpango huo?

(c) Kwa kuwa vipo vikundi vya wanawake na vijana katika maeneo mbalimbali mfano Madaba, Wino, Kigonsera, Namtumbo, Peramiho, Tunduru. Je, ni utaratibu gani umeandaliwa wa kuvifanya vikundi hivyo vinufaike na huo mpango wa uwekezaji wa pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Dhamana ya Uwekezaji ilianzishwa mwezi Juni, 2003 chini ya Sheria ya Udhamini sura ya 375 ya Sheria za Tanzania. Hadi kufikia sasa, dhamana imekwisha kamilisha matayarisho mengi yakiwemo yafuatayo:-

(i) Kutengeneza mpango maalum wa muda wa miaka mitano wa dhamana hiyo.

(ii) Kukamilisha dhana ya mpango wa uwekezaji wa mwanzo utakaoendeshwa na dhamana ambao umepewa jina la Mfuko wa Umoja *(Umoja Fund)*

(iii) Kuajiri watumishi wa taaluma mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu ya kitaalamu ya kuendesha Mfuko wa Umoja.

(iv) Kutoa elimu kwa umma juu ya shughuli za dhamana na kuhamasisha wananchi wajitayarishe kushiriki kwenye mfuko huo hapo utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, inategemewa kwamba Mfuko wa Umoja utazinduliwa tarehe 16 Mei, 2005 ambapo wananchi watawekeza kwenye mfuko huo. Ili kuwezesha mfuko huo kuanza shughuli zake kwa ufasaha, Serikali imekwishafanya maamuzi yafuatayo:-

(i) Kutoa hisa zake asilimia mbili (2%) kutoka kwenye Kampuni ya Bia za asilimia moja (1%) ya hisia zake kwenye Kampuni ya Sigara kama mtaji wa mwanzo kwenye Mfuko wa Umoja. Hisa hizo zina thamani ya takribani shilingi za Kitanzania bilioni 10.

(ii) Kutoa punguzo la bei ya dhamana za mfuko kwa kiasi cha asilimia thelathini (30%) kwa unit moja ili kuwapa nafasi wananchi wamiliki dhamana za Mfuko wa Umoja kwa ajili ya mafanikio yao.Baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Katika kuweka mazingira ya ushiriki wa wanajamii maskini na hasa wale walioko vijijini katika mpango huo, dhamana imefanya matayarisho yafuatayo:-

(i) Kupanga bei ya dhamana za Mfuko wa Umoja kwenye thamani ya chini kabisa yaani shilingi mia moja kwa unit moja. Aidha, kiwango cha chini cha *units* za kununuliwa kuwa hamsini hivyo kuhitaji jumla ya shilingi elfu tano tu kuweza kuwekeza kwenye mfuko huo.

(ii) Kwa kuzingatia punguzo la bei kwa *units* za Mfuko wa Umoja kwa kiasi cha asilimia thelathini (30%) kama nilivyokwishaelezea, ina maana kwamba mwananchi ambaye amewekeza kwa kiasi cha shilingi elfu tano sasa ataweza kuwekeza kwa kiasi cha Shilingi 3,500 tu.

(iii) Taratibu zinaandaliwa ambazo zitamwezesha mwananchi kushiriki katika uwekezaji akiwa Wilayani kwake kupitia mabenki pamoja na Ofisi za Posta.

(b) Malengo ya uwezeshaji wanufaika ambayo yanaendana na malengo ya uwekezaji wa pamoja na pamoja na kuweka mazingira ya makundi mbalimbali ili kujijengea mitaji kwenye njia zinazotambulika na mbinu zinazoeleweka. Nia ni kuweka mazingira ya kukijenga kidogo walicho nacho kufikia kiasi ambacho wataweza kukidhi mahitaji makubwa kuliko wanavyoweza hivi sasa.

(c) Taratibu zilizowekwa na dhamana za kuwezesha vikundi mbalimbali vya wanawake na vijana vikiwemo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge Vijiji vya Madaba, Wino, Kigonsera, Peramiho, Tunduru na kadhalika ili kuviwezesha kunufaika na mpango huu wa uwekezaji wa pamoja ni pamoja na:-

(i) Kuhakikisha kwanza, lazima vikundi viwe vimesajiliwa kisheria na pili, viwe hai na vifikie maamuzi ya kuwekeza kwenye Mfuko wa Umoja kwa kufuatana na kanuni za kikatiba zinazoongoza vikundi hivyo.

(ii) *Unit trust of Tanzania* kutoa elimu kwa vikundi ili kuviwezesha kwanza, kuelewa dhana nzima ya Mfuko wa Umoja na Pili, kujiandaa kushiriki wakati utakapofika.

(iii) Mara baada ya Mpango wa Umoja kuzinduliwa, *UTT* itaanzisha Mpango wa Udhamini wa Mikopo *(Credit Guarantee Scheme)*. Mpango huu utaviwezesha vikundi mbalimbali kukopa toka taasisi za fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye Mfuko ambapo dhamana hiyo itazihakikishia taasisi hizo za fedha ulipaji wa sehemu ya mikopo iwapo vikundi hivyo vitashindwa kulipa.

Na. 49

**Ufuatiliaji wa Malipo ya Pensheni.**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:

Kwa kuwa wastaafu nchini bado wanafuatilia pensheni zao kwenye Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam na kukaa huko kwa muda mrefu bila mafanikio na baadhi yao hupata ajali na kupoteza maisha yao.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kero hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna kila sababu ya kuhamishia huduma hiyo mikoani ili wastaafu wasiendelee kuteseka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wastaafu nchini wamekuwa wakifuatilia pensheni zao Wizara ya Fedha Dar es Salaam ambapo ni mbali na mikoa wanapotoka na hivyo kuwasababishia usumbufu. Kwa kutambua hilo Wizara imeweka na kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuwaondolea wastaafu kero ambayo wamekuwa wakiipata. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kutoa waraka ambao unawaelekeza waajiri wote nyaraka muhimu zinazohitajika wakati wa kufanya malipo na muda wa kuleta majalada yenye kumbukumbu za wastaafu ili malipo yasikwame kutokana na nyaraka pungufu.

(ii) Kuanzisha Hazina Ndogo katika Mikoa yote hapa nchini ambazo pamoja na majukumu mengine zina jukumu la kuwahudumia wastaafu huko mikoani.

(iii) Kuwatumia wastaafu hundi zao kwa njia ya Posta kwa kutumia anwani zao.

(iv) Kuanzisha Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma *(PSPF)* na Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali *(GEPF)*. Vyombo hivi vimekuwa vikichukua kumbukumbu mbalimbali za wafanyakazi wa Utumishi wa Umma, wakati wa kujisajili na hivyo kurahisisha ulipaji wa pensheni wakati wa kustaafu kutokana na kuondoa ucheleweshaji unaotokana na ukosefu wa kumbukumbu za wastaafu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa ni mara nyingi Serikali imekuwa ikitamka kwamba huduma hii ya wastaafu inahamishiwa Mikoani ambayo zimefunguliwa Ofisi za Hazina Ndogo lakini mpaka sasa bado ni wimbo tu. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna haja ya kutamka kabisa muda maalum na wastaafu nchi nzima wasikie ili waache tabia za kuparamia magari na kupata matatizo ya aina mbalimbali huko Dar es Salaam? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa hata Jengo la Kitengo cha Pensheni huko Dar es Salaam linatumia Pangaboi wakati lina Watumishi wengi humo ndani halina hata viyoyozi ukizingatia kwamba Dar es Salaam kuna joto kubwa na wastaafu wanafika wengi. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja pia jengo hilo liwekwe viyoyozi ili watumishi waweze kufanya kazi kwa raha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Malipo ya wastaafu katika *sub treasury* siyo nyimbo, *sub treasury* zipo na *in fact* hayo yameshaanza kufanyika. Kuna baadhi ya wakati yanapotokea matatizo kwamba hakuna rekodi kamili za wastaafu, hapo ndiyo yanapochelewa hapa ndiyo wastaafu wanapokimbilia Dar es Salaam. Lakini hakuna ulazima wa kufanya hivyo. Kuna mifano halisi kwamba baadhi ya Wafanyakazi wamekuja Wizarani kutafuta mafao yao na unawaambia kwamba mbona haya yako katika *sub treasury* yako au kwa mujibu wa wa anwani uliyotoa kwamba malipo yafanyike huko hujaenda na hivyo mwisho wake *cheque* zinarejeshwa Wizara ya Fedha, zimeshachacha. Kwa hiyo, bado tunaomba Wastaafu wanapostaafu bado wafukuzie *sub treasury* na kama kuna matatizo wayapeleke pale badala ya wao kuharakisha kuja Wizara ya Fedha.

Kuhusu jengo kuwa na viyoyozi, hali itakaporuhusu hata kama Wizara ya Fedha hili tunaweza kuweka kwenye Bajeti kwa hiyo tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Na. 50

***Mbinga Coffee Curing Company LTD***

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kiwanda cha Kukoboa Kahawa cha Mbinga *(Mbinga Coffee Curing Company Ltd.)* kinamilikiwa kwa pamoja na Serikali na wakulima wa Kahawa nchini kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika na kwa kuwa Chama Kikuu cha Ushirika Mbinga (MBICU) kilichokuwa kinamiliki hisa kwa niaba ya wakulima wa kahawa Mbinga kimefilisiwa na kuwafanya wakulima hao wa kahawa Mbinga kukosa umiliki katika kiwanda hicho ambacho ni tegemeo pekee la kiuchumi Wilayani humo. Je, ni lini Serikali itauza hisa zake kwa wakulima wa kahawa wa Wilaya hiyo ili kurahisisha mipango ya Serikali ya Ubinafsishaji wa vitega uchumi wake?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha kukoboa kahawa cha Mbinga kilikuwa kinamilikiwa na Serikali kupitia Bodi ya kahawa kwa asilimia mia moja hadi hapo tarehe 18/9/1995, Bodi ilipoamua kugawa sehemu ya hisa hizo kwa Vyama vya Ushirika vilivyochangia kwenye ujenzi wa kiwanda hivyo kukifanya sasa kimilikiwe kwa pamoja kati ya Serikali na Vyama vya Ushirika vinavyojishughulisha na zao la kahawa nchini.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika vya Kahawa nchini kwa ujumla wake vinamiliki hisa 727,750 zenye thamani ya Shilingi 727,750,220 sawa na asilimia 56.5 ya hisa zote na Serikali inamiliki asilimia 43.5 zilizobaki. Hadi kilipofilisika, Chama Kikuu cha *MBICU* kilikuwa kinamiliki hisa 107,402 zenye thamani ya Shilingi 107,402,035/= ambazo ni sawa na asilimia 8.3 ya hisa zote za kiwanda hicho cha kahawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya *MBICU* kufilisika, hisa zake katika kiwanda kama ilivyo kwa mali zake nyingine ziliwekwa chini ya mfilisi. Mali hizo zikiwemo hisa ndizo zinazopaswa kuuzwa ili kuwalipa wadai mbalimbali wa *MBICU*. Kwa hali hiyo vyama vya msingi vya Wilaya ya Mbinga vinapaswa kuomba kununua upya hisa kutoka kwa mfilisi wa Chama Kikuu cha *MBICU* ili viweze kushiriki katika kumiliki tena kiwanda hicho kwa niaba ya wakulima wanachama wake. Kwa hisa zinazomilikiwa na Serikali msimamo ulikwishatolewa kueleza nia yake ya kutaka kuuza asilimia 43.5 ya hisa zake kwa wakulima kupitia vyama vyao vya Ushirika nchini kote. Kwa hiyo, vyama vyenye uwezo na nia ya kununua hisa ambazo bado zinamilikiwa na Serikali vinaweza kufanya hivyo kwa kufuata utaratibu kama ule uliotumika katika kununua hisa za Kiwanda cha *TANICA*, Mkoa wa Kagera. Wizara ya Ushirika na Masoko itatoa msaada wa kitaalam kama itaombwa kufanya hivyo.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kiwanda cha kukoboa kahawa cha Mbinga kinaendeshwa kwa faida kubwa sana na hivyo wanahisa kupata

gawio. Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba lile gawio ambalo Mfilisi anapata linasimamiwa sawasawa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki cha kahawa kinapata faida na kutoa gawio kwa wanahisa wake ikiwa ni pamoja na ile ya *MBICU.* Gawio hilo linakwenda kwa Mfilisi kama ambavyo nisema kwamba sasa hivi mali zote zinasimamiwa na Mfilisi. Kwa hiyo, namna nzuri ya kuhakikisha kwamba inasimamia vizuri ni kwa Mfilisi kuzitunza hizo hisa pamoja na gawio ili itakapokuwa inaziuza kwa wahusika na gawio hilo liweze kuwa ni mojawapo.

Kwa hiyo, namna ya kuhakikisha kwamba zinatumiwa vizuri au inasimamia vizuri ni kwa Mfalisi kufanya kazi yake kwa utaratibu unaotakiwa.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyama vingi vikuu vya ushirika vinafilisika kutokana na mfumo ulioko si nzuri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta sheria ambayo inaleta mazingira mazuri ambayo itafanya wasiweze kufilisika mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kufilisika kwa Vyama vya Ushirika hakutokani na kwamba mambo ya kisheria ni mbaya. Sheria zinazotungwa na Bunge hapa zina nia ya kusimamia utekelezaji nzuri wa vyama vya ushirika. Lakini nataka nikumbushe tu kwamba Mheshimiwa Mbunge anaomba kwamba ije sheria ya kuvifanya vyama vya ushirika vifanye vizuri.

Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba mwezi Novemba 2004 Bunge lako Tukufu lilitunga sheria ambayo moja ya madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha kwamba inadhibiti wizi pamoja na usimamizi mbaya ili kulinda vyama vya ushirika visiweze kufilisika. Kwa hiyo, haiwezi kuleta tena Serikali Sheria nyingine wakati tayari tumeshatunga sheria nyingine hivi karibuni.

Na. 51

**Ukosefu wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo Tutamba na Milola**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mahakama za Mwanzo, zinasaidia kutoa huduma kwa kesi zilizoko katika eneo husika na kwa kuwa Mahakama za Mwanzo za Rutamba na Milola zimekosa Mahakimu kwa muda mrefu sasa na kwamba kesi zote zinazohusu wananchi wa kata hizo zinapelekwa katika Mahakama ya Mwanzo ya Ng'apa na kwa kuwa Mahakama hiyo iko katika Tarafa ya Ng'apa umbali wa kilomita 20 toka Milola:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima haki wananchi wa Kata za Rutamba na Milola kwa kukosa hakimu kwa muda mrefu na ni nani anayelipia gharama za usafiri

mgumu usio na uhakika kwa walalamikaji na walalamikiwa wanaotoka Milola na Rutamba kwenda Ng'apa?

(b) Je, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Ng'apa anapewa posho ya kufanya kazi za Mahakama hizo tatu?

(c) Je, ni lini Serikali itaajiri Mahakimu kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo katika Kata hizo na nyinginezo nchini ambazo zina shida ya watumishi hao?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria D. Watondoha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba ukosefu wa hakimu katika Kata za Rutamba na Milola ni kuwanyima haki wananchi hao, lakini hili halifanyiki kwa makusudi. Mapungufu haya yanatokana na tatizo la upungufu mkubwa wa Mahakimu.

Hivi karibuni Serikali imezindua Mkakati wa Kati wa mwaka 2005/2006 hadi 2007/2008 wenye nia ya kutatua matatizo ya Sekta ya Sheria, upungufu wa Mahakimu ikiwa ni mojawapo. Aidha, ajira mpya ya Mahakimu, upanuzi wa Chuo cha Mahakama Lushoto na ajira ya muda ya Mahakimu Wastaafu ni mikakati mingine yenye nia ya kuhakikisha wananchi wanapata haki hiyo. Pale wananchi wa maeneo husika wanapoahidi kusafiri kwenda Ng'apa kwa usikilizaji wa mashauri yao ya madai, utaratibu wa kisheria ni kwa wao wenyewe walalamikaji au walalamikiwa kujigharamia kwa safari hizo.

(b) Hakuna posho inayostahili kulipwa Hakimu wa Ng'apa akisikiliza mashauri yatokayo Mahakama za Milola na Rutamba, kwa sababu Hakimu anakuwa kituoni kwake na anafanya kazi ndani ya muda wa kawaida wa kazi. Lakini anastahili kulipwa posho ya usafiri na ya kujikimu kwa kipindi anachokuwa nje ya kituo chake cha kazi.

(c) Hivi karibuni Mahakiama itaajiri Mahakimu 55. Mahakimu watakaoajiriwa watatawanywa katika Mahakama mbalimbali nchini kuzingatia uhaba uliopo kiwilaya. Hivyo, Mahakama za Milola na Rutamba nazo zitaweza kupata Mahakimu kwa kuzingatia kigezo hicho.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu na kwa kuwa tuna vijana wengi waliomaliza kidato cha nne, kidato cha sita, lakini hawana kazi. Je, Wizara hii ina vyuo vingapi ambavyo inaweza kuwafundisha Mahakimu ili tuweze kuwapata Mahakimu wengi zaidi? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa kazi ya Hakimu ni kazi nyeti. Je, Hakimu anayekaa katika kituo kimoja kwa zaidi ya miaka 20 Serikali haioni kwamba anaweza akasahau kutenda haki kwa kuzoea eneo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tuna matatizo ya upungufu wa Mahakimu na tunavyo vyuo ambavyo vinafundisha Sheria, zinatoa kwa wingi na sasa hivi niseme tu kwamba tungeweza kuwaajiri hao lakini inabidi wapitie katika Chuo chetu cha Lushoto, chuo ambacho kinafundisha maadili ya Uhakimu ni kimoja tu mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, tatizo kwa kweli lipo hapo kwamba tuna Chuo kimoja ambacho kinawafundisha hasa hao Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na nimesema kwamba tunatarajia kukipanua Chuo hiki. Hiyo ndiyo suluhisho.

Kuhusu Mahakimu kukaa muda mrefu katika maeneo yao, hii ni kweli ni tatizo ambalo tunalifahamu. Lakini kinachogomba hapa kwa kweli ni kutokuwa na fungu la kutosha la kuweza kuhamisha hamisha Mahakimu hawa kila baada ya miaka mitatu au mitano. Tukipata bajeti ya kutosha basi hili tatizo nadhani litakuwa limekwisha.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa kuwa hoja ya msingi ni tatizo la Mahakimu nchini hususan katika Mkoa wa Mtwara, mwaka 2003 nilishaandika barua nikieleza matatizo ya wazee Tarafa ya Chilangala wakilalamika hakuna Hakimu na huko Kitaya na mwaka 2004 nikarejea hiyo barua. Je, nauliza hao Mahakimu sasa hivi wameshapelekwa na kama wamepelekwa wamepelekwa lini?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu barua ambazo amekuwa akiniandikia. Ni kweli nadhani Ofisi yangu pia imekuwa ikijibu. Lakini ingekuwa vizuri zaidi Mheshimiwa Boma kupitia pitia kule Wizarani tukazungumza kwa karibu zaidi ili mambo haya yaweze kuniingia zaidi, na niweze kuyashughulikia kwa ipasayo. *(Kicheko)*

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize angalau swali moja la nyongeza. Kwa sababu tatizo hili la kesi za Milola na Rutamba kupeleka Ng'apa linajirudia kwenye maeneo mengi ikiwepo kwenye eneo la kwangu. Sisi kwetu kesi ya maeneo kama Namindondi, Ngunja na Namnala, watu wanaondoka maeneo yale kwenda Namikupa kilomita zaidi ya 50 mpaka 60, mpaka imefikia mahala watu sasa wamekata tamaa kufuatilia haki.

Sasa kama tunakubaliana kwamba utoaji wa haki ni sehemu ya msingi katika utawala bora. Hivi kama tumekubaliana tuboreshe miundombinu kwa kutenga karibu bilioni 8 kila mwezi. Hatuwezi kufanya mpango huu huu katika kuboresha utaratibu wa kuzalisha Mahakimu ndani ya nchi hii na tatizo hili likaondoka moja kwa moja?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuzalisha mahakimu na hasa kwa jimbo la Tandahimba. Nasema tunazo sera nyingi tulivyokuwa tunazungumza jana katika Semina hapa, tuna mambo mengi ya

kufanya. Kinachogomba nasema ni bajeti. Lazima tuwe na mpangilio wa shughuli zetu na kama nitakavyojibu swali linalokuja, tumezindua swali hili *actually* tumezindua mpango huu wa mkakati wa kufanya marekebisho ya Sekta ya Sheria na moja ni kipaumbele ni kuweza kuwatoa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wengi zaidi katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

**SPIKA:** Twende basi kwenye swali linalofuata, ili uweze kujibu hayo uliyoyasema.

Na. 52

**Mirathi**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ulipaji wa mirathi hufanyika katika mahakama zetu na kwa kuwa malipo ya mirathi hiyo yanapolipwa kwa msimamizi aliyeidhinbishwa na familia na hundi kuandikwa jina lake malipo hufanyika mapema zaidi lakini hundi ikiandikwa kwa jina la mahakama huwa ni kero ya kusubiri pesa kwa miaka miwili au zaidi kutokana na ukosefu wa fedha:-

(a) Je, kwa nini mahakama husumbua sana kama hundi ya mirathi ikiandikwa jina la mahakama husika?

(b) Kama mahakama haina fedha, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa usumbufu wa mirathi ili ilipwe kwa wakati?

(c) Kwa nini mahakama isitumie jina la msimamizi wa mirathi katika hundi lakini idhibiti ugawaji wa mirathi kwa wahusika?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa taratibu za Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Mahakama imepewa dhamana ya kuhakikisha kwamba warithi wote wananufaika na mali ya mirathi ya marehemu. Msimamizi wa mirathi ni mratibu tu wa utekelezaji wa mgao wa mali za marehemu. Mahakama nayo kwa upande wake ni mdhibiti tu wa mgao huo. Ili kuwa na udhibiti, Mahakama inayo akaunti ya mirathi na malipo yote ya mirathi huandikwa kwa jina la Mahakama ili yaingizwe katika akaunti kabla ya mgao. Nia ya Mahakama ni kuwalipa warithi stahili kwa haraka iwezekanavyo na hivi sasa malipo hufanyika kwenye Hazina Ndogo katika Mikoa badala ya Mahakama Kuu. Utaratibu ambao kwa sasa umerahisisha sana zoezi la ugawaji mali za marehemu.

(b) Mahakama wala Serikali haina fungu la fedha kwa ajili ya malipo ya mirathi. Fedha zinazolipwa kwa mirathi ni mali ya marehemu kutokana na vyanzo vyake mbalimbali.

(c) Hundi ikiandikwa kwa jina la msimamizi moja kwa moja, inaweza kuwa vigumu kwa Mahakama kuhakikisha kuwa kila mrithi amepata stahili yake. Msimamizi ambaye hundi ameandikiwa kwa jina lake hatalazimika kurudi Mahakamani ili Mahakama ihakikishe warithi wote wanapata haki yao. Upo uwezekano wa msimamizi kuchukulia fedha hizo kama mali yake na hivyo kutowalipa warithi na hivyo kuwaingiza warithi kwenye mgogoro na malalamiko ya muda mrefu na pengine warithi hao kutopata haki yao kabisa.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini kuhusu swali la (b) inavyoonekana *account* ya fedha zinazolipwa mirathi ya watumishi wa Serikali wanaofariki mara nyingi hundi zile huwa zina matatizo kwamba fedha hazipo kwenye *account* ya Mahakama na usumbufu ndipo unapoanzia. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni busara kutafuta jinsi ya kuweza kurahisha ili *account* hii iwe na fedha wakati wote kwa sababu zinalipwa kutoka Hazina?

Swali la pili, kwa sababu inaonekana Mahakama zimegubikwa gubikwa na woga wa wananchi kuhusu chombo hiki na wanaogopa mara nyingi wanapopata matatizo ya wananchi wao na ni ndugu zao wamefariki kwenda kufuatilia mirathi. Je, si vema Serikali au Mahakama ikatafuta Ofisi ambayo ingeweza kuwasaidia wananchi kutatua matatizo yao kabla hawajafikisha masuala haya katika Mahakama, kama vile Ofisi ya *DC* akiwasaidia ndipo waweze kufika Mahakamani kulipwa hayo malipo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo, ni hili ndani ya Mahakama zetu na Serikali. Lakini kwa utaratibu ambao tunao sasa hivi ndiyo huo kwamba Mahakama ina jukumu la kusimamia mirathi yenyewe. Lakini pesa kwa kweli za warithi zinashughulikiwa katika Hazina Ndogo huko Mikoani. Lakini nasema hili suala tunalitazama na ni moja ya masuala ambayo tunategemea kuyachambua wakati ambapo tutakuwa tuna hoja mbalimbali kwa maana ya hiyo mirathi yenyewe, ndoa, masuala ya watoto katika *White Paper* ambayo sasa hivi Serikali inaiandaa. Suala hili litatazamwa kwa kina wakati huo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wajane wengi wanapata shida kwa kupata mirathi na ni haki yao pamoja na watoto wao. Je, Serikali inaonaje kuweka sheria hii iwe *automatic* anapofariki mzazi mume, mke awe ndiyo msimamizi wa mirathi kwa kuhakikisha kwamba anapata haki yake hiyo kama mjane na watoto wake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli yapo matatizo hayo. Lakini cha msingi ni kwamba Mahakama ndiyo inayoweza kusimamia masuala hayo. Suala la mjane na hasa mwanamke pia inategemea kiasi gani

ambacho naye amechangia. Sasa kama umeingia pale siku moja tu unataka kuchukua mali ya mzee. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo lazima yazingatiwe na Mahakama ndiyo inaweza kuyasuluhisha kwa utaratibu unaofaa. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 53

**Huduma ya Maji - Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya maji ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, na kwa kuwa vijiji vya Mima, Mzase, Kimagai, Iyoma na Chunyu, Wilayani Mpwapwa, vinakabiliwa na tatizo kubwa la maji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia maji vijiji nilivyovitaja?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, kama vijiji hivyo vitapatiwa maji itasaidia sana maendeleo na uchumi wa vijiji hivyo?

(c) Kwa kuwa, benki ya dunia imefanya kazi nzuri sana ya kuboresha huduma ya maji Wilayani Mpwapwa.Je, Serikali ina mpango gani wa kuviweka vijiji hivyo katika miradi ya benki ya dunia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa huduma ya maji ni muhimu kwa maendeleo na uchumi wa nchi yetu. Aidha, maji ni muhimu kwa uhai na maisha ya viumbe vyote na hifadhi ya mazingira. Serikali inayo mipango ya kuboresha huduma ya maji vijijini kwa kutumia fedha zetu wenyewe pamoja na za kutoka kwenye vyanzo vingine, ikiwa ni pamoja na wafadhili. Ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika vijiji nchini, Serikali inatekeleza mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini, kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia, Wilaya ya Mpwapwa ni moja ya Wilaya ambapo mradi huo unatekelezwa hivi sasa. Katika mradi huo, Halmashauri za Wilaya zenyewe ndizo zinachagua vijiji vya kuingizwa kwenye mradi kulingana na vipaumbele vya vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilipanga kutekeleza mradi huo katika vijiji kumi vya Burege, Chaludewa, Chamtumile, Chipogolo, Chisegu, Igoji, Ikuyu, Mazaenje, Mtera na Sasima katika mwaka wa kwanza. Shughuli zilizofanyika ni uchimbaji wa visima virefu 4 ambavyo vinatumia mitambo inayoendeshwa na injini za dizeli, uchimbaji wa visima virefu 2 vinavyotumia mitambo ya umeme na ujenzi wa miradi 4 ya maji ya mtiririko. Jumla ya watu wanaofaidika kwa

mwaka wa kwanza ni 33,673 na gharama ambayo tayari iliyotumika ni shilingi 897,520,901/=. Vile vile vijiji vingine vitano vya Lupeta, Makutupa, Msagali, Pwaga na Seluka vilichaguliwa kutekeleza mradi katika mwaka wa pili. Miradi miwili ya mtiririko imekamilika, visima virefu 3 vimechimbwa na kazi bado inaendelea. Katika hatua hii, jumla ya watu 22,753 watafaidika na awamu ya pili kwa gharama ya shilingi 1,020,674,215/=. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imepanga kutekeleza mradi huu katika vijiji vya Mima, Mzase, Kimagai, Iyoma na Chunyu katika mwaka wa tatu ambao ni 2006/07.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, nina maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa huu mradi wa kijiji Igoji Kusini Salaza, ulikamilika na kwa kuwa hivi karibuni zaidi ya mabomba 10 yalichukuliwa na maji. Hivi sasa vijiji hivi havina huduma ya maji. Ogoji Kusini Salaza, Simai pamoja na Chamanda. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kutuma wataalam wake ili kuhakikisha kwamba wanakarabati mabomba hayo, wananchi waweze kupata huduma ya maji?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali ikishirikiana na Shirika la msaada la Ufaransa wana mpango mkubwa wa kuboresha huduma ya maji Mpwapwa Mjini, kwa gharama ya shilingi milioni 700. Je, mpango huo utaanza lini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Mbunge anaelewa kwamba ujenzi wa miradi hiyo ambayo inafadhiliwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia inafanyika kwa kusimamiwa na Halmashauri ya Wilaya na mikataba inayotumika ni ile ambayo imesainiwa kati ya Halmshauri ya Wilaya na Mkandarasi. Na katika mikataba hiyo nina hakika kuna vifungu vinavyotaka au vinavyotoa uthibitisho wa *guarantee* baada ya mradi kutekelezwa. Kwa hiyo, nina hakika kwa vile mradi huo wa kijiji anachokielezea Mbunge umefanyika hivi karibuni nina hakika kwamba mkataba ulitakiwa kutambua *guarantee* hiyo na mkandarasi anawajibika kwenda kufanya marekebisho na kama haikufanyika hivyo ina maana Halmashauri ya Wilaya ina jukumu la kusimamia mradi huo kwa sababu ni mradi ambao tayari tumeukabidhi kwao.

Hili swali la kuhusu msaada ambao unatarajiwa kufika kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji wa mji mdogo wa Kijiji cha Mpwapwa, nina hakika mambo yatakapokuwa tayari Mheshimiwa Mbunge atafahamu na mradi utatekelezwa nina hakika taratibu sasa hivi bado zinaandaliwa. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Katika utekelezaji wa mradi huu wa usafi wa mazingira wa huduma ya maji vijijini, Wilaya ya Kongwa pia ipo katika awamu ya kwanza na awamu ya pili. Katika awamu ya kwanza vijiji vya Mbande, Manungwi, Iduo, Pandambili, Tububwe, Chamai, Liganga na Mautya vilikuwa vimekubaliwa kwamba navyo ziwemo katika huduma hiyo. Sasa kwa kuwa sasa tuko katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi, lakini hata kijiji kimoja katika vijiji vya awamu ya kwanza vya

Kongwa hakijapata maji hadi hivi sasa ninavyoongea. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, Vijiji hivyo vya awamu ya kwanza Serikali inatoa ahadi gani lini watapata huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Mbunge anaelewa kwamba miradi hiyo kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi linasimamiwa na Wilaya na maendeleo yake Mheshimiwa Mbunge anayafahamu zaidi kuliko hata sisi. Kwa hiyo, nina hakika kulingana na mapatano walio nayo na Mkandarasi na Idara ya Maji ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, nina hakika utaratibu huo wote na mtiririko wote huo unaeleweka kwa Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, naomba tu awahimize wasimamizi wa mradi huo waweze kukamilisha kama walivyokubaliana katika mkataba. Na kama kuna matatizo mengine ya kifundi nitamwomba Mheshimiwa Mbunge awaeleze au awaombe Halmashauri ambao ni wasimamizi watuletee rasmi Ofisini kwetu ili tuone tatizo liko wapi. Na nina hakika mradi huu utakamilishwa kama ulivyopangwa.

Na. 54

**Mradi wa Maji Toloha**

**MHE. JOHN E. SINGO (K.n.y. MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE)** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa maji wa Toloha Wilayani Mwanga ulijengwa na kukamilika mwaka 1956 na kwa kuwa mabomba ya mradi huo yamechakaa kabisa:-

Je, Serikali itakubali mwaka huu kutengeneza upya mradi huo ili wananchi wapate huduma ya maji safi na kuondokana na tishio la magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Professa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mradi wa Maji wa Toroha ni mkachavu kutokana na umri wake kwani ujenzi wake ulianza mwaka 1952 na kukamilika mwaka 1956. Mradi huu una urefu kilometa 15 na mabomba yalitumika kwenye mradi huu ni ya chuma kwa sehemu kubwa ambayo kwa sasa yamechakaa. Ni sehemu kidogo tu ya mradi huu imefungwa kwa bomba za plastiki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003 Wizara iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga shilingi milioni nne kwa ajili ya ukarabati mradi huo. Halmashauri ilikarabati sehemu zilizokuwa zimeoza zaidi kwa kubadilisha bomba za chuma na kuweka bomba za plastiki zenye urefu wa kilometa 1.2. Aidha, nguzo zilijengwa ili kuzuia mabomba yasichomoke katika maeneo yenye miteremko mkali. *(Makofi)*

Wakati huo huo Wizara yangu ilitoa shilingi 470,000/= pamoja na mabomba ya plastiki yenye thamani ya shilingi 870,000/= kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kwa ajili ya kupeleka maji kwenye Kitongoji cha Kwakihindi katika Kijiji cha Toloha. Halmashauri pia inaendelea na mpango wake wa kupeleka maji kwenye Kitongoji cha Gongoni hapo kijijini kwa gharama ya shilingi 1,160,000/=. Tayari wananchi wamepimiwa mtaro na wameanza kuchimba kwa kushirikiana na wahandisi. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika mradi huu, Halmashauri ya Mwanga inakarabati pia birika la kunyweshea mifugo katika kijiji cha Toloha.

Mheshimiwa Spika, ili kukarabati mradi katika sehemu iliyobaki yanahitaji mabomba ya plastiki yenye kipenyo cha inchi 2 na urefu wa kilometa 11. Kutokana na ufinyu wa Bajeti yake, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imepanga kubadilisha mabomba kwa awamu kila mwaka kuanzia mwaka ujao wa fedha. Wizara yangu itasaidiana na Halmashauri ya Wilaya katika kutekeleza mradi kwa awamu kama ilivyopangwa ili kuwaweza wananchi kupata maji safi na salama. Na hivyo kuwaondolea kero ya magonjwa ya kuambukizwa kama vile, kipindupindu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mchango mkubwa wa Wizara katika mradi huu wa maji wa Tolowa. Lakini pamoja na juhudi za Wizara nzuri katika kusaidia mradi huu.

Je, kwa kuwa wananchi wako tayari kuchangia nguvu zao ili mradi huu huweze kukamilika. Wizara inafikiri mradi huu utakamilika lini ili wananchi wapate matumaini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Singo, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza wananchi kweli wanajitolea na sasa hivi wanahusika katika kuchimba mtaro. Na pia nimeeleza kuwa kuanzia mwaka ujao wa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imejipangia kuanza kurekebisha sehemu iliyobaki ya kilometa 11. Vile vile Serikali kulingana na upatikanaji wa fedha, tutazidi kusaidia kama tulivyofanya kwenye ile kilometa 1.2 pamoja na mabomba ambayo tuliwapatia ili kazi hii ifanyike.

Na. 55

**Ujenzi wa Barabara Jijini Dar es Salaam**

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam likiwemo na Jimbo la Ukonga linaendelea kuongezeka kwa kasi kubwa na kusababisha uhitaji mkubwa wa miundombinu hasa ya barabara na kwa kuwa mahitaji ya ukarabati na ujenzi wa barabara mpya unaendelea kuwa makubwa kuzidi uwezo wa Bajeti za Manispaa tatu za Jiji hilo kimapato.

(a) Je, Serikali itakubali kutenga Bajeti mahusi kwa Manispaa hizo kwa ajili ya ukarabati/ujenzi wa barabara nje ya Bajeti ya kawaida ya *Road Toll* inayotolewa sasa ambayo ni ndogo sana?

(b) Kwa kuzingatia mazingira ya kijiografia ya Jiji la Dar es Salaaam je, Serikali itakubali kuivunja *TANROADS* - Mkoa wa Dar es Salaam ili Bajeti nzima ya sasa ya *TANROADS* ya Mkoa huo iwe inapelekwa katika Halmashauri ya Jiji hususan katika Manispaa zake tatu ambako zinaweza kupangwa vizuri zaidi kwa manufaa/mahitaji halisi ya wananchi wa Jiji kwa Madiwani na Wabunge?

(c) Kwa kuwa, Manispaa ya Ilala kutokana na ufinyu wa Bajeti imeshindwa kukarabati/kutengeneza barabara zake nyingi hasa zinazotoka katika barabara kuu ya Nyerere - Pugu kuingia kwenye Kata za Vijiji ambako kuna ongezeko kubwa sana la watu. Je, Serikali Kuu itakubali kutoa haraka angalau kiasi cha shilingi bilioni moja zinazohitajika kwa haraka kwa ajili ya kutengeneza kwa kiwango cha changarawe barabara tatu za Banana - Kitunda Ukonga (Mombasa) - *Moshi Bar* na Gongo la Mboto - Majohe (Mji Mpya) ambazo zimekuwa kero kubwa kupita kiasi kwa wananchi wapatao 80,000 wanaotumia njia hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makorongo Mahanga , Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Jiji la Dar es Salaam linakuwa kwa kasi kubwa kutokana na ongezeko la watu na hivyo kusababisha uhitaji mkubwa wa huduma mbalimbali za jamii zikiwemo miundombinu ya barabara, maji, umeme, vituo vya afya, shule, Mahakama na kadhalika. Kwa kutambua hilo Wizara yangu imekuwa ikisaidia/kuchangia kujenga/kukarabati barabara mbalimbali za Jiji/Manispaa za Dar es Salaam pale hali ya kifedha inaporuhusu.

Baadhi ya barabara hizo zilizojengwa na kukamilika hivi karibuni ni za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sehemu ya Mlimani na Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya cha Muhimbili ,bararaba za kwenda kwenye Hoteli za Kitalii zilizopo kwenye fukwe za Jangwani na Kunduchi, barabara ya kwenda kwenye Hospitali ya *Regency Medical Centre.*

Wizara yangu itaendelea kujenga/kuchangia miradi mbalimbali ya barabara za Jiji na Manispaa za Dar es Salaam kulingana na uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. Hata hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri husika ili nao wapange vipaumbele vya barabara za kujenga kutokana na vyanzo vyao vingine vya fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, *TANROADS* ni Wakala wa Barabara Tanzania chini ya Wizara ya Ujenzi ilioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya *Road Toll Amendment Act No.*

*2 (1998)* na Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997. Kazi kubwa ya Wakala wa Barabara ni kuendeleza na kufanyia matengenezo mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa nchini ambazo zipo chini ya Wizara ya Ujenzi. Mkoa wa Dar es Salaam una mtandoa wa barabara kuu na za Mkoa zenye jumla ya urefu wa kilometa 712.04 ambazo zinahudumiwa na Ofisi ya *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam.

Kutokana na majukumu yaliyotajwa *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam haiwezi kuvunjwa na Bajeti nzima kupelekwa katika Halmashauri ya Jiji na Manispaa zake, kwani Ofisi hiyo inajukumu lake lililowekwa kisheria na pia inawajibika kwa Wizara ya Ujenzi kuendeleza na kufanya matengenezo mtandao wa barabara nilizozitaja hapo juu. Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake tatu zishauriwe kuweka mikakati bora ya maendeleo na matengenezo ya barabara zake kwa kutumia fedha za Mfuko wa barabara na zile zitokanazo na vianzo (makusanyo) mbalimbali kwa ubora zaidi.

(c) Mheshimiwa Spika, Barabara za Banana - Kitunda Ukonga (Mombasa) hadi *Moshi Bar* na Gongo la Mboto - Majohe (Mji Mpya) zinazohudumiwa na Halmshauri ya Manispaa ya Ilala. Kwa sasa Wizara yangu , kutokana na ufinyu wa Bajeti haiwezi kutenga fedha kwa jili ya babarabara hizo.Hivyo kama nilivyoshauri katika (a) hapo juu, Manispaa ya Ilala itoe kipaumbele cha matengenezo ya barabara hizi kwa kutumia fedha zake za Mfuko wa Barabara, fedha za ruzuku ya barabara za zile fedha zitokanazo na vyanzo vyake vya makusanyo mbalimbali.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(1) Kwa sababu bado mpaka sasa kuna mkanganyiko mkubwa wa majukumu kwa maana ya barabara zinazohudumiwa na *TANROADS,* Jiji na Manispaa za pale Dar es Salaam. Na kwa sababu wananchi kwa kweli wa kawaida hawajui barabara zipi pale Dar es Salaam ni za Mkoa, Wilaya au Barabara Kuu.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufikiria hoja yangu hata ikibidi kubadilisha Sheria ya *TANROADS* ili kwa mahsusi kwa Dar es Salaam ambayo kijiografia kama nilivyosema kuna mkanganyiko iangalie uwezekano wa kuweka chombo kimoja tu cha kushughulikia barabara zote?

(2) Kwa sababu kama nilivyosema katika swali langu la (C) barabara hizo za Jimbo la Ukonga kwa kweli kimezidi uwezo wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Na barabara hiyo kwa mfano barabara ya Banana - Kitunda, Ukonga (Mombasa) *Moshi Bar* pamoja na Gongo la Mbota - Majohe zimekuwa mbaya pamoja na zingine. Na kwa kweli zinatishia hata kura zangu. Lakini vile vile zinatishia kura za Serikali iliyoko madarakani. *(Kicheko)*

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kusaidia Manispaa ya Ilala ili kwa kweli hizi kura za wananchi wa Ukonga ambao mpaka leo watakuwa wamejiandikisha 320,000 tuweze kuzipata na waweze kupata barabara imara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

(1) Linahusu kwamb barabara za Dar es Salaam zina mkanganyiko wa kueleweka zipi za *TANROADS* na zipi ambazo zisizo, hii nitamwaahidi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Dar es Salaam kwamba tutawagawia *list* ya kujua ni zipi barabara za Dar es Salaam zinahudumiwa na *TANROADS* ili kusiwe na mkanganyiko huo. *(Makofi)*

(2) Kuhusu barabara zinazotishia kura za Mheshimiwa Mbunge wa Ukonga na Serikali iliyopo madarakani, suala la barabara nchi nzima naweza kusema ni gumu sana hasa kwa sasa hivi mvua zinavyonyesha. Na kama tukisababisha/kutumia hiki kama ndicho kigezo cha kubadilisha Sheria iliyounda *TANROADS* tuibomoe sasa iwe *TANROADS* ya Dar es Salaam tu. Mwanza nao watadai kuwe na *TANROADS* ya Mwanza tu na Tanga nao pia watadai *TANROADS* ya kwao. Waheshimiwa Wabunge mimi naomba tustahimili tutumie chombo hicho cha *TANROADS* kukarabati barabara kuu na barabara za Mkoa na bararaba nyinginezo tuende hivyo hivyo tunavyojiweza kufuatana na uwezo wetu wa Bajeti *(Makofi)*

Na. 56

**Barabara ya Dar es Salaam - Mingoyo**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. BERNARD K. MEMBE)** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi - Mingoyo ilitegemewa kumalizika kujengwa mwaka 2005, kabla ya kumalizika kwa kipindi cha Awamu ya Tatu ya uongozi; na kwa kuwa macho ya wakazi wa Mkoa wa Lindi yanaona kuwa ujenzi huo unasuasua.

(a) Je, Serikali inaweza kusema sababu za kusuasua huko?

(b) Je, ni lini hasa barabara yote itakuwa imekamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernard K. Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi hadi Mingoyo yenye urefu wa kilometa 508 inaunganisha Mikoa ya Kusini Mashariki na Jiji la Dar es Salaam. Chini ya mpango wa ujenzi wa barabara hii, miradi mitano ya ujenzi inaendelea kwa awamu tofauti kwa lengo la kuikamilisha kwa kiwango cha lami katika mwaka wa

fedha wa 2006/2007 na si mwaka 2005 kama muuliza swali alivyosema. Maendeleo ya ujenzi wa miradi hii inatofautiana toka mradi mmoja hadi mwingine kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Dar es Salaam hadi Kibiti (kilometa 135): Kilometa 90 zimekamilika kwa kiwango cha lami, sehemu iliyobaki ya kilometa 45 mazungumzo kati ya Serikali ya *Kuwait Fund* yanaendelea ili sehemu hiyo iweze kukamilishwa na Wizara kupitia *TANROADS.*

(ii) Sehemu ya Daraja la Mkapa (kilometa 13.9): Sehemu hii imekamilika na kufunguliwa na gharama shilingi bilioni 35 zimetumika.

(iii) Sehemu ya Ndundu - Somanga (kilometa 60): Mradi huu utajengwa kwa fedha za mkopo kutoka *Kuwait Fund* na *OPEC.* Usanifu wa mradi huu umeanza Novemba, 2004 na unafanywa na Kampuni iitwayo *Parkman* ya Uingereza na ujenzi umepangwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu wa 2005.

(iv) Sehemu ya Somanga - Masaninga na Bonde la Mto Matandu (kilometa 33) na daraja la Matandu. Mradi huu ulikamilika mwezi wa Februari, 2005 kwa gharama ya Shilingi bilioni 13.9 zilizotolewa na Serikali ya Tanzania na mradi umefunguliwa na Mheshimiwa Rais.

(v) Sehemu ya Nangurunguru - Mbwemkuru (kilometa 95): Mradi huu unatekelezwa chini ya utaratibu wa usanifu na ujenzi kwa pamoja *(Design na Build).* Kimkataba mradi umepangwa kukamilika mwezi wa Oktoba, 2005. Lakini kutokana na Mkandarasi kuchelewa kukamilisha usanifu ndani ya kipindi cha miezi sita, Mkandarasi ameagizwa na amerekebisha mpango wa kazi kwa kuajiri Mkandarasi wasaidizi wawili *(Sub-contractors)* na ameongeza vifaa zaidi vya ujenzi ili kuongeza kasi ya utekelezaji. Gharama ya mradi mzima ni Shilingi bilioni 40.328 na zitatolewa na Serikali ya Tanzania.

(vi) Sehemu ya Mbwemkuru - Mingoyo (kilometa 95) - gharama ni shilingi bilioni 52.6 za kitanzania.

Mradi huu pia unatekelezwa chini ya utaratibu wa usanifu na ujenzi kwa pamoja yaani *Design and Build* kama ilivyo mradi wa Nangurukuru - Mbwemkuru. Kimkataba mradi umepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2005. Kutokana na Mkandarasi kuchelewa kufanya maandalizi muhimu *mobilization* ndani ya kipindi cha miezi sita. Mkandarasi ameagizwa na ametekeleza yafuatayo ili kukamilisha mradi katika muda wa mkataba.

(1) Mkandarasi amekwisha wasilisha mpango mpya wa kazi baada ya kuongeza vifaa na mitambo ili kongea kasi ya utekelezaji.

(2) Mkandarasi ameagiza vifa vingine kutoka nje ya nchi.

(3) Mkandarasi ameajiri Makandarasi wasaidizi wawili *Sub-con tractors* ili kuongeza nguvu ya utekelezaji na wameishaanza kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara yote kutoka Dar es Sa laam hadi Mingoyo kupitia Kibiti, Nangurukuru na Lindi utakuwa umekamilika mwaka wa fedha wa 2006/2007 kama nilivyofafanua hapo juu.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba niulize kama ifuatavyo:-

(1) Kuna baadhi ya sehemu yeye mwenyewe amezitaja ambazo kasi ya ujenzi inakwenda pole pole mno hasa sehemu hiyo Mingoyo, Lindi - Nangurukuru. Sisi wananchi wa Kusini tunavyoona sehemu ile kuna vifaa vingi lakini utendaji wa kazi unakwenda taratibu mno. Tulikuwa tunauliza Wizara hivi itasimamia kwa namna gani kuhakikisha kwamba kasi hii inaongezeka na kazi hii inakamilika hapo mwezi Oktoba?

(2) Hivi karibuni tumesikia kwenye vyombo vya habari kwamba kuna matatizo ya utapatikanaji wa fedha kutoka *Kuwait Fund* ambayo Mheshimiwa Waziri hakuwahi kutueleza hapa. Tungeomba atueleze matatizo hayo ni nini na kama yatakwamisha utekelezaji wa mradi huu. Je, Serikali haingefikiria kwa sasa hivi kuanza kutumia fedha zake wenyewe ili tuweze kufanya kazi hii na Kuwait watakapokuja kulipa baadaye pesa tuweze kurekebisha ipasavyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mrope kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika eneo la barabara ambalo amelijitaja kutoka Mbwemkuru - Lindi hadi Mingoyo, ambayo ameeleza kwamba kazi zake zinaenda taratibu na kwamba inatokana labda na matatizo ya fedha za *Kuwait Fund.*

Kwanza nataka kumthibitia Mheshimiwa Mrope kwamba barabara ya kutoka Nangurukuru - Mbwemkuru hadi Mingoyo, ambapo kuna zaidi ya kilometa 180 inalipiwa fedha kwa asilimia mia na Serikali ya Tanzania. Kwa hiyo, hapo hatutegemei fedha za *Kuwait Fund. (Makofi)*

Katika maelezo ambayo ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza kuna hatua ambazo zimechukuliwa katika hayo Makampuni mfano Kampuni ya *SICO* ambayo inajenga kati ya Nangurukuru - Mbwemkuru na Kampuni ya *Ms Karafi and Sons* inayojenga kati ya Mbwemkuru - Lindi hadi Mingoyo. Katika hatua hizo ambazo zimechukuliwa mmoja ni ku-*sub-contract* baadhi ya kazi wameongeza pia baadhi ya vifaa ili kuhakikisha kwamba kazi zinakamilika kwa wakati uliyopangwa. Wasipokamilisha katika mwezi wa Oktoba, tutaanza kuwakata *liquidations* ili kusudi wajue ukandarasi ni tofauti na kutengeneza gongo. *(Kicheko)*

Lakini katika suala la *Kuwait Fund. Kuwait Fund* ni kweli tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa *Kuwait Fund* katika eneo la kilometa 45 zilizobaki kati ya Barabara ya Dar es Salaam - Kibiti ambayo ina jumla kilometa 135 zimebaki kilometa 45 ambazo zinatakiwa kukamilika. Mazungumzo haya yakishakamilika, hilo eneo nalo litaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kusini kwamba barabara hiyo yote ya kutoka Dar es Salaam - Mtwara, itakuwa imekamilika kufika mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Na. 57

**Hifadhi ya Misitu ya Asili**

**MHE. MUSA A. LUPATU** aliuliza:-

Kwa kuwa misitu ya asili ikihifadhiwa ni chanzo kizuri cha mvua na mazingira mazuri; na kwa kuwa, katika maeneo ya milimani Wilayani Korogwe, hasa katika Tarafa ya Bungu iko misitu ya asili ambayo iko ndani ya maeneo ya mashamba makubwa ya chai yanayomilikiwa na Kampuni binafsi na maeneo ya Kanisa.

Je, Serikali ina mamlaka gani katika kusimamia hifadhi ya misitu hiyo ya asili?
**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, misitu iliyoko ndani ya maeneo ya mashamba makubwa ya chai yanayomilikiwa na Kampuni binafsi na maeneo ya Kanisa yanasimamiwa na Kampuni na makanisa husika kwa kuwa ni misitu yao binafsi.

Hata hivyo, Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002 (Kifungu Na. 15(1) ambayo imeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 inawataka watu, Mashirika na Taasisi binafsi zinazomiliki eneo la msitu linazidi hekta 50 ziandae mpango wa Usimamizi yaani *management plan* unaozingatia madhumuni ya kuhifadhi msitu husika na jinsi utakavyotekelezwa. Mpango huu ni lazima uridhiwe na Serikali (Mkurugenzi wa Misitu) na mmiliki anatakiwa ausimamie msitu husika kwa mujibu wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Misitu, Serikali itakuwa na mamlaka ya kufuatilia ili kuhakikisha kuwa misitu ya binafsi inasimamiwa kwa misingi

ya Mpango wa Usimamizi ulioridhiwa na Serikali. Napenda kuyapongeza na kuyashukuru Makampuni ya Chai ya Ambangulu na Dindira na Kanisa la KKKT Lutindi yanayomiliki misitu Wilayani Korogwe.

Kampuni ya Chai ya Ambangulu inamiliki hekta 772 wakati Kampuni ya Chai ya Dindira inamiliki hekta 200 na KKKT Lutindi wanamiliki hekta 100 za misitu ya asili. Misitu hii inatoa mchango mkubwa katika kuhifadhi vyanzo vya maji katika maeneo husika.

Serikali inapenda kuhimiza wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Makampuni na madhehebu ya dini wahifadhi misitu kwa ajili ya kukidhi mahitaji na huduma zitokanazo na misitu.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

(1) Kwa kuwa, katika Shamba la Dindira eneo hilo linazozungumzwa kwamba ni la misitu inahifadhiwa limekatwa ule msitu kwa kiwango kikubwa na kuharibu sana mazingira. Kwa kisingizio kwamba wanalipa kodi ya ardhi.

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa hiyo kodi ya ardhi kwa eneo hilo kusudi waweze kuwa na kauli?

(2) Kwa kuwa, eneo hilo limeharibiwa sana. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Makampuni haya kuhusu kurudisha au kurejesha uoto huu wa asili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Lupatu Mbunge wa Korogwe Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilieleza hapo awali kwamba utaratibu wa matumizi na misitu hii ni kuwa na *Management Plan* (Mpango wa Matumizi). Na suala ambalo Mheshimiwa Lupatu analieleza la kwamba maeneo yameharibiwa nikiri kwamba sina taarifa nalo. Lakini tutafuatilia na tutaangalia *Management Plan* yao iko namna gani. Kwa sababu kuna utaratibu ambao pengine wanakata miti lakini na kupanda miti. Na pengine miti ile ambayo inatumika labla kukausha chai katika maeneo yale. Lakini napenda kumhaadi Mheshimiwa Lupatu kwamba mimi nitalifuatilia suala hili. *(Makofi)*

Na. 58

**Kilimo cha Vanilla**

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO (K.n.y. DR. DIODORUS B. KAMALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Kagera wameitikia kwa wingi wito wa kuwa na mazao mengi ya biashara na kwamba baadhi ya wakulima wameanza kilimo cha zao la Vanilla.

Je, Serikali imechukua hatua zipi za kuwasaidia wakulima wa zao la Vanilla?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Vanilla ni zao jipya sana nchini na limeanza kupata umaarufu kutokana na kuwa na bei nzuri. Hivi sasa zao hilo linazalishwa kibishara katika Mkoa wa Kagera. Katika mwaka wa 2003/2004 kulikuwa na wakulima 3,040 wenye mashamba yanayokadiriwa kuwa na jumla ya hekta 113 ambayo yalitoa kilo 5,069 ya vanilla mbichi. Katika msimu wa 2004/2005 wakulima 6,000 wanatarajiwa kuzalisha kilo 6,000 za vanilla mbichi kutoka kwenye hekta 200 za vanilla.

Ili kusaidia wakulima kuongeza tija, uzalishaji na kipato, Serikalli inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Serikali imetoa leseni kwa wanunuzi watatu wa zao la vanilla ili wakulima wapate soko la uhakika wa zao hilo. Wanunuzi hao ni *Al-Mashirick General Traders Ltd, Kagera Vanilla Farmers Association Tanzania* na Chama cha Maendeleo ya Wakulima Kagera.

(ii) Serikali inatoa mafunzo kwa wakulima na wataalam wa kilimo katika maeneo mengine yanayoweza kustawisha zao hilo nchini. Hadi mwaka 2003/2004 jumla ya wakulima wakufunzi 34 kutoka kwenye Mikoa ya Mbeya, Pwani, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam walipatiwa mafunzo kwa lengo la kuwawezesha kutoa mafunzo ya kilimo bora cha Vanilla kwa wakulima wenzao.

(iii) Serikali inahimiza wakulima kujiunga katika vikundi vya uzalishaji ili waweze kupatiwa huduma za upatikanaji wa soko na mafunzo ya kilimo bora cha Vanilla. Hadi sasa kuna vikundi 46 vya wakulima wa zao hilo nchini.

(iv) Serikali inafanya utafiti wa Vanilla ni kubaini mbinu bora za kuongeza tija na uzalishaji, kupambana na wadudu na magonjwa na mbinu za kuzalisha vipando vya zao hilo kwa wingi na kwa haraka zaidi.

Utafiti huo unaendelea katika vituo vya utafiti vya Maruku Mkoani Kagera Katrin Mkoani Morogoro na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA) Morogoro.*

(v) Wizara inaandaa kajitabu juu ya kilimo cha Vanilla ambacho kitawaelekeza wananchi wanaotaka kulima zao hilo linavyolimwa.

Na. 59

**Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugonjwa wa malaria ni hatari sana na unazidi kuendelea kwa kasi kubwa, na kwa kuwa, ili mgonjwa athibitike kuwa ana vimelea vya malaria katika damu yake ni lazima ichukuliwe damu yake ikapimwe kwa kutumia darubini ambazo zinatumika kwenye hospitali nyingi za Serikali na za binafsi na kwenye vituo vya afya vilivyopo vijijini na kwa kuwa inatokea mara nyingi kuwa mtu akipimwa kwa siku hiyo hiyo kwa nyakati tofauti yanatokea majibu tofauti.

(a) Je, ni kwa nini kunatokea majibu tofauti kwa damu ya mtu huyo huyo?

(b) Je, Serikali inazifanyia ukaguzi darubini hizo na ni wangapi wamethibitika kutumia darubini zisizo na majibu sahihi na wamechukuliwa hatua gani hasa ikitiliwa maanani kuwa majibu tofauti ya vipimo yanaweza kumwathiri mhusika kulingana na dawa atakazopatiwa kufuatia majibu yaliyotolewa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Mariam Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa malaria ni ugonjwa hatari na unaenea kwa kasi. Aidha nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ili kudhibiti kuwepo kwa malaria kwa mgonjwa ni lazima damu ya mhusika ipimwe ili kubainisha kuwapo kwa vimelea vya malaria kwenye damu.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, kutofautiana kwa majibu ya vipimo kwa mtu mmoja kwa nyakati tofauti kunaweza kusababishwa na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

* Inawezekana wakati mgonjwa anapochukuliwa damu vimelea vya malaria vinaweza kuwa havipo katika mzunguko wa damu hivyo mpimaj hawezi kuviona vimelea hivyo kwa njia ya darubini. Pia mgonjwa huyo huyo baada ya kipindi atakapokwenda kwa mpimaji na kuchukuliwa damu kuna uwezekano wa vimelea kuonekana.

* Wakati mwingine mgonjwa huwa ametumia dawa chini ya kiwango kinachohitajika kabla ya kupima hivyo kufanya vimelea visionekane kwa wakati huo. Nguvu ya dawa inapopungua vimelea huonekana tena kwenye damu.

*	Makosa ya mpimaji kutokana na kutokuwa na ujuzi wa kutosha kutofahamau vizuri utayarishaji wa vipimo yaani *blood slide preparation.* Au vifaa vya kupimia visivyokidhi viwango huweza kusababisha vimelea kutoonekana. Wizara yangu imeanzisha mpango wa mafunzo ya kuwapiga msasa Watumishi wote wanaohusika na matibabu ya malaria chini ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria.

(b)	Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inacho Kitengo cha Ukaguzi ambacho hutembelea vituo vya huduma na kukagua vifaa vya tiba vyote zikiwemo darubini. Kazi hii hufanyika mara kwa mara na vile vibovu hutengenezwa.Aidha, Maabara za watu Binafsi hukaguliwa na Msajili wa Maabara Binafsi. Kwa mfano mwaka 2003/2004 jumla ya Maabara Binafsi 338 zilikaguliwa. Kati ya hizo Maabara 110 zilifikia viwango na 208 hazikufikika viwango.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Maabara 83 kuelekezwa kufanya marekebisho; Maabara 110 zilifungwa na Maabara 16 zilifungwa na wamiliki wake kupelekwa Mahakamani.

Aidha, Mheshimiwa Spika, Bodi ya Maabara Binafsi imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa Mameneja wa Maabara wa Kanda za Mashariki, Kaskazini, Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati. Kanda ya Ziwa itaanza mafunzo mwezi Mei, 2005. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mfaki umeridhika, nashukuru na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Kuna tangazo la Kamati mbili zinazokutana leo:

(1)	Ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti anaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo ya Uwekezaji na Biashara wakatane saa 4:30, tuseme mara baada ya kipindi hiki cha Maswali katika ukumbi 231, ghorofa ya pili.

(2)	Ni Kamati ya Uongozi naomba Kamati ya Uongozi tukutane katika *lodge* ya Spika, vilevile mara baada ya Maswali. Hii ni kwa sababu tumepata ombi la kufanya semina muhimu ya Wabunge wote, na hatukuwa tumeipangia nafasi lakini ni muhimu ifanyike tumeambiwa na Serikali, ni muhimu ifanyike. Kuhusu ripoti ya Kamati ya Afrika Mashariki iliyopendekeza mwendo wa kasi kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki yaani *East African Community Report of the Committee on Fast Tracking East African Federation).*

Waheshimiwa Wabunge tulishawagawia hizi nadhani mkutano uliopita, kwa hiyo kwa kuwa kuna semina inakuja kama kuna Mheshimiwa ana nakala yake karibu bora aipitie tena, vinginevyo ziko kwenye maktaba yetu kujikubusha, kujiandaa na semina kwa siku itakayopangwa na Kamati ya Uongozi hii leo. Ni lazima tupange kwa sababu BAKWATA wametutangazia jana kwamba siku ya Ijumaa wiki hii itakuwa ndio siku ya Maulidi. Mwanzoni tulidhani ni Alhamisi. Kwa hiyo, tukawa tumepanga shughuli za kufanya Ijumaa. Sasa Ijumaa itakuwa ni sikukuu na kazi za Serikali ambazo bado ziko

zitakuja kwenye *Order Paper* ni Muswada huu unaoisha leo na halafu kuna Miswada mingine miwili ya Wizara ya Ushirika na Masoko, lazima tuimalize na kuna Maazimio ya Kuridhia. Kwa hiyo, itabidi kazi hizo tuzifanye mpaka Alhamisi tukamilishe halafu wiki ijayo tulipanga shughuli zisizokuwa za Serikali. Taarifa za Kamati, hoja binafsi na mengine

Kwa hiyo, inabidi Kamati ya Uongozi ikae ili tupange upya namna tutakavyo kamilisha shughuli za mkutano huu wa kumi na tisa. Sasa Mheshimiwa Ali Said Salim, aliomba mwongozo wa Spika, nikamkatalia kwa msingi wa kanuni zetu. Ngoja nimbushe kanuni inasema nini kuhusu kuomba mwongozo wa Spika. Ni kanuni 55 kifungu kidogo (3) kinasema: " Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema, na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema katika kikao cha siku hiyo. Kwanza kuwe hakuna Mbunge mwingie anasema na liwe limshatokea katika kikao cha siku hiyo. Sasa Mheshimiwa Ali Salim yeye amesimama wakati Spika anazungumza na yeye amekosea kifungu cha (1) halafu pili amesimama mwanzoni kabisa hata hatujaanza shughuli yoyote anataka mwongozo juu ya jambo gani. Kanuni inataka iwe ni jambo lililotokea katika kikao hichi. Sasa la kwake haiwezekani kwamba lingekuwa limetokea hata kabla hata hatujaanza. Kwa hiyo, ndio maana nikakukatalia Mheshimiwa Ali Salim ni kwa mujibu wa kanuni zetu.

Wachangiaji ili wajiandae wanne wa mwanzo au watano wa mwanzo watakuwa ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa John Singo. Wasiende mbali ndio watakuwa wanachangia mwanzoni hapa. Baada ya maelezo hayo sasa tunaendelea na shughuli za Bunge. Lakini namwomba Mheshimiwa Mwenyekiti Anna Makinda aje anipokee kiti ili mimi nikaongoze Kamati ya Uongozi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, namwona hayupo, Prof. Juma Mikidadi, tunasubiri kwanza. Tusubiri dakika chache Wabunge watoke wanaokwenda kunywa chai.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa Mwaka 2005 *(The Rural Energy Bill, 2005)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Prof. Juma Mikidadi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri.

**MHE. PROF. JUMA MTUPA MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza leo kuchangia Muswada ulio mbele yetu, kuhusu Umeme Vijijini. Kabla ya kuchangia napenda kutoa salam zangu za rambi rambi

kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza kusimama Bungeni, kwa Mheshimiwa Marehemu Dr. Ahmed Hassan Diria pamoja na Balozi Paul Bomani ambao wametangulia mbele ya haki. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema, na wote waliokuwa wamepata misiba pamoja na mimi mwenyewe kufiwa na mama yangu tunaomba Mwenyezi Mungu Subhaana Watakhala awajalie maiti hizi Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema pamoja na wafia awape faraja pamoja na subira. Kuhusu Muswada huu kusema kweli umechelewa ilibidi uje mapema kabisa. Kwa sababu masuala ya umeme vijijini ni masuala mazito wakati fulani ilikuwa katika kijiji kimoja huko Kusini nikamwuliza alikuwa jamaa makonde mtani wangu amechonga vinyago, basi katika kuchonga vinyago nikaviona vinyago vizuri sana nikata kununua kupeleka nyumbani, nikamwuliza mbona vinyago vizuri sana, lakini watoto wako hawa unaozaa ni wabaya vipi imekuwaje? Mmakonde yule akajibu njomba hivi vinyagao nachonga *nchana* lakini watoto nachonga *uchiku*. Maana yake ni kwamba usiku kiza, sasa kutokana na hali ile ilinichekesha sana, mimi nilikuwa nimecheka kweli kweli kwamba, kwa sababu vijijini kule kuna kiza basi maana yake watu wakati fulani nilisema watu wanalala mapema sana.

Kwa maana hiyo basi kuna haja ya kuona kwamba kuna uharaka wa kupeleka umeme vijijini. Ili watu wawe na muda mrefu wa kufanya kazi kuliko muda wa kulala. Kwa hiyo, nasema Muswada huu umechelewa kuja hapa Bungeni, ilibidi uje mapema sana. Sasa naingia katika Muswada wenyewe moja kwa moja, Muswada wenyewe katika kipengele cha pili ule ukurasa wa 45, wenzangu wamezungumzia kwamba unahusu Tanzania Bara pekee yake kwenye ile Ibara (2) *This Act shall apply to main land Tanzania only.* Mimi nadhani suala hili lingefikiriwa kwa sababu umeme wa Unguja unategemea Bara na kama tunataka uwe umeme uliokuwa madhubuti, kule Unguja basi maana yake ni kwamba kukiimarika Bara na Unguja kutaimara. Kwa hiyo, mimi sidhani kwamba suala la Unguja liachwe peke yake likitenganishwa na Tanzania Bara. Kwa hiyo, kipengele kile nadhani kingebadilishwa kama Wabunge wenzangu waliotangulia kusema kihusishwe pia na Tanzania Zanzibar yaani kule Visiwani. Kwa sababu nao umeme wao unategemea kutoka Bara zaidi. *(Makofi)*

Baada ya hapo katika Ibara ya (22) ukurasa wa 59 mpaka 60 kwamba vyanzo vya mfuko huu wa nishati Muswada huu unasema kwamba kisheria vyanzo vya mfuko au matumizi ya vyanzo ya mfuko huu wa nishati vitumike kupunguza gharama za uwekezaji wa waendelezaji wa nishati tu, yaani *Qualified Developers,* na sio watumiaji wa nishati yenyewe vijijini. Kusema kweli hili jambo si nzuri wala si jambo ambalo litaleta manufaa makubwa kwa watu wetu vijijini. Kwa sababu hawa *Developers au Qualified Developers* wanaoendeleza miradi ya umeme vijijini ni watu wenye kujiweza ni watu ambao wana uwezo mkubwa wa kipesa, ukilinganisha na watumiaji wenyewe. Ni kweli kwamba wanahitaji msaada ili waweze kuwekeza. Lakini huko vijijini nani tunafahamu atakayeweza kuwekeza umeme kule mwananchi au mwanakijiji, itakuwa ni ndoto kabisa. Maana yake msaada huu, mfuko huu utakuwa unakwenda zaidi kwa wale wenye uwezo wa kipesa, wale wajanja ambao waliokuwa wana mbinu mbalimbali za kuweza kutumia mbinu zao kuweza kupata faida katika hali ya maskini ambao kusema kweli hawana kitu. Kwa hiyo, mimi nadhani msaada mkubwa au matumizi ya mfuko huu yangekwenda kweli kwa wale ambao walikuwa wanawekeza vijijini, lakini sehemu kubwa ingekwenda

kwa watumiaji wenyewe huko vijijini. Kwa sababu wao tunajua kule vijijini ni tabu sana watu kuwa na uwezo wa kipesa kuweza kujimudu kuendesha miradi ambayo inashughulikia nishati vijijini.

Kwa hiyo suala hili mimi ningesema matumizi ya vyanzo vya mfuko huu zingewafikiria pia hawa customers au wale watumiaji umeme weneyewe kule vijijini. Baada ya hapo sehemu ambayo inayohusu masuala ya nishati, kusema kweli Tanzania tumekuwa na nishati ya maji kwa muda mrefu hasa hasa tukisema vyanzo vidogo vidogo vile Mtera, Hale, Nyumba ya Mungu na kadhalika. Kusema kweli ni tatizo ambalo limetupata, ikiwa tulikuwa tunataka matumizi ya maji tupate msaada mkubwa sana. Pale Rufiji sisi tulikuwa na mradi mkubwa *Stiglers Gorge* ambao ungeweza kutoa *Megawatt 2000,* lakini bahati mbaya tukauacha na ahsante Naibu Waziri wa Nishati amenisaidia ni *Megawatt 2000.* Sasa tukaacha mradi ule wa *Stiglers Gorge* tukachukua vijimradi vidogo vidogo hivi ambavyo kusema kweli hata sisi wenyewe umeme wenyewe haututoshi ambapo tungejenga ule mradi mmoja wa *Stiglers Gorge* tungekuwa na umeme wa ziada na tungeweza kuuza nje ya nchi yetu.

Sasa sijui tunasua sua katika mradi huu kwa nini nadhani wakati umefika muafaka kama ni kwamba tunataka kuendeleza matumizi ya nishati ya maji basi ifikirie Serikali, Wizara ya Nishati na Madini ifikirie jinsi gani ya kuushughulikia mradi ule *Stigler au Stiglers Gorge.* Kwamba na ule mradi wa *Stiglers* ulikuwa unahusu si kutoa umeme peke yake bali ulikuwa unahusu hata masuala ya umwagiliaji. Kwa sababu katika bonde la Mto Rufiji lote lilikuwa ni kwamba baada ya kuweka kuzuia maji pale katika *Stiglers* ingelikuwa ni tayari mpango mzuri ungekuwa umefanyika katika bonde lote la mto Rufiji kanzisha kilimo cha umwagiliaji. Maana yake maji yangelikuwa yanadhibitiwa na kwa maana hiyo yanakwenda kwa utaratibu unaotakiwa. Kwa hiyo, tungeweza sisi kwa bonde lote la Mto Rufiji kuanzisha kilimo cha umwagiliaji na umeme uliokuwa unapatikana ungetutosheleza Tanzania na kuuza nje ya nchi na hasa hasa tunataka sisi umeme uliokuwa unapatikana uende zaidi katika uzalishaji kuliko matumizi na tunajua umeme kwenda vijijini ni matumizi zaidi na sio uzalishaji.

Kwa maana hiyo basi kwamba mimi ningesisitiza suala la kuhuisha au kurudisha fikra ya kuendeleza mradi ule *Stiglers* kuna umuhimu mkubwa sasa kuliko hapo nyuma. Kwa hiyo, naiomba Serikali suala hili ilishughulikie mapema iwezekanavyo tuweze kutumia maji yale ya mto Rufiji pale *Stiglers* kwa ajili ya kuzalisha umeme na kwa ajili ya kumwagilia mashamba *Irrigation.* Mimi nilidhani pia kwa kupatikana *gas* ya songosongo na sasa hivi kunafanywa uchunguzi zaidi wa kujua kiasi gani cha *gas* tuliyokuwa nayo kule *Mnazi Bay,* lakini *gas* ya songosongo nilidhani ingekuwa ni ukombozi mkubwa katika upande wa nishati na kwamba kwa sababu tunazo sikumbi tani milioni ngapi pale za *gas* pale songosongo. *Gas* ilikuwa pengine ingekuwa nishati mbadala kwa upande wa maji na zile ambazo wananchi hawawezi kuziweza kwa mfano za mwanga wa jua *Solar* au nyinginezo za *Bio gas* na kadhalika.

*Gas* ingekuwa imetukomboa sana ingelikuwa sisi tungelikuwa tumeitumikia, lakini mimi nilishangaa wakati fulani na nimekuwa naye Naibu Waziri katika Jimbo langu, namshukuru sana kulitembea Jimbo langu na ametupa ahadi pale Kibiti kwamba

kuanzia mwezi wa sita Juni mwaka mambo yatakuwa mazuri na pengine umeme wa *gas* tutaweza kupata pale katika Wilaya ya Rufiji. Lakini akanipa *dose,* akanipa jambo ambalo limenitia wasi wasi kwamba umeme ule wa *gas* hautokuwa chini, bei yake haitakuwa chini na umeme huu unaopatikana sasa hivi wa maji. Sasa nikajiuliza kwamba umeme wa *gas* tuliambiwa kwamba utapatikana kwa bei nafuu, sasa kwanini uwe sawa sawa na umeme huu wa kawaida au gharama zake zisiwe chini ya umeme huu ambao sasa hivi tunautumia. Hilo nafikiri iwe changamoto kwa Wizara ya Nishati na Madini, kuona kwamba *gas* ambayo tunaipata iwe basi ipunguze gharama katika vijiji vyetu na ningependa zaidi umeme huu wa *gas* ungekwenda katika vijijini mbalimbali ili kuweza kuondosha tatizo hili la nishati huko vijijini. *(Makofi)*

Mwisho kwamba nilianza na mmakonde yule anasema njomba nachonga vinyago *nchana* lakini hawa watoto natengeneza *uchiku.* Sasa kutokana na hali hii nasema kuna suala zima la jinsi gani tunavyofikiri suala la umeme, tunadhani kwamba ni umeme maana yake lazima uwe mjini. Lazima umeme sasa uende vijijini ili kuwarudisha watu waliokuwa mijini kwenda vijijini, kwa sababu umeme unavyokuwa vijijini watu waliokuwa mijini ambao wamekwenda kule kwa ajili ya kutafuta na kwa ajili ya kuwa na maisha mazuri wataona kwamba kule vijijini hali sasa itakuwa nzuri ya maisha. Kwa hiyo, inamaana tutapunguza influx ile ya watu kutoka vijijini kwenda mijini watarudi kwenda kule vijijini na kwa maana hiyo vijiji vyetu vitakuwa vya uzalishaji, vijiji vitakuwa vya kufanya kazi na vijiji vitakuwa katika hali nzuri zaidi vya maendeleo kuliko hivi sasa hivi. Kwa hiyo, mimi naomba Wizara sasa hivi Muswada huu upite ili kazi iende vizuri zaidi na Serikali isiiachie masharika tu ya binafsi kuendesha mambo haya isipokuwa yenyewe ijiusishe katika masuala ya kusambaza umeme vijijini.

Mwenyekiti, nashukuru, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Sheria ya kuanzisha wakala wa mfuko wa Nishati Vijijini ya mwaka 2005. Napenda kwanza kutoa salam za rambi rambi za wenzetu wote ambao wamepoteza jamaa zao ikiwemo familia ya Mheshimiwa Balozi Diria, Mheshimiwa Balozi Bomani pamoja na jamii yote ya Wakristo na hasa wakotoliki na watanzania wote na dunia zima kwa kumpoteza Papa Yohana Paul wa II katika kipindi hiki kabla hatujakutana hapa Bungeni. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Naomba kwanza mimi niseme naunga mkono sana madhumuni yaliyomo katika Muswada huu ambao lengo kuu na madhumuni makubwa ni kuweka utaratibu wa kisheria ambao ni kuanzisha wakala wa mfuko wa nishati vijijini. Kwa lengo hasa la kuweza kuratibu juhudi za kuendeleza nishati ya kisasa Tanzania Bara, kuchochea uendelezaji wa nishati bora na vilevile kuhakikisha ukuaji wa huduma za nishati zinaenea kote vijijini.

Ukitazama madhumuni haya kwa kweli ni mazuri mno, kwa sababu yanalenga kusaidia juhudi za kujenga uchumi mpaka maeneo ya vijijini ambako wananchi watashirikishwa katika maeneo mbalimbali na wataweza kupata huduma mbalimbali hasa katika maeneo ya afya, elimu, maji safi, usalama wa raia na mengine yanayohusu hayo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unalenga pia kuona kwamba hali ya maisha ya wananchi waishio vijijini pia inakuwa bora. Wanaokusudiwa kwamba watasaidia katika kuboresha jambo hili ama kulifanikisha, ni kwamba sekta binafsi zitashirikishwa, sekta ya umma na wananchi wenyewe. Kwa kipindi kirefu tumekuwa tukisubiri namna ya kusaidia kuboresha ama kufikisha umeme vijijini na tulikuwa tumeahidiwa kwamba Serikali iko katika harakati za kuunda mfuko utakaoweza kupeleka ama kusaidiana nayo kuweza kufikisha umeme vijijini. Kwa sababu gharama za umeme ni kubwa mno kwa hiyo wananchi wenyewe peke yao hawawezi kumudu na Serikali iliona haiwezi kumudu. Kwa hiyo, ikawa imetuahidi kwamba ingeweza ikaanzisha mfuko wa kusaidia kufikisha umeme vijijini. Pengine Muswada huu umekuja kwa lengo la kutaka kukamilisha jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa mimi hapo nakuwa na hofu ambayo napenda niieleze kwamba Serikali itabakia na kazi yake ya kuratibu na kuhamasisha maendeleo endelevu ya mradi huu na hiyo itakuwa tu ikishirikiana na sekta binafsi pamoja na sekta ya umma. Sasa wasi wasi wangu ni kwamba kama wenzangu waliotangulia walivyosema, gharama za umeme huu kwa mwananchi wa kawaida zitakuwa ni kubwa mno kiasi ambacho hofu yetu inabaki kwamba mwananchi hatoweza kumudu kuutumia umeme huu.

Lakini tunapozungumza umeme, jambo la kwanza linalokimbilia katika akili ya m wananchi wa kawaida ni kuona kwamba tunahitaji umeme kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Pengine hamasa kubwa ingeweza pia ikafanyika kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo vinavyotumia nishati ya umeme wa gharama nafuu ambao hasa ni ya maji ili kuweza kuwashirikisha wananchi katika uchumi huu.

Lakini vile vile sijui ni kwa kiwango gani ambacho Serikali imeliangalia suala zima la zahanati zetu, vituo vya afya na hata baadhi ya hospitali ambazo zimejengwa nje na mbali kabisa ya mfumo wa umeme wa Serikali, *Grade* ya Taifa. Ambazo zitahitaji kupata umeme na ambazo gharama yake kutoa pale ambapo njia kuu ipo kufikisha huko ni mbali, kwa hiyo gharama ni kubwa sana, sijaelewa hawa wawekezaji binafsi, sekta binafsi inaweza ikatusaidia vipi. Tulipokuwa katika zoezi hili lilipoanza la ubinafsishaji wa mashirika ya umma tulipata wawekezaji binafsi wengi, lakini walikimbilia kwanza kubinafsisha ama waligombania sana kiwanda cha Bia pamoja na Sigara kwa sababu waliona kwamba viwanda hivi vilikuwa vinaendelea kufanya kazi na vilikuwa vinazalisha. Sababu iliyotolewa ni kwamba mwekezaji binafsi anakimbilia kwenda kupata faida. Kwa hiyo, wanakwenda kuwekeza pale ambapo wana uhakika kwamba wataweza kupata faida. Kwa hiyo, wakakimbilia katika maeneo ya Bia na maeneo ya Sigara. Sasa mimi hofu yangu itakuja kwamba ile tabia ya sekta binafsi kupenda kupata faida, itaendelea kuwa pale pale. Kwa hiyo, tunapofika katika ile imani ya kwamba tunakwenda kupeleka umeme katika vijiji na sasa tunaipa sekta binafsi nafasi kubwa, mimi naendelea kuwa na hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka karibu mitatu niliomba katika Bunge hili hili Wizara ya Nishati na Madini kwamba waweze kutusaidia kufunga umeme mathalan katika Kata ya Kagoma makao makuu ya Kata ya Kagoma katika Jimbo la Muleba

Kaskazini ambapo ni kilomita tisa kutoka pale nguzo ya mwisho ilipo katika jimbo langu. Waliniambia kwamba ni wastani wa milioni 92. Serikali tangu wakati huo imekuwa ikinipa majibu ambayo siridhiki nayo kwamba haiwezi kufunga huo umeme kwa sababu haina uwezo wa kutoa milioni 92 na sababu ni kwamba umeme huo haulipi japo kuwa kulikuwa na wananchi wengi ambao walikuwa tayari wapatao kama 60 au zaidi kufunga umeme na hata wengine tunaamini wangejitokeza. Lakini Serikali iliendelea kunipa jibu ya kwamba umeme huo haulipi. Sasa kama leo Serikali inakwenda kubaki kama mratibu na mhamasishaji, sekta binafsi ndio inayokwenda kupewa nafasi kubwa, na hapo hapo unakwenda kukuta kwamba pia sekta ya umma ndio inayotegemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapo naona kama inaweza ikatuchukua muda mrefu zaidi na inawezekana pengine isifanikiwe. Nami naamini kabisa kwamba Serikali kwa kweli katika hili basi ingeuchukua ule umeme wa vijijini ukawa ni sehemu ya kutoa huduma badala ya kufanya kwamba ni umeme wa biashara.

Kwa hiyo, kuna maeneo mengi tu kwa mfano ninayo maeneo ambayo umeme unapita tuseme nguzo za umeme zinapita katika vijiji hivyo lakini unakuta vijiji hivyo haviwezi kupata umeme. Sababu ambazo inayotoa Serikali ni kwamba kushusha umeme katika kile kijiji ni gharama kubwa, na mimi nikiamaini pale ambapo tayari nguzo zimeshakuwa karibu na umeme unapita karibu vijiji hivyo pengine utaalam unaotakiwa kutumika pengine si mkubwa mno kama wakwenda kukatisha umeme pale ambapo haupo kabisa.

Kwa mfano kupeleka kilomita tisa, kilomita 100, kilomita 200 kama vile ambavyo Tanzania tulivyo tunafahamu maeneo jinsi yalivyo. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali kwamba iliangalie upya suala la umeme vijijini, badala ya umeme kuwa ni wa faida basi uwe ni umeme wa huduma na wananchi waelimishwe kwamba si umeme wa kutumia majumbani tu bali pia wa kuzalisha kiuchumi. Kusudi uweze kutumika katika kuwaongezea hali ya kipato cha maisha, kubadilisha maisha yao na sasa hivi ukizingatia kwamba Tanzania tumeingia katika ushirikiano wa Afrika Mashariki ni wakati ambapo tuna ushindani mkubwa sana. Kila mwananchi mwenye uwezo angetakiwa kuzalisha pale mahali alipo, badala ya kutumia gharama yake kubwa kusafiri kwenda makao makuu ya miji. Sehemu ambayo ajira ni za matatizo na kuacha maeneo ya vijiji ambapo tungeliweza wananchi wakakaa kule na wakaweza kujitegemea.

Lakini ni kwa kiwango gani ambapo wananchi wameelimishwa kuweza sasa kuutumia umeme huo, kama sekta binafsi lengo lake ni kufanya biashara. Inawezekanaje sasa hii biashara tunayokusudia kwamba umeme wote tunaotegemea sasa usimamiwe na sekta binafsi kwamba utaweza kufikia vijiji vile vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu inakuwa ni hapo na mimi ningeliomba sana suala hili wakati Waziri ana-*wind up* basi anitoe haya mashaka yangu ili niweze kuona kwamba kweli wananchi wetu ambao wanauwezo mdogo wataweza kufikiriwa na sekta binafsi kuwafungia umeme huo na wenzangu waliochangia wiki iliyopita walizungumza kwamba kufunga umeme katika nyumba ya kawaida ni takribani 700,000.

Mwananchi huyu anasaidiwa vipi kuweza kufunga katika nyumba yake umeme huo upatao 700,000, wakati ambapo tunafahamu kwamba uwezo wake wa maisha ni mgumu na kujipatia huduma zingine ambazo zinazomuhusu vile vile ni vigumu. Je, umeme huu utapelekwa vijijini kuwahudumia, ama utapelekwa vijijini ili kuweza kuzalishwa kwa faida.

Kwa hiyo, nina rudia kwamba Serikali iangalie umeme wa vijijini usiingizwe katika faida, bali uwe ni huduma inayolenga kusaidia huduma za vijijini. Ili maendeleo katika nchi yetu yaweze kwenda sawa sawa katika Tanzania nzima, kama vile walivyo mijini. Basi iwe hivyo hivyo pia katika vijiji uwe mradi maalum unaolenga kuweka maendeleo sawa ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliposikia *Net Group Solution* imeanza, tulifurahi sana. Lakini baada ya muda mchache tu tuligundua kwamba umeme ulikuwa haubebeki hata kwa wale wanaoishi mijini umeme haubebeki. Umekuwa ni gharama kubwa sana kiasi ambacho kwa kweli watumiaji wengi wa umeme wa mijini wamebaki, sasa ni kuutumia kwa ajili ya majumbani na wale wa viwandani sasa wamebakia na wenyewe wengi wakijaribu kutumia njia nyingine ambazo wanadhani zinaweza zikawasaidia kwa sababu ya gharama kubwa ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa umeme usiendelee kuwa mzigo wa Mtanzania, ila uwe ni nyenzo ya kumsaidia kumuinua katika hali ya uchumi, kumwimarisha kiafya, kumsaidia katika elimu na kumsaidia katika maendeleo yake ya jumla na kuweka mazingira haya ambayo mwenzangu aliyetangulia alitoa mfano wa Mmakonde. Lakini mimi nasema Tanzania inapokuwa giza wakati wa usiku Watanzania wanatumia muda mwingi sana kulala badala ya kutumia muda mwingi sana kufanya kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mataifa yote ambayo tunaiga kuendelea na ambayo tunawaomba watusaidie, wamejitahidi sana katika suala zima la umeme. Kwa hili Serikali isikwepe, ikubali kubeba mzigo wa huduma ya umeme vijijini ili wananchi wote waweze kupata umeme na kushirikishwa katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na vile vile niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naona fahari kubwa kusimama mbele yako wakati ukisimamia shughuli hizi na kwa *agenda* hii.

Pili ningependa kabla ya kutoa mchango wangu niungane na Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa familia za ndugu zetu waliotutoka au waliotutangulia mbele ya haki hayati Balozi Ahmed Hassan Diria na Balozi Paul Bomani, Mungu aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata taabu kidogo kuunga mkono Muswada huu kwa sababu dhana ya *rural* kwa hapa haiko wazi, ni nje ya Wilaya. Ni kijijini kabisa. Pili, je, kama pale Njombe pana Mto Ruhuji au Hagafiro na kuna maporomoko na pale ni mjini pale huu Muswada hauhusiki? Au lazima watoe umeme wa pale mjini kupeleka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo ukiangalia ramani au picha ya Bara la Afrika wakati wa usiku. Bara la Afrika likpigwa picha wakati wa usiku utakuta kwamba Bara la Afrika ndio Bara jeusi kupita mabara yote katika Dunia. Ina maana kwamba hakuna mwanga isipokuwa labda upande wa *South Africa* na *North Africa* ni giza tupu wakati wa usiku kama unapita kwa ndege, Mabara mengine unaona kuna mwanga.

Kwa hiyo, Bara la Afrika ni Bara lililo katika hali ya giza, *it is the darkest continent in the world.* Miaka mingi kabla na baada ya ukoloni vile vile Bara la Afrika liliwahi kupewa jina la kuwa *dark continent,* Bara la giza. Kwa wakati ule walimaanisha Bara lisiloendelea, lisilojulikana ambalo liko kwenye vita wakati wote au lisilomjua Mungu kwa maana ya Mungu huyu wa Kikristo. Lakini leo bado hata baada ya vigezo vyote hivi hili Bara limekuwa jeusi zaidi, giza zaidi, vita, umaskini lakini inapokuja kwenye Bara kama hili kwamba watu robo tatu ya wakati wa usiku hawafanyi kazi, ni kigezo cha kutokuendelea kabisa.

Kwa hiyo, Muswada huu umekuja wakati mzuri, lakini nadhani nia ni nzuri isipokuwa haiambatani na mikakati iliyosahihi, nitafafanua hilo. Kwa nini ni mifuko? Tuna mfuko wa mbolea, elimu, tuna mifuko mingi tu. Tumejifunza nini kutoka mifuko hiyo? Je mfuko huo ndio muarobaini wa matatizo ya umeme kupelekwa vijijini sidhani. Uzoefu katika Shirika la *TANESCO* unaonyesha kwamba kuna mabingwa na vijana wengi wa Tanzania waliobobea katika suala la umeme vijijini, wakina Kingu, Massawe, Msofe na wengine wengi tu.

Kwa miaka yote wamekuwa wakifanya kazi hii na hivi sasa wanakaribia kumaliza Wilaya. Lakini walikuwa *occupied* na kazi ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Mikoa kwa muda wote huu. Pamoja na matatizo ya Shirika la *TANESCO* hakuna Shirika lililofanya kazi kubwa katika Bara la Afrika upande wa umeme kama *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo Serikali inatakiwa ijue ni kwamba madeni haya yaliyolimbikizwa kwa miaka mingi kutokana na mikopo kama Serikali yenyewe ilivyokuwa inakopa ndio yanayozorotesha Shirika la *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayotakiwa hapa ni kuondoa madeni haya kwanza na kuanza ukurasa mpya, vinginevyo tunaendelea kupiga kelele hapa. Haiwezekani. Tunanyofoa chombo hiki cha kupeleka umeme vijijini kwa sababu ya matatizo ya *TANESCO* eti kwa sababu lina madeni mengi. Kwa hiyo, tukibakiza hapa haitawezekana, ni kama tulivyoondoa *NBC* tuliponyofoa matawi mazuri ya *NBC* ya mijini kutenganisha na yale ya vijijini. Kumbe yale ya mijini yalikuwa ndio yanasadia ku-*support* matawi ya *NBC* ya vijijini ambayo yalikuwa hayawezi kuleta faida. Kwa hapa umeme mijini ndio utakaosaida ku-*support* umeme vijijini. Lakini hapa tumetenganisha

bila ya *force* kutoka kwa wahisani, kwamba nyofoa hapa utengeneze hapa? Chombo hiki cha *TANESCO* kingeweza kabisa kufanya kazi hii kwa sababu kuna idara ya umeme vijijini na inafanya kazi vizuri tu, ina utaalamu wenye uzoefu wa kutosha. Kinachokosekana hapa ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kuunda tena chombo kama hiki ambacho kitakuwa na menejimenti na bodi na urasimu na wataalamu wengi tena hela zitaishia kuliwa na watu hawa kwa sababu ya mishahara. Tunajenga matende ya urasimu ambayo yatakuwa yanakula hela na maendeleo yatabaki pale pale. Nadhani njia hii siyo sahihi, nia ni nzuri. Kama tunashindwa kupata hela za kuendesha umeme kufikisha kila Wilaya hivi sasa tunapata, huku tutapata vipi? Au kwa sababu ya wahisani tukubali kwa sababu tusipowakubalia hawatatuletea fedha labda tuseme hili, lakini mkakati hapa utokane na Bajeti ya Serikali kama tunavyohangaikia katika barabara, vinginevyo haitawezekana kabisa.

La pili kudhani kwamba Serikali itakuwa *facilitator* nadhani tunajidanganya, lazima Serikali iwe *provider*. Hawa maskini ukipeleka umeme vijijini bila *support* ya Serikali haiwezekani. Uzoefu unaonyesha kwamba wanaotaka kutoa umeme huu wanataka wa huku kwenye gridi halafu wapate hela kiurahisi tu, lakini sio waende kufuatilia kwa mkulima wa kawaida vijijini. Hii ni kazi ngumu. Lakini watatoka wapi, hawa unaodhani watakwenda vijijini kutengeneza umeme labda hawa wanao-*retire* kutoka *TANESCO.* Lakini wana uwezo gani. *This may be a leap in the dark, a non starter.* Tunabaki tu na malengo mazuri. Tuwasaide wananchi vijijini, tusiwakimbie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini njia zipi zitasaidia. Mimi nina mashaka makubwa sana. Nia ni nzuri lakini tungesadia idara hii ya *TANESCO* tuliyonayo sasa hivi na chini ya *support* ya Serikali tukimaliza Wilaya twende kwenye vijiji kwa kutumia shirika hili na watu hawa, *after all* Wilaya nyingi ni vijijini tu. Kwa hiyo, *concept* ya ku-*define* wapi ni *rural,* wapi ni mjini nayo inatakiwa ifunuliwe vizuri kusudi tusije tukakwepa *we can hide but we can't escape.* Wajibu wa kupeleka umeme vijijini ni kama kupeleka elimu vijijini ni kazi ya Serikali. Kudhani kwamba kutakuja mtu mwekezaji awekeze katika umeme, katika mazingira haya kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia ni kazi ngumu sana. Mtu binafsi anataka faida hawezi kujenga bwawa la maji. Mtu binafsi anataka faida.

Kwa hiyo, hili ni wazo zuri lakini labda tulifanyie majaribio kwanza. Kwa mwanzoni tufanye kama mchezo wa *relay,* Serikali iendelee kufanya kazi ya ku-*provide* sio ku-*facilitate* mpaka tutakapofanikiwa ndio baadaye iweze iachie huyo itakayemwona anafaa, vinginevyo tunaweza kuwa hapa ni njia tu ya ku-*escape* kazi hii iliyo ngumu inakwenda mahali pengine, gharama za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za umeme zinatokana na madeni na hakuna njia ya mkato, njia ni kufuta madeni ya *TANESCO* tuanze ukurasa mpya, vinginevyo haitawezekana. Kusema hawa waende pembeni kusudi hawa waendelee na mtindo huu haiwezekani. Nchi inazidi kuhangamia wawekezaji wanazidi kukimbia na watu wanazidi kukwepa umeme hata ungetenezwa, wanakwepa kwa sababu ya gharama. Sasa tunatafuta

njia za mkato hapa, hapana tufute madeni yale ambayo yamekaa miaka mingi kutokana na Serikali yetu kukopa. Sawa sawa inawezekana wazo hili ni zuri *it is a desirable idea* lakini *not necessary* kwa wakati huu. Lakini kama ni kwa sababu ya pesa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya nne ningependa utupe nafasi kushukuru Shirika la *TANESCO* na Serikali kwa ujumla kwa kushusha umeme Makambako ili kueneza katika vijiji vya Wilaya ya Njombe vya wakulima wa chai na hii itatupa nguzo nzuri ya kupeleka umeme kwenye shule zetu pamoja shule yako ndugu Mwenyekiti ya Yakobi kwa makusudi wafanye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili wazo la kupeleka umeme vijijini liambatane na hii *concept* ya kupeleka elimu vijijini. Bila kupeleka umeme kuambatisha na shule vijijini maana yake ni kwamba hizi shule tutakuwa na watu wanatoka *semi-illiterate* kwa sababu dunia ya sasa *illiteracy* ni pamoja na kujua *computer* bila kuwa na umeme kwenye shule yako ya Yakobi pale wale watoto watatoka bila kujua *computer*. Kwa hiyo, elimu ya *computer* itashikwa na watu mijini nao wa mijini ambao ni asilimia 20 ya Watanzania wote wanakaa mijini ndio wanaofaidi asilimia 80 ya huduma za *computer* na umeme katika nchi hii. Kwa hiyo, ndio watakaokuja kututawala sisi tulio asilimia 80, asilimia 20 inatawala asilimia 80. Kwa hiyo, kuwe na maamuzi ya makusudi ya ku-*develop the rural area.* Vinginevyo kwa nini mimi nikae kijijini na ku-*condemn* watoto wangu wasipate elimu kabisa kwa sababu ya kukaa kijijini hakuna umeme, huduma, hakuna kila kitu.

Hivi sasa watu wote wanakimbilia mijini ili hawa watoto wasije kuwa *condemned* na kubaki watawala, hatuwezi tukaishi na Taifa la watu nusu watumwa na nusu huru. Kukaa kwenye giza katika dunia ya sasa ni kigezo cha utumwa kabisa. Ni kweli ni maskini lakini unafanyaje kama tulivyoamua elimu basi na umeme tuamue hivyo hivyo. Vinginevyo tutaua nchi hii watu watazidi kuuwa miti, kukata miti majangwa yataongezeka na watu watakuwa *condemned to death.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo mimi ningependa nimalizie kusema kwamba atajitokeza *developer,* haiwezekani ila napendekeza kwamba ngazi ya Wilaya pamoja na hili wazo wawe na mfuko vile vile wa *energy* kusudi kueneza umeme kwenye maeneo *strategic* katika Wilaya kusudi waweze kuendeleza Wilaya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mada iliyopo mbele yetu. Lakini awali ya yote nitoe salaam za rambirambi kwa familia na wananchi wa Jimbo la Rahaleo kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria. Pia nitoe salaam za rambirambi kwa uongozi wa Chuo Kikuu na *Tanzania Breweries Limited (TBL)* kwa kumpoteza kiongozi wao shupavu Mheshimiwa Balozi Paul Bomani. Nimalizie salaam zangu za rambirambi kwa kutoa salaam hizi kwa waumini wote wa Katoliki kwa kufiwa na kiongozi wao Duniani Papa Yohana Paul wa Pili.

Baada ya hapo nianze kuchangia Muswada huu kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Daniel Yona, kaka yangu, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kazi nzuri na ambayo ni changamoto kubwa kwao kwa maendeleo ya umeme katika nchi yetu. Nichukue nafasi ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa ziara aliyofanya Jimboni kwangu hivi karibuni ambapo amekuja na kutoa hamasa na changamoto kwa Shirika la *TANESCO* kwa wananchi wa vijiji vyetu vya Same vilivyoko barabarani ambako umeme unapita na wao walikuwa hawaufaidi, napenda nimshukuru sana.

Sisi kule Same inasikitisha kwamba umeme unapita pale lakini wananchi walikuwa hawaufaidi. Kwa hiyo, napenda nitoe shukrani za pekee kwa sababu hiyo, nilikuwa namwambia kwamba mdomo ukila, pua inasikia, sasa sisi kule tulikuwa tunasikia mdomo unakula tu, lakini pua haipati chochote. Kwa hiyo, namshukuru angalau wananchi wameweza kupata jibu hilo.

Baada ya kutoa shukrani hizo na pongezi, nipende kusema kidogo kuhusu Muswada huo ambao uko mbele yetu. Muswada huu umeletwa kwa wakati na nafikiri kwamba iwapo sisi Wabunge tutaupitisha nina imani kabisa tutaleta sura mpya ya maendeleo ya wananchi wetu huko vijijini. Kwa sababu umeme ni nishati muhimu sana katika maendeleo ya watu wetu kila mahali bila kujali wa kijiji wala mjini. Lakini sasa Muswada huu jinsi ulivyoletwa na mfumo wake na mpangilio wake mimi ningependa kutoa mambo matatu, manne ya tahadhari ili Wizara iweze kuyaangalia wakati wanahitimisha hoja ya Muswada huu.

La kwanza ni kuhusu bei ya umeme kuwa kubwa. Tunaweza tukawa na juhudi za makusudi za kupeleka umeme vijijini kweli kufuatana na malengo ya mradi huu. Lakini bei ya umeme ya sasa hivi iko kubwa mno na wakati mwingine umeme wa sasa hivi wana-*charge* mpaka *interest.* Sasa watu wetu kule wakisikia kwamba waliambiwa wanadaiwa shilingi 6,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shilingi 6,000/= zimeongezeka zimekuwa shilingi 10,000/= wanaona kabisa ni kitu cha ajabu kwa sababu wananchi wetu vijijini hawajui maana ya *interest* ni nini. Kwa sababu kwanza wenyewe hawaishi kwa *interest.* Duniani kuna watu wanaishi kwa *interest* lakini sio watu wa vijijini. Kwa hiyo, ningeomba hili suala liangaliwe, tusije tukapeleka huduma hii halafu ikakosa wateja.

Lingine ni kuiomba Wizara, bei ya umeme imekuwa kubwa sana *unbearable,* labda kwa sababu ya *operation cost* zimekuwa kubwa kwa sababu gani labda mishahara ya watumishi ni mikubwa mno. Inasemekana kwamba mishahara ya watumishi wa *TANESCO* imekuwa mikubwa mno. Kuna maneno kwamba mishahara inakwenda mpaka kuwa shilingi milioni 26 kwa mwezi kwa wageni, sasa hili nalo lingefikiriwa na kuangaliwa.

Lingine ni kuhusu umeme ambao tunapata wa gesi ambao tunaambiwa ni umeme rahisi. Sasa kama tumeanza kuutumia kwa nini unafuu hauonekani. La tatu umeme wa sasa tunaoutumia ni *hydropower,* unatumia maji, maji ambayo wananchi wetu walikuwa wanatumia katika kilimo kwa maana nyingine tumewanyima wananchi maji waliyokuwa

wanatumia katika kilimo ili tuyatumie kwa umeme. Na umeme tunaowapelekea bei yake ni ghali. Wakati huo tumewafanya maskini kwa kushindwa kulima kwa sababu ya kukosa maji. Kule kwetu Mto Pangani unavunwa maji mara mbili. Unavunwa maji pale Nyumba ya Mungu na kule Hale. Maana yake wananchi wote walioko pale walikuwa wanategemea ule Mto kwa ajili ya kilimo sasa juhudi zao za kilimo zimepiga ukuta. Wakati mwingine maji hayo hayo bado wanawa-*charge* ili *TANESCO* waweze kupata maji ya kutosha kwa ajili ya umeme.

Sasa lazima tu-*strike a balance* tunawapelekea wananchi umeme kweli wa maji. Lakini hapo hapo maji hayo tunatumia yangetumika kwa kilimo. Tumewanyima uchumi wao wa kilimo, je, watakuwa na uwezo upi wa kulipia umeme? Ningeishauri Wizara kwa mpango wake wa baadaye ifikirie kutumia *alternative source of power.* Kama wangeweza kutumia umeme wa maji, gesi, makaa ya mawe, badala ya kutumia umeme wa maji ili maji yatumike kwa kilimo kama tunataka kuwajenga watu wetu ambao *80 percent* ya Watanzania wanategemea kilimo. Sasa kama maji yote tutakuwa tunayatumia kwa ajili ya umeme hawa wananchi wataishije? Kwa hiyo, ili tuweze ku-*strike a balance* Wizara iweze kuliangalia hilo kwa siku zijazo.

Vile vile kwa siku zijazo Wizara iangalie *Stiglers Gorge* ambayo iko karibu na Bahari nje ya tegemeo la wakulima waweze kuvuna yale maji wakiyatumia kwa ajili ya kuweza kufulia umeme. La tatu, Muswada lengo lake ni kuwapendelea wananchi wa vijijini, lakini isije ikatokea hatari ya kuwabagua wananchi wa vijijini. Tulipobinafsisha Benki ya Biashara ya Taifa tulisema Benki ya *National Microfinance* ile ya makabwela ya watu wa vijijini sasa tena tumeinyemelea sasa tunakuja kwenye *power.* Tunakuja kwenye *power* sasa kwenye umeme tunasema sisi tunaanzisha hii Sheria ya umeme vijijini kwa sababu ya kuwapatia wananchi wa vijijini upendeleo. Lakini isije tukawageuzia kibao baadaye badala ya Serikali kuwajibika na kuwapelekea wananchi umeme wananchi wakawa wamekosa huo umeme. *(Makofi)*

Mimi ningeomba kwa hili Wizara iliangalie sana. Tumesema kwamba tunaipitisha hii sheria kwa ajili ya umeme vijijini. Lakini tuna miji ambayo haina umeme, Miji kama Kigoma, Lindi, Mtwara. Sasa hawa watakuwa wapi, je, tutakuwa tena na sheria itakayoletwa ya umeme mijini? Maana wao hawana umeme utaratibu wao utakuwa wapi? Ningependa kupata jibu lake. Sisi kule Same tunashukuru sheria hii ikija kwa sababu wananchi wetu wengi wanaishi milimani. Kule milimani hakuna umeme kabisa pamoja na kwamba Waziri anatoka kule, lakini tarafa tatu hazina umeme. Tarafa ya Mwembe, Mbaga, Gonja, Mamba -Vunta, zote hizo hazina umeme kabisa ni giza.

Tuna imani hii sheria itakapopitishwa angalau itatutoa katika hilo giza alilokuwa analisema Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwamba kule sisi milimani tumakuwa ni *dark district* yeye amesema *dark Continent.* Lakini mimi nasema ile ni *dark district* na umeme unapita pale lakini hatupati huduma yake.

La tatu ni urasimu wa bodi na wakala wa sheria hii. Mimi nikiangalia urasimu wake utakuwa mgumu kwa sababu kuna bodi, wakala halafu kuna sijui *supervisor,* sijui ni kwa nini watu gani Serikali yenyewe inajiita ni *facilitator.* Sasa mimi nashindwa na

ukija kwa wakala unakuta wakala hawa Ofisi yao iko huko katika Taifa. Huko ambako wanapeleka huduma yao hawana *structure,* wala hawana ushirikishi. Wananchi vijijini hawajashirikishwa. *TANROAD* wamefanikiwa kwa sababu wameshirikisha viongozi na wananchi wa vijijini.

Tungeomba hawa Wakala wawe na *structure* kule katika Mkoa, Wilaya wasiishie katika Taifa watawafikia wananchi wa vijijini vipi? Wafanye kama vile ambavyo *TANROAD* imefanya. Tuna bodi ya Mkoa ya *TANROAD* japo hatuna katika Wilaya, lakini viongozi katika Wilaya wanashirikishwa katika bodi ile. Je, hawa wakala wa umeme watawashirikishaje wananchi wa vijijini ili waweze kueleza shida zao zinazowasibu kule kwa kukosa umeme.

La mwisho ni kuhusu wajibu wa kupeleka umeme vijijini, mimi ningeomba Serikali isijindoe ikasema ni *facilitator.* Maana *facilitator* ni mwezeshaji, maana yake wakala akishindwa anaeleza kwamba wakala ameshindwa, wananchi wakikosa umeme anakwenda anaeleza mmekosa kwa sababu hii. Mimi naona Serikali bado ichukue jukumu lake la kuwa *developer,* yeye ndio *investor* wa kuwapelekea wananchi umeme vijijini. Serikali ndio yenye uwezo na sheria. Sasa wakala huyu tukimwachia ni kama tunawatelekeza wananchi wa vijijini. Ninataka nitoe mfano ambao unafanana wa namna hii wa Serikali kujiweka pembeni.

Mama mmoja alikuwa anakwenda kuteka maji mtoni akiwa ameweka mtoto katika mgongo amefunga na mbeleko. Alipofika bahati mbaya mtoto akaanguka mtoni. Akafikiria mtoto wake atauwawa na maji. Lakini yule mama alikuwa ana busara sana akapiga yowe wananchi wakaja walipokuja kufuata yowe ile akasema jamani kwa nini mtoto wangu auwawe na maji? Baba mmoja alikuwa na upinde na mshale akamuuliza kwani unataka auwawe na nini akasema kheri auwawe na kingine lakini isiwe maji. Kama nini, mshale? Yule baba akamtia yule mtoto mshale akamwambia mama nimekufanyia kazi uliyoomba. Mama akapiga yowe ya pili akasema sasa mtoto wangu hakuuwawa na maji ameuwawa na mshale, akadai fidia.

Sasa tunaiomba Serikali ichukue mfano wa huyo mama ambaye mtoto wake ameanguka mtoni! Isijiweke pembeni wananchi wakidai hawana umeme vijijini wanasema ni tatizo la wakala inajiweka pembeni tunaomba Serikali bado ichukue wajibu wake wa kupeleka umeme vijijini. Kwa sababu umeme ni muhimu sana vijijini, hata huduma ya simu haiwezi kupatikana vijijini kama hakuna umeme hao ndugu zetu wanajenga minara, minara hii ya simu za mkononi, wanasema wanahitaji umeme kama hakuna umeme hawawezi kujenga minara ile. Simu za sasa hivi ukitaka zipate *charge* ni umeme, sasa hata tukiwapelekea wananchi wetu huduma za simu watapataje umeme? Halafu utandawazi *(computers)* unataka kujua biashara ya Kimataifa lazima upitie katika *computer* kule vijijini wanahitaji huduma hizi hasa katika karne hii ya utandawazi.

Kwa hiyo, mimi nafikiri Serikali isijiondoe. Shule zetu zinahitaji umeme, sio mtoto amalize sekondari anakuja kuona umeme Dar es Salaam. Sio elimu kwake, tunaiomba Serikali iwe *investor* au *developer* kwenye upande wa kupeleka umeme vijijini isijiweke pembeni. Hilo likasahihishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niipongeze Wizara kwa kuleta Muswada wake huu na naunga mkono asilimia mia moja na *Inshallah* umeme ufike kwa wananchi vijijini. Ahsante.

**MHE. DR JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii, kwa kuwa ni mara yangu ya pili kuongea basi nitakwenda moja kwa moja kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwapongeze Wizara kwa hatimaye kuleta Muswada ambao niseme ulikuwa unasubiriwa kwa siku nyingi kidogo. Kwa sababu ya taratibu ambayo Serikali ilijiwekea kwamba taratibu inaendelea kujitoa katika kufanya biashara moja kwa moja. Kwa hiyo, ni mantiki kwamba lazima kwa kuelewa kwamba kimsingi jukumu la kusambaza na kufanya matumizi ya nishati yaongezeke sio katika maeneo ya mijini tu na maeneo ya mbali vijijini, ni jukumu lao basi wameona ni bora wakalifanya kupitia walau kwenye wakala kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kama nilivyoanza ni kwamba Muswada ni mzuri kwa hiyo, unastahili kuungwa mkono lakini una maeneo ya kuboresha na kwa kweli nitaomba kwa dhati kabisa wanivumilie na kama nitashindwa kupata muda wa kumaliza katika mchango wangu wa hapa basi wakati wa Kamati ya Bunge Zima nafikiri nitajitahidi sana kuongezea yale ambayo nitakuwa nimeyaacha. Nataka nianze kwa kutamka kwamba jina lenyewe kwa kweli ni kubwa kuliko dhamira ya Muswada wenyewe. Kwa sababu ukisoma Muswada wenyewe unakuonyesha wazi kabisa kinachozungumziwa hapa ni umeme.

Sasa umeme ni sehemu ndogo sana ya nishati, unapokuwa na jina kubwa hili ambalo limetolewa hapa wao wanasema kwenye jina lenyewe *an Act to establish the Rural Energy Board, Fund na Agency* halafu na *responsibilities* wamezitamka hapo kidogo. Wanatumia neno *energy* halafu ukienda ndani wanaanza kwenye *clause four* kwa mfano, wanatumia neno *modern energy.* Sasa hapo tayari waanza ku-*narrow* tena kwa sababu unaposema *energy, energy it much wider than modern energy. Modern energy* ni *narrow* inakwenda kwenye zile *energies* ambazo kidogo wamezipatia *definition* kwenye upande wa *definition* hapa ambazo hata hivyo hiyo *definition* siyo *exhaustive.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema ni kwamba hili jina siyo sahihi kwa huu Muswada. Hili nataka niseme kabisa ni kwa msingi kabisa na ninapenda wanisikilize. Hili jina siyo sahihi kwa sababu kinachozungumziwa hapa ni umeme. Kinachodhamiriwa huku ndani au Muswada ni umeme peke yake na hii inaonekana hata kama hamjatamka hivyo kuna mahali mmefanya masahisho kwenye *clause 4(a)* kwenye *amendment* zenu mmependekeza *modern energy electricity* kuna neno lilikuwepo pale mmesema lifutwe. Lakini *still what is implied by this act* ni umeme kwa hiyo, nataka niseme *this is narrow* kama tulitaka ku-*cover energy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuonyeshe *how wide is energy? Energy* kwa Tanzania tu ni kuonyesha kwamba kwa mahitaji ya *energy* ya Tanzania umeme una-*account for only 0.6 percent* na wanaotumia umeme ni *only 7 percent* ya *population* yetu.

Sasa *you want to rich the others* kwa hiyo, *you can see* hii *task* siyo ndogo ni kubwa sana. Sasa kama tumeamua mimi nafikiri ni hatua ya kupongeza. Kama tumeamua kuanzia kwa upande huo wa umeme *particularly* katika kufanya *energy* iwe *accessible* pia kwa watu ambao wako mbali kwa maana ya vijijini basi ni vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *energy* kubwa inayotumika hapa nchini ni *energy* ya kuni *(wood fuel).* Takwimu za *World Bank* za mwaka 1997 zinaonyesha mahitaji yetu yalikuwa 89.6%. *I am talking of the total energy* ambayo unataka kuitumia *Tanzania for every and each activity* unayofanya hapa Tanzania. Wakati ule 89.6% ndio ilikuwa inakuwa *accounted for* na kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana nataka niseme hapa suala hili tunaweza tukalipeleka pasipo. Baadaye kidogo Profesa Luhanga na Profesa Mwandosya walitoa tena utafiti wao bado *figure* ikawa imeongezeka *it became 90% okay the difference is 0.7% increase but still* ilikuwa kama ni *confirmation* kwamba tukiongelea mahitaji ya *energy* Tanzania *essentially* tunaongelea *energy* inayotumika huko kwenye maeneo ambayo hayafikiki kwa sababu *it is only 7%* ambayo tunaweza kui-*supply* na *electricity.*

Kwa hiyo, nafikiri hili ni la msingi sana. Kwa hiyo, nataka kwa ajili ya manufaa ya sekta nyingine huko siku za usoni hili lisahihishwe, lieleweke hivyo kwa sababu vinginevyo hapa mimi ningeweza hata kuongelea kwa mfano *cooperates* za *biomass energy* kuna vitu vya namna hiyo *I don't want to go that far* lakini nafikiria hilo ni la msingi kabisa na lazima tulielewe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *definitions* wamemtamka *developer means a developer of or an investor in,* lakini nafikiri bado *ownership* hapa ni muhimu sana kwa sababu tutatumia pesa hapa ambazo zitakuwa zimekusanywa kwa ajili ya kupeleka nishati na nataka nirudie tena umeme huko vijijini ambao utatokana na gridi au utakaotokana na *standalone generator* kama za mafuta, *diesel* na nini au kama ni *solar systems* ambazo tunaziongelea kwa ajili ya umeme lakini bado ni umeme. Nafikiria kwamba hapa ile *ownership* ya hizi *projects* kwanza lazima ifahamike kabisa kwamba nani atakaye-*own* kwa sababu *we know the Government is pulling out, Government* wanataka ku-*support* tu na wakati mwingine wanajiita *facilitators,* vizuri, lakini nani atakaye-*own* kwa sababu hatutaki tukusanye pesa hapa ambapo nyingine inaweza kuwa ni msaada kweli au nyingine italipwa baadaye kama madeni halafu waanze kufaidi watu ambao watakuja kama *investors* kutoka nje, hatutaki kuwapatia *capital* hawa watu. Kwa hiyo, *you can see* kazi inawezekana ikawa kubwa hata kuwa-*organize* watu ambao watataka ku-*invest* inawezekana pia ikawa ni jukumu la Serikali na lazima tufanye hivyo kwa sababu vinginevyo basi hii *energy fund* itamkwe kabisa kwamba haita-*finance projects* ambazo ziko *owned* na *foreigners* ambao wanataka kuja kuwekeza kwenye umeme kule. *This is very important* kwa sababu tusije tukaanza kuwa-*finance* watu wanaotoka nje halafu *in essence* tutakuwa tunafanya *capital flight* kwa sababu hawa watu hawatatunza pesa yao hapa lazima wataipeleka nje, tutakuwa tumetoa pesa nje, watatengeneza pesa hapa watairudisha tena nje kwa gharama yetu, *I think* sio *proper* hiki ni kitu cha msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza huu Muswada kimsingi unaunda Bodi ya Nishati lakini huko ndani wanasema itakuwa na Wakala halafu kutakuwa na ile *fund.* Sasa ukiangalia hii bodi ni kama inaning'inia tu lakini *actually* kazi zitafanywa na wakala halafu wakala *by the way* ndio aliyepewa, ukiangalia kwenye *clause 14(2)* hii ambayo inaangalia *agency* sasa, hapa kwanza kwenye 14(1) wana-*establish* hiyo *agency* halafu 14(2) wanasema: *"the agency shall be a body corporate with perpetual succession"* na vitu vya namna hiyo ni kwamba *legal corporate.*

Nilikuwa najiuliza kwa nini sasa hii bodi inabakia ina-*hang hang* tu ndio ni kwamba bodi itakuwa ina-*oversee* shughuli ya hii *agency* ndio maana nafikiria au tume-*misuse* maneno hapa? Nafikiri ni bora labda tungetamka kwamba ama hii *clause 14(2)* ihame ije huku baada ya *clause 6(1)* ambayo hiyo *clause 6(1)* kwanza ndio inatamka kuanzishwa kwa bodi halafu sasa hiyo bodi ndio iwe haswa yenye hiyo *legal status* halafu hizi *agency* ziwe chini yake kwa sababu *after all* kwa muundo ambao tumeletewa hapa ni kwamba ziko chini yake na hata hii fund itakuwa *managed* na yeyote yule lakini chini ya bodi. Kwa hiyo, nafikiria hili nalo ni la msingi sana ili kupunguza mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nafikiria ni bora tu hata kama wangetamka kwamba Muswada huu ni wa kuunda *agency* ya umeme, hiyo ambayo imesema *establishment of the agency* iwe badala ya bodi kwa sababu ile *agency* sasa ndiyo iwe na bodi kule ndani kama wanataka ibakie hivyo kwa sababu hii *legal status* iko kwenye *agency* basi hii bodi iwe ndio bodi ndani ya *agency* au tuseme hii *agency* iwe inaongozwa na hii bodi ambayo inatamkwa hapa. Kwa hiyo, kuna haja ya ku-*reverse* hii lakini vinginevyo unapata *impression* kama una vitu vitatu ambavyo kimoja kina viwili ndani yake. *It is confusing!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *confusion* utaiona zaidi utakapokuja kuongelea kwa mfano *clause 10(3)* anasema: *"Members of the board shall be entitled to payment of"* malipo yale halafu anaendelea kule chini: *"and which shall be funded from the operational budget of the agency."* Kwa hiyo, *actually operational budget* itakuwa ni *agency.* Mwanzoni nilifikiria labda wamekosea badala ya kuandika *board* wameandika *agency,* lakini nilipoangalia humu ndani nikaamini kweli kwa sababu *operational decisions* zitakuwa chini ya *agency.*

Kwa hiyo, ni kweli kwamba pesa zitatoka pia kwenye *agency.* Sasa hii ndio nauliza kwa nini basi hii bodi iwe peke yake kwa nini isiwe *embodied* au tuseme hii bodi iwe inaongoza ile *agency* yenyewe ndani ya *agency* kwa maana ya kwamba badala ya kusema tunaunda bodi basi tuseme tunaunda *agency* ambayo itakuwa na *fund* mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *establishment of the rural energy fund, clause 17,* wanasema: *"There shall be established a fund to be known as a rural energy fund for the purpose,"* halafu wameendelea pale. Sasa mimi naona kwanza kuna *redundancy* hapo kwa sababu ukiendelea 18(1) ni kama wanarudia kitu kile kile kilichotamkwa hapo baada ya hilo neno purpose kwenye hiyo *clause 17.* Nafikiria hiyo *redundancy* inaweza kuondoka na ni muhimu kwa sababu nafikiri hii *redundancy* pia inaharibu mtitiriko

ambao baadaye unaanza kuukosa kwamba ni nani mkubwa hapa ni bodi, ni *fund,* ni *agency* au ni nani, nafikiri hilo nalo ni muhimu sana. Kwa hiyo, napendekeza kwa mfano pale baada ya neno *the purpose* unasema *of the fund that is, there shall be established a fund to be known as the Rural Energy Fund for the purpose of the funds* na sababu zimetamkwa huku chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikienda ile *ownership* ambayo nilikuwa naitamka Mheshimiwa Mwenyekiti kwenye *clause 18(2)(a)* hapa anasema *grants towards the capital costs of projects implemented by private and public entities* na kuendelea. Sasa hapa *I thought* ni mahali pazuri pa ku-*stamp* ile *ownership* kwa maana ya kwamba tutatumia pesa hizi kama tunapeleka mtaji kwa Watanzania tusije tukawa tunampatia mtaji mtu wa nje *it is not* kwa *interest* yetu kum-*finance* mtu wa nje ambaye baadaye atatoa hizo pesa. Kwa hiyo, nafikiria hapa hiyo *ownership* inaweza kuonekana zaidi kwa mfano ukisema *grants towards the capital costs of Tanzanian owned projects* au *Tanzania an owned projects* halafu *and implemented by private and public entities* na kuendelea. Nafikiri hilo nalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini 18(1)(c) wanasema *the provision of financial assistance,* mimi naona kama ina-*hang* sijaelewa kwa nini imeongezewa basi hata ingetamkwa basi *to whom* na kwenye kitu gani, *on what* lakini vinginevyo nafikiri inaweza kuondoka tu bila madhara yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause 19(3)(c)* na (d) nafikiria zinaweza kuondolewa tu nazo bila madhara yoyote kwa sababu zinazidi kufanya *readability* ya Muswada sio kwamba imeongeza *details as such* lakini nafikiri inaleta *confusion* fulani ambayo nimeona. Kwa sababu ukisoma kwa kufuata mtitiriko huu kwa kweli utakuta kuna vitu ambavyo vinakuchanganya utakuta unakwenda mbele na nyuma. Sasa nafikiri moja ya vitu ambavyo vinachanganya ni pamoja na hii *clause 19(3)(c)* na (d), vikiondolewa itakuwa vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nafikiri kwenye hiyo hiyo 19(3)(a) mwishoni pale anasema: *"...or as may be determined by the Minister for Finance."* Sasa mimi nafikiri hapa tunatakiwa kuamua kama tunafanya hivi vitu lazima tuamue kwamba nani atakuwa *responsible* ili tujue mahali pa kwenda tusije tukakuta kuna *collective responsibility and nobody's responsibility.* Kwa hiyo, nafikiri kuna haja kwa kweli ya ku-*sharpen* ule utaratibu mzima wa kufanya *decisions* kwenye *implementation* ya *project* ambazo zitafanyika chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nafikiri ningependa nisubiri mpaka wakati wa Kamati ya Bunge, nafikiri naweza kupata nafasi nzuri zaidi labda kupewa pia na maelezo ya papo kwa papo. Lakini vinginevyo nataka nisisitize tena Mheshimiwa Mwenyekiti *essentially* ningependa niamini kwamba Muswada huu unataka kujikita katika kupeleka nishati ya umeme vijijini na kwa maana hiyo ni lazima hilo liwe *clear* kwa sababu limewekwa mahali lakini ukisoma Muswada unajielekeza hivyo na kwamba kama tunazungumzia *energy* kama *energy* ni pana kuliko ambavyo imekuwa *covered* hapa

tutakuwa tunafanya *disservice* kwa maeneo mengine ambayo ni sehemu muhimu sana kwa *energy* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla ya kuanza kutoa mchango wangu kuhusu Muswada huu, naomba niungane na wenzangu nitoe rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Mzee Paul Bomani kwa msiba mkubwa ambao umezipata familia hizo na niungane na wenzangu katika kumwomba Mwenyezi Mungu ili aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupeleka nishati ya kisasa vijijini ni suala muhimu sana na kama walivyosema wengine inawezekana tumechelewa sana kulishughulikia kwa kasi au nguvu ambayo tunataka tufanye hivi sasa. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuamua kuja na Muswada huu Bungeni ili angalau suala la usambazaji wa umeme vijijini liweze kushughulikiwa kwa nguvu ya kisheria. Umuhimu wake ni wa wazi kabisa, huko ndiko waliko wananchi wetu wengi zaidi ya 80% wako vijijini na hata uchumi wa Taifa hili kwa kiwango kikubwa sana unategemea shughuli za wananchi walioko vijijini. Kwa hiyo, maendeleo ya Taifa kwa kiwango kikubwa sana yanategemea shughuli za kiuchumi ambazo zinafanywa huko vijijini na wananchi wetu walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu kama ilivyoelezwa kwenye madhumuni ya Muswada ni kusambaza umeme vijijini ili kuweza kuchochea maendeleo vijijini pamoja na kuboresha hali za maisha ya wananchi vijijini, safi kabisa. Kama nilivyosema kwa kweli wakati umefika tuanze kulitazama suala hili kwa nguvu kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningetegemea ili tuweze kufanikiwa na malengo haya ambayo yametamkwa na Muswada basi Muswada huu ungekuja na majibu ya matatizo muhimu ambayo yanakabili suala la usambazaji na utumiaji wa umeme katika nchi yetu hivi sasa. Kuna matatizo mawili kwanza ni usambazaji wenyewe wa umeme kuwafikia wananchi wengi kadri inavyowezekana lakini la pili ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kumudu kuutumia umeme huo. Jitihada kubwa zimefanywa hadi sasa kupeleka umeme katika miji mbalimbali ya Taifa hili lakini kutokana na gharama zake nyingi sote tunajua kwamba si wananchi wengi mijini ambao wameweza kuutumia umeme huo. Kwa hiyo, kama suala la gharama za umeme halikupatiwa ufumbuzi wakati tunafanya jitihada hizi za kupeleka umeme vijijini basi tunaweza kwa kiwango kikubwa tukafanikiwa kama Muswada huu unavyokusudia kusambaza umeme vijijini lakini wananchi wengi vijijini wakashindwa kuutumia umeme huo kutokana na gharama zake kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilitegemea ninapousoma Muswada huu angalau nilione hili linajitokeza yaani mipango, mikakati au makusudio ya wazi kabisa ambayo yanalenga kuwasaidia wananchi hawa ambao tunakusudia kuwapelekea umeme na tatizo hili la gharama kubwa za umeme. Maana kama umeme huu ambao

tutaupeleka vijijini utafika huko na gharama hizo hizo kama zilivyo hivi sasa kwa hakika tutakuwa hatukufanikiwa katika lengo letu kwa sababu nina hakika kabisa kwamba wananchi wengi hawataweza kuutumia umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tunavyo vijiji ambavyo tumefanikiwa kufikisha umeme wa gridi huko lakini kama sote tunavyoshuhudia ukipita katika vijiji hivyo utakuta ni wananchi wachache sana ambao wamevuta umeme huo na wanaoutumia sana sana ni wenye biashara ndogo ndogo ndio wameweza kufanya hivyo lakini mkulima wa kawaida kijijini hakuweza kufanya hivyo.

Katika Jimbo langu la Bahi ninacho kijiji changu kimoja ambacho kiko katika umeme wa gridi ambao unakwenda kwenye Studio za Redio Tanzania Kanda ya Kati, wamefanikiwa kuwapa umeme pale lakini idadi ya wananchi ambao wameweza kuutumia umeme huo mpaka sasa ni wachache sana na wengine wameshindwa kufanya hivyo kwa sababu ya gharama zake. Hata ukitoka hapa kwenda Dar es Salaam viko vijiji vingi njiani hapo vimepewa umeme huu wa grid lakini kama ilivyo katika vijiji vingine vyote watumiaji wa umeme huo ni wachache sana kutokana na gharama zake kuwa kubwa. Kwa hiyo, suala hili la gharama za umeme haliwezi kupuuzwa hata kidogo katika azma yetu ya kupeleka na kusambaza umeme vijijini kwa lengo la kuchochea maendeleo vijijini na kuboresha hali za maisha vijijini. Lazima suala hili la gharama lipewe kipaumbele.

Sasa nasema nikisoma Muswada mzima sioni hiyo ikijitokeza badala yake naona kwamba Muswada huu umejielekeza kama wenzangu wengi walivyosema katika kuwasaidia hao ambao watakuwa wanatekeleza miradi hiyo ya umeme kupeleka vijijini kuwasaidia katika gharama za miradi hiyo *(capital costs)* ili waweze kutekeleza miradi hiyo. Sasa nia hiyo ni nzuri, azma ni kuhakikisha kwamba tunapeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningependa Serikali inisaidie au ituhakikishie namna ambavyo wanafikiri kwa kuwasaidia hao watakaokuwa wanaendeleza miradi hiyo katika gharama za ujenzi wa miradi hiyo namna ambavyo kwa kufanya hivyo tutakuwa vile vile tunawasaidia watumiaji wa umeme huo yaani wananchi ambao tunawapelekea umeme huo. Je, kwa kuwapa unafuu huo, maana tena hatuwasaidii kama mikopo ni misaada na ruzuku tena vyanzo vya fedha za mfuko huo utakuwa ni pamoja na Bajeti ya Serikali lakini kuna ushuru kutokana na uzalishaji wa umeme kwenye nguvu ya gridi na vyanzo vingine vya umeme kwa matumizi binafsi ambavyo vyote hivi vinaweza kuwa vinachangiwa na watu wengi.

Lakini hasa katika hili kwamba mfuko huu utategemea vile vile Bajeti ya Serikali ambayo Watanzania wote tutakuwa tunachangia, je, Serikali inaweza kutuhakikishiaje kwamba kwa kutumia fedha hizo ambazo moja ya chanzo chake ni Bajeti ya Serikali manufaa watakayopata hao watakaosimamia miradi hiyo, watakaojenga miradi hii ya kupeleka vijijini, manufaa hayo vile vile yatawafikia wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena kilichonishangaza ni kwamba katika Kifungu cha 22 cha Muswada huu ni marufuku kwa fedha zitakazotokana na mfuko huu wa kupeleka umeme vijijini kusaidia gharama za uendeshaji wa miradi hiyo. Mimi nilitegemea labda

kama tungesaidia au tungetoa ruzuku kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa miradi hiyo ya umeme vijijini ingeweza kuwasaidia kuwafanya hao watakaopeleka umeme huo kupunguza angalau gharama za umeme unaokwenda vijijini lakini kusaidia zile gharama zao za uendeshaji hairuhusiwi isipokuwa tu kusaidia gharama za ujenzi wa miradi yenyewe. Sasa kwa kufanya hivyo tunawasaidiaje wananchi katika suala hili la gharama za umeme? Kama hilo haliwezi kutiliwa maanani na likatafutiwa ufumbuzi basi hata kama tutafanikiwa kuusambaza umeme vijijini, tukapeleka umeme katika vijiji vingi bado unaweza kukuta watumiaji wakawa wachache sana na kwa hiyo manufaa yanayotegemewa na Muswada huu ambapo moja kubwa ni kuchochea maendeleo na kubadili hali ya maisha vijijini hayatafikiwa kwa misingi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwenzangu mmoja amezungumza muda mfupi uliopita kwamba hawa ambao tunawategemea kuja kuendeleza miradi hii ya kupeleka umeme vijijini natumaini hawatakuwa Watanzania tu watakuwepo hata watu wa kutoka nchi za nje. Sasa kama tutachukua fedha zetu za bajeti tunachangia mfuko huu, mfuko huu unasaidia wageni na labda na Watanzania wachache hatimaye tunaweza kujikuta sasa tunasaidia watu ambao baadaye watahamisha fedha kupeleka kwao na sisi tusipate manufaa yoyote. Mimi naomba sana hili suala la mkakati huu ambao mkazo wake ni watekelezaji wa miradi labda lingeangaliwa upya na tuangalie namna tunavyoweza kutoa ruzuku kwa ajili ya walaji wenyewe, watumiaji wa umeme huko vijijini.

Hii kengele ilikuwa ya kwangu au ya mtu mwingine?

**MWENYEKITI:** Ya kwako.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kurudia suala moja ambalo niliwahi kulisema hapa wakati tulipokuwa kwenye semina iliyohusu umeme kwa wote. Niliwahi kuongelea juu ya suala la kuvuta umeme kutoka hapa mjini na kuufikisha Bahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tulilizungumza wakati mkandarasi wa ujenzi wa barabara kutoka hapa Dodoma mpaka Manyoni alipokuwa anaanza kazi yake. Alikuwa na lengo la kuvuta umeme toka hapa mjini mpaka Bahi ambapo alitegemea kuweka kambi yake kuu kwa kushirikiana na *TANESCO* ambao ndio wenye jukumu la kusambaza umeme hapa nchini. Tulikubaliana suala hili katika kikao tukiwa na Naibu Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na tukawa tumeliacha kama suala tu la utekelezaji. Lakini kadri nilivyoendelea kulifuatilia suala hili, taarifa nilizopewa ni kwamba *TANESCO* hawakutaka kushirikiana na mkandarasi huyo ambaye alikuwa tayari angalau kutoa sehemu ya gharama ya kuvuta umeme huu mpaka Bahi ambapo baadaye ungeendelezwa hata kwenda kwenye Jimbo la jirani yangu, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati mpaka Manyoni.

Lakini kinachonishangaza ni kwamba hata baada ya kupata mtu ambaye yuko tayari kuchangia katika gharama ambazo kwa kweli ni jukumu la *TANESCO* inafika mahali wao wenyewe hawaonyeshi ushirikiano wowote. Hili ni jukumu lao na kama sio leo hata kesho na sisi wa Bahi huko tunahitaji kuwa na umeme. Sasa wanaipoteza nafasi

hii ya mtu ambaye alikuwa tayari kuchangia halafu baadaye wanaweza kulazimika kubeba mzigo wote wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa naomba, niliomba wakati tulipokuwa kwenye semina hiyo maelezo ya Serikali kwa nini *TANESCO* hawakutaka kushirikiana na mkandarasi ili kuvuta umeme huo mpaka Bahi? Jibu sikupewa.

Sasa naomba basi leo kwa sababu wananchi wote huko walijua kwamba umeme unakwenda kwa ushirikiano kati ya *KONOIKE* na *TANESCO* mpaka Bahi ambao ungesaidia vile vile katika vijiji vya Kigwe, Ibihwa, Mpamandwa na Bahi yenyewe. Basi angalau tupate maelezo sio mimi tu lakini na wananchi huko wasikie kwa nini suala hili lilifika mahali likakwama. Kama ni *TANESCO,* tujue maana ni jukumu lao kwa nini hawakutaka kuichangamkia nafasi hiyo waliyokuwa wamepata ya mtu mwingine kuchangia kwa kiasi chochote kile ambacho angechangia hata kama angechangia kiasi kidogo au vipi lakini ingekuwa ni kwa manufaa yao kabisa. Sasa wamemlazimisha mkandarasi huyu anatumia *generator* njia nzima sasa sijui kama ni kwa unafuu wake au ni kwa gharama zaidi lakini nina hakika kama *TANESCO* wangeweza kutoa ushirikiano uliotakiwa labda gharama zingepungua kwa kila upande na sisi tungelipia tu kama watu wengine sio kwamba tulikuwa tunauhitaji huu umeme ili labda tusilipie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa Muswada wenyewe mengi wamekwishazungumza wenzangu kwa kweli nilichofanya ni kusisitiza tu kwa yale ambayo nafikiri ni muhimu sana. Kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono Muswada huu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada wa Nishati Vijijini, Muswada ambao unaendelea kujadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia Muswada wenyewe, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa familia, ndugu na wananchi wa Jimbo la Rahaleo kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu marehemu, Balozi Ahmed Hassan Diria. Hali kadhalika nitumie nafasi hii kutoa pole kwa familia na ndugu wa Marehemu Balozi Paul Bomani, kufuatia kifo chake. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote wawili mahali pema peponi, *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu sana kwangu mimi na kwa wananchi wa Jimbo langu la Nanyumbu. Kwa miaka kadhaa sasa nimekuwa nikiomba Serikali kupeleka umeme Nanyumba bila mafanikio. Serikali imekuwa inatoa sababu mbalimbali wakati mwingine sababu hizi zinapingana. Nakumbuka kuna wakati hata tulielezwa gharama za kupeleka umeme Nanyumbu lakini sababu ambazo zimekuwa zinatolewa ni za kusubiri umeme labda wa makaa ya mawe Mchuchuma, umeme wa gesi *Mnazi Bay* na wakati mwingine umeme ulioko Masasi hautoshi lakini umeme ule wa Masasi kwa kweli umesambazwa katika Wilaya kadhaa za Mikoa ya Lindi na Mtwara na umeme ule ni wa uhakika kuliko umeme mwingine ambao unapatikana sehemu zile za Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Muswada huu, nashawishika kuamini kuwa Serikali imeshindwa kupeleka umeme Nanyumbu kwa sababu ilikuwa hailazimiki kisheria, hakukuwa na Muswada wowote au sheria yoyote ambayo ilikuwa inaifanya Serikali ipeleke umeme Nanyumbu. Lakini sasa kwa Muswada huu naamini kuwa sasa Serikali itapeleka umeme Nanyumba. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kutamka mapema kabisa kama hiyo ndio nia basi, naunga mkono Muswada huu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna nyanja ambayo wananchi wa Jimbo la Nanyumbu hawajaona maendeleo yake basi ni la nyanja hii ya umeme au nishati. Licha ya Masasi kama nilivyoeleza kuwa na umeme wa uhakika lakini watu wa Nanyumbu bado hawajabahatika kupelekewa umeme. Kwa hiyo, naomba kupitia Muswada huu au sheria hii itakapokubaliwa basi Jimbo la Nanyumbu lifikiriwe haraka zaidi ili lipelekewe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Muswada sehemu ya pili, Ibara ya nne kuwa kupeleka umeme vijijini kunaharakisha ukuaji wa uchumi, kiuzalishaji na kitija pamoja na ustawi wa jamii siyo kwa vijijini tu bali kwa nchi nzima kwa sababu maendeleo ya kweli ni yale ambayo yameenea nchi nzima. Kutokana na umuhimu huo suala la Serikali kujitoa katika usambazaji wa umeme vijijini lisiwepo kabisa kama walivyozungumza wenzangu.

Pale ambapo watu binafsi, Mashirika binafsi, Makampuni binafsi na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Vikundi vya Ushirika vimeshindwa kupeleka umeme vijijini ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa maeneo husika nayo yanapata umeme ndiyo maana tunasisitiza suala la Serikali kushirikiana na makampuni hayo binafsi kuhakikisha nchi nzima inapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasambazaji binafsi watakuwa ni wafanyabiashara na lengo lao kubwa ni kutengeneza faida hivyo watapeleka huduma zao pale ambapo wataona watapata faida lakini zile sehemu ambazo wataona hawatapata faida hawawezi wakapeleka huduma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inaweza ikaigawa nchi yetu katika makundi mawili, kundi la kwanza lenye maendeleo kwa vile tu wanapata umeme na kundi lingine ni lile lisilokuwa na maendeleo kwa sababu tu wamekosa umeme. Naomba Serikali isitufikishe huko kwa yenyewe kujitoa katika usambazaji wa umeme, kinachotakiwa Serikali ku-*balance* usambazaji wa umeme ili kule ambako wafanyabiashara hawataki kwenda au wanasita kwenda basi Serikali ndiyo ichukue jukumu la kwenda kusambaza umeme. Kwa namna hiyo nina uhakika nchi nzima itakuwa ina maendeleo na maeneo yote yatakuwa yamepata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imejaaliwa na vyanzo vingi vya umeme kuanzia maji ya mito, makaa ya mawe, gesi na mabaki ya miwa ukiachilia mbali mafuta ambayo bei zake huendelea kupanda kila kunapokucha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inazungumzia uundaji wa *Board* ambayo itakuwa na kazi ya uhamasishaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini kwa kuwezesha upatikanaji wa umeme katika uzalishaji kiuchumi, afya na elimu, maji safi, usalama wa raia na hata matumizi majumbani. Ili kufanikisha hilo *Board* itakuwa inatoa ruzuku kwa wasambazaji binafsi na vikundi vingine, hapa ningependa kuiomba *board* hiyo kuwa makini katika utoaji wa ruzuku hiyo ili ruzuku hiyo isiende sehemu zile ambazo tayari kuna umeme na kuacha maeneo ambayo bado hayajapata umeme.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia wametaja baadhi ya maeneo ambayo hayana umeme hivyo na mimi nisingependa kuyarudia kuyataja, lakini uzoefu umeonyesha au unaonyesha kuwa siyo wote wanaopewa ruzuku kutumia kama inavyotakiwa hivyo *Board* lazima iwe makini sana kwa kuhakikisha kuwa ni vile vikundi tu vitakavyotumia ruzuku hizo katika kusambaza umeme vijijini ndiyo vinapewa ruzuku. Kuna wengine wanatumia ruzuku hizi kwa shughuli ambazo siyo walizoombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, Ibara ya tatu inazungumzia juu ya kumpata Mwenyekiti wa *Board,* bahati mbaya Muswada hauelezi Mwenyekiti atatokana na wajumbe wa *Board* au la pamoja na kueleza kuwa atachaguliwa na wajumbe wa *Board* na kuridhiwa na Waziri. Kwa hiyo, kwa nafasi muhimu kama hiyo ni vizuri Muswada ukaeleza Mwenyekiti atatokana na watu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ulianza kujadiliwa wiki iliyopita na Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia na mengi yamesemwa hivyo na mimi nilikuwa najazia hapa na pale naomba basi nimalizie mchango wangu kwa kuishukuru Serikali kuleta Muswada huu ambao utahakikisha kuwa umeme unapatikana vijijini ili kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe machache tu kuhusu Muswada tulio nao hapa mbele yetu.

Kabla ya kuchangia mawazo yangu nadhani nitaunga mkono wenzangu wote walionitangulia katika kutoa rambirambi zangu za dhati kwa wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mheshimiwa Balozi Ahmed Diria na Balozi Paul Bomani pamoja na rambirambi hizo ziende kwa Mikoa yao au Majimbo kwa Bwana Ahmed Hassan Diria alilokuwa analiendesha.

Kuhusu Muswada wenyewe mimi sina mengi ya kusema labda mawili matatu hivi halafu nitasema yale ambayo ni ya jumla.

Kwanza nitoe pongezi ya dhati kabisa kwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yao ya wataalam kwa kutengeneza Muswada ambao umeletwa hapa kwa wakati muafaka na tumeutafakari kwa muda mrefu pamoja na kutupa maarifa ya semina ambayo

tumekaa nayo sasa hivi siku ya tatu ya nne. Nampa pongezi kwani Muswada ni safi na umekuja wakati mzuri na kuna haja tu baadaye labda kupitia vipengele vichache hapa na pale kuufanya uboreke zaidi hasa baada ya kusikia mchango wa Wabunge waliotoa siku hizo mbili, tatu.

Kwa upande wangu ninayo mawili, matatu hivi, kwanza kabisa iko ile *source* ya *funds* sasa hili wengi wamelisemea kwa kuwa Serikali inataka kujiweka pembeni tunasema hapana kama itajiweka pembeni lakini kwa mimi nasema kwa moja hilo la kutafuta fedha liwe mstari wa mbele Serikali iwe mstari wa mbele na hasa watoe hoja kama ile iliyojengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya *Road Funds* na hiyo ndiyo tuwe nayo kuwa tuwe na *Energy Fund, Rural Energy Fund* ambayo itaweza kuwasaidia *agency* yenyewe pamoja na wale watu wachache wanaoweza kuingia kwenye sekta hiyo ya kuzalisha umeme. Nadhani wengi wanataka kuzalisha umeme kwenye *Mini-hydras* wengine kwenye mkaa, kwenye gesi na kadhalika lakini wanashindwa kwa sasa hivi sheria haiwapi nafasi kusema kama watabanwa na mtiririko wa fedha waende wapi, lakini kama *fund* kama hiyo itakuwepo watasema wanaweza kupata *subside* na msaada kidogo wengi wataingia katika hiyo shughuli ya kuzalisha umeme, hiyo ni moja kuwa tutengeneze *Rural Energy Fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, nilikuwa na wasiwasi na ukurasa ule wa 51 ambapo Waziri anataka tumpe madaraka ya kufukuza *board* yake, ukurasa wa 51 *section* ya 9 (3) inasema: *"The Minister may suspend the appointment of Member including the Chairman,"* nikadhani kuwa hiyo anatafuta utata wa bure tu kwa kuwa *board* ameichagua yeye mwenyewe na ameipa nafasi kule ya kuteua *chairman* wajichague kule kati yao halafu kati yake na Rais wanaweza kufanya hayo bila kuiweka kwenye sheria maana hii nakumbuka mwaka juzi tulikuwa tunabishana hapa juu ya *NMB* kiasi kuwa Waziri akaenda kumwambia Rais kuwa ile Benki haifai kabisa labda *Board* mbaya kumbe *Board* ilikuwa right na sisemi kama Waziri hakuwa right ila inaelekea kuwa *NMB* iliendelea vizuri na zaidi siyo kama ilivyo Mawizara sasa tulifukuza *Board* kwa makosa na wakapewa watu wengine sifa ya kuwa wamefanya vizuri lakini kwa kweli ilikuwa ni mtiririko wa *information* haukuwa *proper* na haukuweza kuchukua maamuzi yote kwa kuwa nasema yeye Waziri angejitoa kwenye hilo aiachie hapo.

La tatu, sikuona mahali panaposema *specifically* kama *TANESCO* wata-*deal* na hizo *private* pamoja na umeme wa jumuiya za kidini au wananchi wenyewe *Community Based* Umeme watakaotengeneza watahusiana vipi na *TANESCO,* na kama *TANESCO* itakuwa katika *format* hiyo hiyo iliyopo au itabadilishwa kama ilivyokuwa inasemwa miaka iliyopita miwili, mitatu kuwa watai-*decentralize* kuwe na sehemu tatu za *TANESCO* nina wasiwasi hapa kwa kuwa kwa kweli *TANESCO* sasa hivi wana *power* ya kuhodhi madaraka ya umeme, kutengeneza umeme, kusafirisha pamoja na kusambaza, kazi zote tatu sasa mara nyingi wanasema kuwa wewe ukitengeneza umeme binafsi wewe uende kuongea na *TANESCO* ndiyo yeye atakayekuwa mnunuzi wa kwanza na wa mwisho kwa hiyo ikiwa bado itakuwa ni utaratibu huo itakuwa vigumu sana kwa *private sector* hata mashirika mengine ya Serikali yanayotaka kutengeneza umeme yanashindwa kuendelea kutengeneza kwa kuwa ile sheria inamlinda sana *TANESCO* na *TANESCO*

anaiona kuwa hiyo ndiyo hasa nafasi yake ya kuwaambia hawa wamsaidie kutengeneza pesa.

Sasa ningependa kwenda labda mambo yale ya jumla, ya kwanza nilisema kuwa umeme kusini umechukua miaka 40 kufikiriwa, kufikiriwa tu na haujaenda bado kwa mikoa ile ya kusini, kusini yote siyo kusini Mtwara na Lindi peke yake ila Lindi, Mtwara, Ruvuma pamoja na Rukwa ni sehemu ambayo umeme haupo hata ukiona waya siyo waya labda kamba tu za porini za miti, miaka 40 ni giza tu na kama tutakwenda kwa mtindo huu nadhani tutakuwa na miaka mingine 40 miaka 40 labda tutaweza kuwa na umeme lakini kwa sheria hii ikipitishwa nadhani Waziri atakuwa na nafasi ya kuanza na kutengeneza umeme *Rural Electrification* na mikoa hiyo minne ya Kusini, kusema kuwa kule aanze kwanza kutengeneza miundombinu ya kusambaza umeme sasa hivi kusudi itakapokuja umeme wa gridi miaka miwili mitatu ijayo ikute ile miundombinu ya vijijini iko tayari pale lakini tukifuata mtiririko uende kwanza gridi ya Taifa halafu tuende vijijini hivyo vijiji vya kusini vitapata umeme labda mwaka wa 3,000 na siyo katika karne hii ya sasa.

Lingine nilotaka kulisema ni kwa sehemu hiyo ya nchi ambayo iko kusini ina nafasi kubwa sana ya kuongeza uchumi wa nchi hii, sasa hivi tunaangalia *Mtwara Development Corridor* lakini wengi tunayo mawazo finyu tu ya kusema kwa ajili ya hasa kwa mikoa ile mitatu au saba ambayo iko Kusini lakini kwa kweli mikoa ile saba Kusini ndiyo hasa *future* ya nchi yetu ya Tanzania nzima. Kule ndiko kunakotoka chanzo kikubwa cha umeme kitakuwa kule tukisema maji hayatatengeneza umeme kama walivyosema wasemaji wengi hapa basi itabaki zaidi ni mkaa, gas hatuna uhakika iko kiasi gani labda itakuwa nayo pia lakini mkaa ndiyo utakuwa hasa chanzo kikubwa cha umeme na mkaa uko sehemu hiyo ya *Mtwara Corridor* kuanzia hiyo Ruvuma kuja Mbeya kwenda mpaka Rukwa, kule ndiko kuna mkaa na ni mkaa mwingi sana kwa hiyo na hiyo italeta hasa maendeleo ya viwanda tuseme kuwa kama gesi ya Songosongo ingetengeneza umeme mkubwa viwanda vianze pale Kilwa, kuna malighafi ya *gypsum* kuna malighafi ya kutengeneza *cement,* kutengeneza mbolea, kutengeneza chumvi, iko chumvi pale *deposit* kubwa kuliko hata ile ya kule Kigoma na hiyo ina mazao tena mengi sana mle ndani yanayoweza kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lindi na Mtwara wataweza kuwa na *Fishing Industries* zinaweza kuwa pale, *agriculture processing* hata kufufua yale mashamba makubwa ya *OFC* ambayo yalijenga *Mtwara Port* lakini yakashindwa lakini yale yanaweza kufufuliwa siyo kwa ajili ya karanga peke yake ila kwa *oil seeds* za kila aina zinaweza kufanyika pale. Halafu kama *smelting* kama wenzetu wa *Mozambique* wana *smelter* moja tu, uchumi wao uko *above 10% per year* kwa ajili ya *smelter* tu moja ya bati lakini wanategemea kuweka ya pili, sisi tunaweza kuweka *smelter* pale Mtwara kwa ajili ya chuma na bila shaka kwa ajili ya *copper,* kuna *copper,* kuna *manganese* tunaweza kuweka *smelters* mbili pale zikaleta uchumi wetu ukakua kwa haraka sana.

Ukienda Ruvuma ndiyo nilikosema kuwa ndiyo nyumbani kwa *coal,* kuna zaidi ya site kama saba hivi za *coal* ambazo zipo tu katika Mkoa wa Ruvuma zinazoweza kuchimbwa tukatengeneza umeme, mafuta, lami kutokana na hayo tu mazao mengine

mengi tu kutokana na hata mafuta uzuri toka hiyo *coal* yako mahali pa kuchimba shaba, haya ni *proven* na yanaweza kuchimbwa na kutengeneza umeme hata mpaka kama ni *megawatts 2,000* tunaweza kutengeneza toka sehemu hiyo, Iringa wanayo Mchuchuma, Liganga, wanaweza kutengeneza umeme pia kwa kutengeneza mazao mengine na kadhalika.

Kwa hiyo, nasema tu kwa upande wetu ingekuwa inaweza kuwa na maarifa hayo ya kuendeleza sehemu hiyo kwa kupeleka umeme kwa kuanzisha viwanda vyenye uzito tungekuwa tunaweza kuwa *at a rate of more than 15% per annual ili by year 2025* tutakuwa *a Newly Industrialized Country* na labda kabla ya hapo tungeweza kuwa katika mtiririko ule wa Malaysia au Brazil au *Latin America* kuwa ingeweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria sasa la mwisho ni kuwa tunafikiria kwa upande wa *NDC* wanajaribu kutengeneza kitu kinaitwa *Mega Project,* fedha duniani ziko nyingi sana, dunia yote ina fedha nyingi na inatafuta miradi na miradi wanayotafuta ni mikubwa kama ni *private sector* hawataki miradi midogo midogo ya dola 25, 45, 50, 1,000,000, wao wanataka kubwa ya *billions of dollars* na sisi kule tunaweza kutengeneza mradi kama huo tuki-*base* kuwa tuna *coal* pale Mchuchuma ambayo itatengeneza umeme na *coal* hiyo hiyo itapeleka umeme Liganga. Liganga kama ikiwa *fully operational* inahitaji zaidi ya *megawatts 500* halafu kama tutaweka *Rail Electrified* kwenda Mtwara itahitaji zaidi karibu *1,000 megawatts* kwa hiyo inaweza kuwa ni Mchuchuma nadhani ya kwanza ni *Mchuchuma Coal for power and beneficiation* ya *Liganga Iron Ore - smelter for steel and steel alloys; using Titanium, Vanedeum, Manganese and Huge Port at Mtwara and Electric Railway Mtwara - Masasi - Tunduru - Songea - Mauda via Mchuchuma Branch line. Mchuchuma - Liganga Electric Railway with facilities for Automatic loading and off loading.*

*The magnitude of this Mega Project in terms of Amendment approxmately US dolla 3 - 5 million.*

*This project can be implemented in 10 to 15 years, well a head of 2025.*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Ya pili, *okey* ahsante, mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Job Ndugai, ndiye msemaji wetu niliye naye kwenye *list* mpaka sasa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu. Katika kuanza kwa vile ni mara ya kwanza naongea safari hii na mimi nitoe salaam za rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Kongwa kwa vifo vilivyotokea kwa Ndugu yetu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mzee wetu Balozi Paul Bomani na Papa John Paul wa Pili, tunamwomba Mwenyezi Mungu roho za marehemu zikae mahali pema peponi. *Amina.*

Vile vile nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri Makadinari ambao wanaanza kukaa leo kule Vatican kutupatia Papa atakayefuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema naunga mkono hoja na napongeza sana zoezi hili linaloendelea lililoletwa na Serikali hapa mbele yetu kwa ajili ya uundwaji wa *agency* ya Umeme Vijijini na Mfuko ambao utawezesha zoezi zima la umeme vijijini kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunajua kwamba nishati kubwa ambayo imekuwa ikitumika hadi sasa vijijini na kwa sehemu fulani mijini katika maeneo wanayoishi maskini ni kuni, wataalam wenyewe wanakadiria ni asilimia 85 ya matumizi ya nishati ni kuni na umeme wanakadiria kwenye asilimia sita au saba kwa matumizi ya nchi nzima kulinganisha na matumizi ya wananchi wote. Matumizi haya ni madogo sana tena yako sehemu za mijini peke yake.

Kwa hiyo, iko kila sababu ya kufikiri namna gani tunaweza kupeleka umeme kwa hawa wananchi karibu asilimia 90 ambao mpaka hivi sasa huduma hii muhimu haijaweza kuwafikia. Imeshaelezwa na wachangiaji waliotangulia kabla yangu athari kubwa ambayo nchi hii inapata kutokana na matumizi makubwa sana ya kuni mojawapo likiwa hili la misitu kupotea kwa haraka sana na matatizo yake mengi sana ambayo yaambatana na zoezi hilo.

Lakini vilevile ziko athari za kiafya za matumizi ya kuni yanayoendelea hasa baadhi ya miti ambayo si mizuri sana ambayo moshi wake unasababisha asthma, tatizo ambalo hata mama yangu mzazi ana tatizo hilo kubwa sana inambana mara kwa mara kutokana na matumizi haya ya kuni ambazo baadhi yake moshi wake una athari kubwa sana. Tungekuwa na umeme labda maradhi kama haya yasingewapata wazee wetu hawa, kwa hiyo, ni jambo jema la kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii tunaanzisha *agency, Board* itakayoendesha hiyo *Agency,* tunaanzisha Mfuko na kutakuwa na chombo au kitu kinaitwa *Trust Agent* sasa nikianza na *Board,* walikwisha eleza wenzangu na mimi nipitie hapo kwamba *Board* hii iliyoko hapa haipendezi sana lakini sasa hivi tunapozungumza ni mwishomwisho sidhani kama Mheshimiwa Waziri ataweza kubadili chochote lakini tuweke tu kwenye kumbukumbu.

*Board* hizi zinazoundwa na Makatibu Wakuu zimekuwa nyingi sijui maana mwaka una siku 365 tu tukizidi kuwaongezea hawa watu kila siku kila aina ya *Board* watu walewale sijui watafanya kazi lini na hawa watu wako *busy* sana na haya mambo tunayoanzisha ni mambo muhimu sana na mimi naamini wako Watanzania wengi wenye muda wa kutosha wa kufanya shughuli hizi na si vizuri kila sheria inayokuja iwe inaweka Makatibu Wakuu kuwa ndiyo *board members.*

Lakini vilevile ukiangalia kwa suala la umeme vijijini ukiacha Makatibu Wakuu ambao hawaishi huku vijijini jambo wanashughulikia baadhi mambo yao vijijini lakini

wapo  Wawakilishi kutoka *Tanzania Bankers Association* hakuna mabenki huko vijijini, wako hawa *Tanzania Chamber of Mines and Energy* sawa wana *interest* lakini ndiyo hivyo hawa wako Wajumbe *Tanzania Confederation of Industries,* viwanda vingapi viko vijijini? Kwa hiyo, ukiitazama hiyo *Board* kwa ujumla ina wazito lakini wadau wenyewe hasa wa vijijini ni pamoja na Wabunge hawa wa vijijini ambao hawamo kabisa kwenye *Board* kama hizi.

Kwa hiyo, ingawa tumechelewa lakini ndiyo hivyo, hata unaposema Mheshimiwa Waziri awe na uwezo wa kufukuza *Board,* hata ukiifukuza utakapoiunda tena unaunda Makatibu Wakuu walewale kwa hiyo *more less* wanarudi watu walewale *more than 50%* ni walewale kwa hiyo inakuwa haibadilishi sana *content* kama nia ilikuwa ni hiyo katika kuvunja *board* za aina hii ambazo zinaundwa kwa maofisi ya watu kwa uwingi wao katika *board* husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni-*comment* kidogo kwenye hawa wanaoitwa *Trust Agent* ambao jukumu lao kubwa litakuwa *disbursement* ya *grant payments.* Huyu *Trust Agent* anafanya *almost* kazi ya fund ndiyo kazi zake hasa *fund* ilipaswa ifanye sasa sijui ni sababu zipi zilizosababisha atafutwe huyu *Trust Agent,* wanasema atakuwa *responsible* kwa masuala ya utawala wa hizo *Payaments, Financial  Disbursements* na *monitoring* ya *activities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunaongeza majukumu baadaye inaongeza gharama za uendeshaji, wakati upo mfuko hapa na huu mfuko ndiyo ungefanya *disbursements* hizo ndiyo ungefanya *monitoring activities* na ku-*verify* mambo yote yanayoendelea kule lakini labda kuna sababu za msingi za hiyo nitaomba tu kama muda utakuwa unaruhuru tueleze zaidi hii *Trust Agent* umuhimu wake mkubwa ni nini hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa kwamba kutakuwa na uchangiaji au makato ya namna moja au nyingine ya asiliamia 5 ambayo yataingia katika huu Mfuko maalum kwa ajili ya usambazaji wa umeme vijijini kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya watumiaji, hili ni jambo jema  ili mradi tu jambo hili halitaongeza tena bei ya umeme ambayo tayari ni mzigo sana kwa watanzania ambao wanalia kwamba bei ya umeme ni kubwa sana hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu na mimi nisisitize sana kuhusu suala la Serikali kukaa kando na kuwa *facilitator* hili limetupa uoga wengi wetu sote kabisa hapa, tungependa kabisa Serikali isijitoe katika suala zima la kupeleka na kuendesha huduma za umeme vijijini, Serikali i-*provide* na i-*facilitate* na Serikali ndiyo iweke vipaumbele vya usambazaji. Suala la kuwa na *developers* ni zuri, *developers* binafsi, Washirika, Makampuni ni zuri lakini ni tata kwa sasa hivi kwa sababu hawa *developers* watapata *grant support* kutoka kwenye *Board* yetu hii na Mfuko wetu, watakuwa wanapeleka miradi yapo kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wetu ni kwamba suala la *equity* hapa litaenda vipi inawezekana hawa waombaji wakaomba miradi mingi kwenye eneo moja la nchi yetu wasipende sana kuomba kugawa umeme kule Kongwa na sisi *Board* tunagawa miradi kadri ilivyoombwa, ndivyo walivyoomba hawa kwa hiyo maeneo mengine yanakuwa hayawezi kupata huduma hii ni wasiwasi.

Kwa hiyo, tutaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie atakapokuwa ana- *wind up* kutuondolea wasiwasi huu wa suala la vipaumbele ataweka nani kwani ni vizuri hao waombaji waombe katika vipaumbele ambavyo vimeshawekwa na Serikali vinginevyo itakuwa tatizo kubwa sana. *Project Proposals* zitakuwa zinaegemea pande fulani za nchi kwa sababu za kiuchumi tu na urahisi wa mambo na kadhalika.

Kama tunavyojua kupeleka umeme vijijini ni *capital intensive,* kwa hiyo, watu watapenda mahali ambapo pana vijijini lakini ni miji midogo zaidi na ningeshauri kama walivyosema wenzangu tutumie zaidi kile kitengo cha umeme vijijini cha *TANESCO* kilichopo hivi sasa ambacho tayari kina uzoefu mkubwa sana wa kusambaza umeme vijijini basi ikiwezekana hawa ndiyo waanzishe hii *Agency,* litakuwa ni jambo zuri sana tutakuwa tumeendeleza jambo ambalo lilikuwepo toka mwanzo kwa sababu wanachokosa hawa hadi sasa hivi zaidi ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tunaanzisha chombo hiki muhimu na chombo hiki katika kufanya kazi zake kwa namna moja ama nyingine watapitia *Hansard* zetu kuona Waheshimiwa Wabunge wakati wanaanzisha chombo hiki walikuwa wana *spirit* ipi nichukue fursa hii vilevile kukumbusha kwa hicho chombo maombi yetu sisi watu wa Kongwa ya muda mrefu sana ya kusambaza umeme vijijini katika maeneo ya kutoka pale *NARCO* kuelekea Chamae, Hogoro, Songambele, Mkoka, Matongoro na Norini kama mradi mmoja ambao tumeuomba mara nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri sasa chombo hiki kinapokuja basi kitoe kipaumbele kikubwa sana hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa mradi wa Pandambili, Hembahemba na Njoge haya ni maeneo ya wakulima wanaojitahidi sana kupiga hatua kubwa sana za maendeleo ndiyo wanaotupa sifa sisi Kongwa kwa kilimo kikubwa kinachoweka soko la kimataifa la Kibaigwa pale, wakulima hawa wanajitahidi sana kununua matrekta yao wangependa kuchomeleachomelea na kufanya maintance ndogondogo ambazo hawawezi kufanya bila nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumalizia kwa kurudia tena kusema tena kwa kweli miradi ya umeme vijijini ni gharama kubwa *returns* zake huchukua miaka mingi kidogo kwa hiyo wawekezaji binafsi hawangependa kuwekeza katika kitu kinachoitwa umeme vijijini kwa hiyo ni lazima Serikali tujitoe na ninaamini katika zoezi hili ndiyo Serikali inajaribu kutekeleza sasa kwa kujitoa ili kuwekeza fedha zetu katika zoezi zima vijijini. Kwa hiyo serikali isikae kando iwe ndiyo *Investor, Developer* na *Planner* ili umeme uweze kwenda vijijini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja na kukushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wamo humu ndani walioomba kuchangia wamekwisha changia lakini wengine hawamo humu ndani lakini ni nia yetu kwamba tutakaporudi tuwaachie Wizara waanze kujibu Naibu Waziri na Waziri na ndiyo tutafunga mjadala.

Kwa hiyo, naomba niahirishe kikao mpaka saa 11.00 jioni

*(Saa 06.30 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotoa taarifa wakati naahirisha Kikao mchana, wazungumzaji waliokuwemo ndani ya nyumba walipewa nafasi wote. Kwa hiyo, sasa nitamwita Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii nichangie kwenye Muswada huu wa Kuanzisha Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini. Lakini kabla sijasema naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibaha, kutoa rambirambi zangu kwa wenzetu waliotutangulia mbele ya haki, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria na Mheshimiwa Balozi Paul Bomani. Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria nilikuwa na mahusiano naye ya kipekee kabisa, niliwahi kufanya naye kazi kama Waziri wangu wa Mambo ya Nje, mimi nikiwa Katibu Mkuu wake. Kwa hiyo nilikuwa na ukaribu naye wa aina hiyo na nawaombea wote Mwenyezi Mungu awarehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme mambo ya ujumla yaliyojitokeza katika mjadala wa leo na Mheshimiwa Waziri akipata nafasi atakwenda kwenye mambo mengine yanayowahusu Wabunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada ni kukabiliana na umaskini wa nishati, yaani *energy poverty* kama nyenzo muhimu ya kupiga vita umaskini kwa ujumla. Kama tunavyofahamu, mipango yetu yote ya maendeleo kama nchi, imekuwa ikielekezwa katika kuhakikisha kwamba tunajikomboa katika janga hili la umaskini, lakini umaskini huu hauwezi kupigwa vita barabara endapo nyenzo muhimu ya kupiga vita umaskini ambayo ni nishati haitapewa kipaumbele. Kwa madhumuni ya Muswada kama ambavyo imeelezwa na Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha na pia michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ni kuhakikisha kwamba tunaipeleka nishati Vijijini na nishati hii itumike kama ni nyenzo muhimu ya kupiga vita umaskini. Kwa maana hiyo basi, nishati ni sekta mtambuka wa maendeleo kwenye maeneo ya afya, elimu, mawasiliano, biashara, kilimo na uzalishaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani mtazamo huo haukuwa umeingia sana kwa upande wa miradi au mipango ya kurekebisha uchumi na hata kwa upande wa wale ambao tunashirikiana nao katika kuleta maendeleo, lakini sasa hivi ni jambo ambalo linakubalika Kimataifa kabisa kuwa huwezi kupiga vita umaskini bila kuhakikisha

kwamba nishati ambazo ni nyenzo muhimu, zinapewa kipaumbele cha aina hii ambayo Muswada huu unajaribu kufanya. Ndio maana basi, kwa upande wa Serikali yetu na kwa upande wa Wizara tuna mradi kabambe wa kuhakikisha kwamba mpango huu unafanikiwa, yaani *energizing rural transformation* ambao Wakala na Mfuko huu utahakikisha kwamba nishati hii inafikishwa Kijijini.

Kama nilivyosema awali, hata katika Kanda na hata Kimataifa, sasa hivi Wizara na Mawaziri wa Nishati wamekuwa wakifanya Vikao na kuunda mfumo wa kuhakikisha kwamba tunaweka msukumo kwa wafadhili na kwa wengine tunaoshirikiana nao katika kuleta maendeleo kuhakikisha kwamba nishati inapewa kipaumbele cha pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, mwaka huu mwezi Machi tarehe 14 -16 pale *Washington DC* Mawaziri wa Nishati wa Afrika walikutana na *World Bank* ili kuhakikisha kwamba suala la nishati Afrika linapewa kipaumbele na kuhamasisha uwekezaji wa Sekta binafsi pamoja na Sekta ya Umma katika kuhakikisha kwamba nishati inapelekwa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala zima la Serikali kujitoa katika usambazaji wa umeme Vijijini. Napenda nichukue nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba, kwa kweli Serikali haijitoi na ukitazama maudhui ya Muswada huu, huu Muswada unachofanya ni kuonyesha dhahiri kwamba Serikali imejiandaa kushughulikia kikamilifu suala la umeme Vijijini kama nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo. Kwa hiyo, badala ya kujitoa, kinachotokea sasa hivi kwa kweli Serikali inajiingiza ndani zaidi katika kuhakikisha kwamba nishati inapewa kipaumbele katika kupata umeme Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele yatapangwa na Bodi na kama ninavyofahamu Bodi hii inaundwa na Serikali na hiki chombo chenyewe. Chombo cha Wakala na Mfuko, vyote hivi ni vyombo vya Serikali na Bodi yenyewe itateuliwa na Serikali. Pia, kutokana na marekebisho yaliyofanywa katika Ibara ya Saba ya Muswada iliyosambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, Bodi hiyo haitakuwa ya Makatibu Wakuu kama ambavyo imekuwa ikisemwa katika michango ya asubuhi hapa. Bodi hii itakuwa na Wawakilishi wa Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, *TAMISEMI*, Sekta binafsi na kadhalika. Kwa hiyo Serikali imetilia maanani wasiwasi wa Waheshimiwa Wabunge kwamba ikiwa Bodi hii itakuwa ni ya Makatibu Wakuu tu, basi inawezekana kwa mujibu wa kazi zao zilivyokuwa nyingi isipate aina ya umuhimu au mchango mkubwa ambao unatakiwa kwa kazi nzito iliyopo mbele yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kuzungumzia suala la Serikali, kuna dhana iliyokuwa inasemwa kwamba, pengine Serikali inajiweka kando. Lilitajwa pia suala la kupeleka umeme Makao Makuu. Napenda nichukue nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, suala la kupeleka umeme kwenye Makao Makuu, bado litabaki kuwa ni jukumu la Serikali kupitia *TANESCO*. Kwa hiyo, katika Wilaya zile ambazo bado umeme haujafika Makao Makuu yake, ningependa Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasiwasi wowote, kazi inaendelea na itaendelea hadi tuhakikishe kwamba Wilaya zote, Makao Makuu yake yanapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya gharama za umeme kiujumla tunaweza kukubaliana kwamba kweli gharama za umeme ni kubwa kulingana na hali ya kipato cha wananchi wetu, lakini kama tunavyofahamu, ni sera yetu na ni malengo yetu ya muda mrefu kuhakikisha kwamba bei hizi zinapungua. Lakini labda niseme tu kwamba, hata wakati tunasubiri hatua hizi za kati na za muda mrefu, Serikali inatoa ruzuku kupitia Shirika lake la Umeme *TANESCO* kwa watumiaji wadogo wale wanaotumia *units* 50 za umeme kwa kulipia *unit* moja kama Sh. 25/=. Pia upo mpango ulioanzishwa wa kuhakikisha wale wanaotaka kuunganisha umeme badala ya kulipa moja kwa moja kwa mkupuo, ama mtu akijiweza anaweza kulipa moja kwa moja, anaweza kulipa kwa awamu tatu kwa maana ya miezi mitatu au anaweza kulipa kwa muda wa miezi kumi na mbili katika mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo imefanywa hivi ili iweze kuwapa unafuu wananchi ambao wangependa kuunganishiwa umeme. Lakini kutokana na hali ya kipato, wasingeweza kulipia gharama hizi za kuunganishiwa na nafahamu kwamba *TANESCO* wamekuwa wakitoa matangazo kupitia vyombo vya habari mbalimbali kuhusu utaratibu huu. Lakini endapo kuna wananchi ambao hawajapata kufahamu hili, basi nichukue nafasi hii kutangaza rasmi kwamba upo mpango wa kulipia uunganishaji wa umeme kwa awamu ambao unasambaa kwa muda wa miezi kumi na mbili na wananchi wanaweza kuutumia mpango huu katika kuhakikisha kwamba wanaunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa Songosongo ambao umezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na hususan Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti, hapa alikuwa na wasiwasi juu ya umeme wa maeneo yake. Napenda nichukue nafasi hii kama alivyosema mwenyewe nilikuwa katika Wilaya ya Rufiji kama mwezi mmoja uliopita na napenda nirejee yale ambayo niliyasema wakati wa ziara ile kwamba tunatarajia Miji ile ambayo ipo kando kando na mradi huu wa Songosongo na Makao Makuu ya Wilaya ya Utete kama ilivyo kwa Kilwa na Miji ya Kibiti, Utete, Mhoro, Ikwiriri na mingineyo itapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa waanze fidia mwanzoni mwa mwezi wa nne, wamechelewa kidogo, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti na wananchi wa Rufiji kwa ujumla kwamba fidia hizi *TANESCO* wameandaa kupeleka *cheque* kwa Mkuu wa Wilaya siku ya Jumatano keshokutwa na utaratibu mzima wa ulipaji fidia utasimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Baada ya hapo, kazi ya kuanza ujenzi wa umeme katika maeneo haya utaanza mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa pia kwamba, tulikosea pengine kwa kutokuanza na miradi mikubwa kama ya *Stigler's*. Ni kweli kwamba Mradi wa *Stigler's* ungekuwa na umeme mwingi na nadhani niseme tu kwamba licha ya kwamba sisi wenyewe tulikuwa hatukuchukua fursa hii katika miaka ya sabini katika kujenga mradi huu kwa wakati ule, lakini hapa katikati pametokea upinzani mkubwa katika medani ya Kimataifa na kwa upande wa wafadhili ya kukataa miradi mikubwa inayotumia maji kwa sababu ya athari za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kusema kwamba sasa hivi hata hao wafadhili na washirika wengine wa maendeleo wamekubali kwamba kwa kweli haiwezekani wakaendelea na msimamo wa aina ile wakati kunahitajika kuendeleza miradi mikubwa ya aina hii kwa ajili ya kuongeza vyanzo vya umeme na kwa ajili ya kuleta mashirikiano baina ya nchi mbalimbali yaani kikanda, kwa mfano, nchi za Afrika Mashariki, nchi za Bonde la Mto Nile, nchi za *SADC* na kadhalika. Msukumo huu umefanywa na Mawaziri wa Nishati wa Afrika na Mawaziri wa Mazingira kuanzia Mkutano wa Bonn mwaka jana 2004 na pia Mkutano wa mwaka huu Washington wa 2005, nakumbushwa na Mawaziri wa Maji, Mazingira, na Nishati kuanzia mwaka jana mpaka mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumetajwa suala la umeme wa Mtwara na Lindi kwa Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo yale na hasa Mheshimiwa Uledi wakati anazungumzia masikitiko yake ya umeme wa Masasi. Niseme tu kwamba, Mikoa ya Mtwara na Lindi imekuwa na matatizo ya aina mbili. Tatizo la kwanza dogo kwa maana ya upatikanaji wa umeme, ni kukatikakatika kwa umeme na umeme usiotosheleza.

Kwa upande wa Masasi pangekuwa na tatizo la mashine za kuzalisha umeme ambazo hapo awali zilikuwa nzuri sana na nzima sana, lakini sasa zimekataa lakini kwa bahati nzuri *TANESCO* wameshaagiza vifaa na vimeshafika nchini. Kwa mujibu wa ratiba ya kurekebisha mashine hizi na kutengeneza mashine hizi tarehe 25 Aprili, wanatarajia kwamba timu ya wataalam na vifaa hivi vitakuwa vimefika Masasi na wataweza kuanza kazi ya kutengeneza mashine hizi na kazi hiyo inatarajia kuchukua wiki nne na baada ya hapo Wilaya zote ambazo zinategemea umeme wa Masasi kama Nachingwea, Ruangwa na Masasi yenyewe watakuwa wamefaidika na hatua hizi ambazo zitakuwa zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa hatua ya muda mrefu ni kuhakikisha kwamba Mikoa ya Lindi na Mtwara inapata umeme wa uhakika. Hapa napenda niseme kwamba uwekezaji ambao tumekuwa tukiusema siku zote katika Bunge hili Tukufu wa Kampuni ya *ATUMAS* kutoka Canada ya mradi wa Mnazibay, nimeutembelea mradi huu kama wiki mbili zilizopita. Ni mradi ambao una matumaini makubwa kwa Serikali na kwa nchi. Wamefikia hatua nzuri sana na ni matumaini yetu kwamba ifikapo Desemba mwaka huu angalau Kijiji cha Msimbati kitakuwa kimeshaanza kupata umeme na mwanzoni mwa mwakani tunatarajia kwamba kazi ya kusambaza umeme itakuwa imeenea katika sehemu nyingine. Hivi sasa Kampuni hii tayari imeshaitisha tenda za ujenzi wa njia za kupeleka umeme mpaka Mtwara na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limezungumzwa kwa ujumla suala la umeme Ruvuma na Kigoma. Mheshimiwa Profesa Mbilinyi alikuwa anauliza hapa, kama itachukua miaka arobaini mingine ili kufikisha umeme Ruvuma. Labda nichukue nafasi hii nimhakikishie ndugu yangu kwamba kwa mujibu wa hatua zinazochukuliwa sasa hivi , Serikali haitachukua miaka hiyo arobaini mingine kufikisha umeme Ruvuma. Hivi tunavyozungumza tayari mshauri ameshapatikana wa kuhakikisha kwamba kazi ya

kufikisha umeme Ruvuma inafanyiwa tathmini ya kutosha. Kama ambavyo tumeshawahi kusema hapa Bungeni, hatua muhimu sana ya kufikisha umeme Mkoani Ruvuma ni ile ya kuhakikisha kwamba *substation* ya Makambako inajengwa. Hivi tunavyozungumza, kazi hiyo ya ujenzi wa *substation* umefikia hatua ya kupata wajenzi. Ni matumaini yetu kwamba baada ya ujenzi wa *substation* hii kazi iliyobaki ya kuhakikisha kwamba zinapatikana fedha za kupeleka umeme Ruvuma itakuwa imekamilika. Nadhani ilifika hatua Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisambaza barua kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma kuwaeleza hatua ambayo Serikali ilishafikia katika kuomba fedha za kupeleka umeme huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia asubuhi kulikuwa na swali la Mheshimiwa Kusila juu ya umeme wa Bahi. Namshukuru kwa maneno yake mazuri juu ya Mkutano ambao niliuitisha na yeye mwenyewe alihudhuria kuhusu umeme wa Bahi. Labda niseme tu kwamba ni kweli kwamba Konoike walikuwa na dhamira ya kupata umeme pale Bahi kwa kazi yao ya ujenzi wa barabara na. Ni kweli kwamba tulidhani ingekuwa ni nafasi nzuri kwa upande wa *TANESCO* kushirikiana na Konoike ili kufikisha umeme Bahi na hivyo kuweza kuwanufaisha wananchi wa maeneo yote husika kuanzia hapa Dodoma. Sasa ingekuwa ni moja kwa moja mpaka Singida.

Mradi mzima ulikuwa unagharimu Shilingi milioni 794. Mpaka wakati wa Mkutano kulikuwa na dalili njema kwamba ingewezekana pakafikiwa maafikiano baina ya *TANESCO* na Konoike. Lakini napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya *TANESCO* kufanya kazi ya kutoa makisio na kazi nyingine ambazo zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa mradi, baadaye wenzetu wa Konoike walitoa taarifa kwamba kwa kweli wao wasingeweza kushiriki tena katika mradi huo. Hii ndio ilikuwa sababu kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme tu kwamba kwa upande wa *TANESCO* kama ingekuwa hali ya kifedha ya Shirika ni nzuri, nadhani wangetumia nafasi hiyo kupeleka umeme kama ambavyo wangetumia nafasi hiyo kupeleka umeme maeneo mengine. Lakini kama tunavyofahamu katika kipindi cha miaka miwili hii na zaidi sasa hali ya *TANESCO* kifedha kutokana na hali ya uzalishaji umeme imekuwa mbaya na kwa hiyo bajeti yake haikuwezesha kutafuta fedha kama hizi za kupeleka umeme hadi Bahi pekee bila kuwa na mshirika mwingine. Lakini kutokana na mpango huu ambao tunauzungumzia hapa, ni matumaini yangu kwamba umeme katika maeneo ya Bahi kama ilivyo katika maeneo mengine utafikishwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango huo wa ujumla napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia na naomba Waheshimiwa Wabunge waupitishe Muswada huu tukitilia maanani yale niliyoanza nayo kusema kwamba tumeuleta Muswada huu ili kupiga vita umaskini wa nishati ambao ni muhimu ili kupiga vita umaskini wa kipato. Bila kupiga vita umaskini wa nishati hatuwezi kupiga vita umaskini huu mwingine.

Kama nilivyoeleza awali, nishati ni sekta mtambuka na inahitaji kuwepo ili kuwa na *manpower* zaidi ili kuwa na manufaa zaidi kwenye Sekta ya Afya, Elimu, Mawasiliano, Biashara, Kilimo na uzalishaji kwa ujumla. Ni matumaini yangu kwamba

Waheshimiwa Wabunge wataungana na sisi na wataupitisha Muswada huu ili nchi yetu iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Msabaha kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo wameitoa wakati wa kujadili Muswada huu. Michango ilikuwa mingi na mizuri na hasa ilikuwa ya kututahadharisha sisi Serikali kwamba tuwe makini katika kuendesha Wakala huu pamoja na ule Mfuko wa Nishati Vijijini ili azma ya Muswada iweze kufikiwa mapema na kwa wananchi wote na kwa hali ambayo ina uwiano wa kijiografia, haina upendeleo na kila mwenye hamu ya nishati apatiwe nafasi au fursa ya kupata nishati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi ni wengi na kwa ruhusa yako, naomba niwataje. Nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Nazir Karamagi, kwa niaba ya Kamati; Mheshimiwa Isaac Cheyo, Upande wa Upinzani; Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa George Mlawa na Mheshimiwa Herbert Mntangi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi na, Mheshimiwa Job Ndugai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Irenius Ngwatura, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Dr. William Shija na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, hoja zilikuwa nyingi, nyingine zinafanana na zilitoka kwa Wabunge mbalimbali lakini tumejaribu kuziorodhesha zile ambazo kwa kweli zinahitaji maelezo kwa muda huu

ambao tumepatiwa. Namshukuru Naibu Waziri kwa yale ambayo ameshayagusia na sitayarudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo ningependa kuizungumzia ni ile inayosema Zanzibar ihusishwe kwenye Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini. Zanzibar tumeihusisha kwa maana ya Serikali ya Zanzibar wakati tukijadili Muswada huu. Kwanza Muswada huu tulifikia hatua hii baada ya kukaa Vikao mbalimbali na wadau mbalimbali nchini kote ikiwa ni pamoja na watumiaji wa nishati hii, wataalam, wafadhili na hata Waheshimiwa Wabunge, tulifanya Semina kule Dar es Salaam na katika Semina mojawapo ya kujadili Muswada huu.

Mwenyekiti wa semina hiyo alikuwa ni Katibu wa Nishati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli wakati wote ule hatukupata hoja kwamba wangependa kushirikishwa kwenye mradi au shughuli hii ya kusambaza umeme Vijijini kwa kupitia wakala wa umeme Vijijini. Nadhani sababu ni kwamba nishati *per se*, sio shughuli ya Muungano maana Bara (Serikali ya Muungano) ina Wizara na Waziri wake na Zanzibar nayo (Serikali ya Mapinduzi) ina Waziri wake wa Nishati, na Shirika lake la Nishati ambalo linashirikiana na *TANESCO* kama mteja, lakini wa umeme ambao unazalishwa huku Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani wenzetu waliona kwamba huu sio wakati wa kuingia kwenye shughuli hii. Hata bei za umeme utakuta Zanzibar wana *tariffs* zao ambapo sisi huku Bara tuna makundi ya *tariffs*. Lakini *tariffs* za chini kwa mfano za walaji wadogo wadogo ni *penterritorial* yaani nchi nzima tuna *tariff* moja kwa umeme wa *TANESCO;* kwa kundi la watumiaji kwa mfano, wa majumbani, viwandani wana *tariffs* zao na kadhalika. Unguja wana *tariffs* zao na namna zao za kuuziana na kukusanya mapato ya umeme.

Kwa hiyo, waliona kwamba labda wakati haujafika wao kushirikishwa katika hili na vile vile tulipokuwa tukizungumza na Wafadhili ambao watatusaidia sana katika kuunda Mfuko huu, kwa kweli Zanzibar haikuwepo kwenye mjadala huo. Nadhani miaka ijayo wakiona kuna manufaa ya kuingia wanaweza wakaleta hapa Bungeni badiliko dogo tu, mahali pa kusema: “Tanzania Bara” tukasema: “Tanzania nzima.” Kwa hiyo mlango haukufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ilikuwa kwamba sekta binafsi isilazimsihwe kujiunga na sekta ya Umma katika utekelezaji wa miradi. Hoja hii ni kweli na sekta binafsi haitalazimishwa na hasa tuwahamasishe wale ambao wana uwezo, mtu au kikundi au Chama cha Ushirika au Halmashauri itakayokuwa na uwezo wa kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme mahali popote pale wakiweza wao wenyewe, basi watapewa leseni, ushauri na watasaidiwa na Serikali wafanye shughuli hiyo kama mradi wa sekta binafsi, mradi wao wenyewe.

Pale ambapo hawataweza na watahitaji msaada wa Serikali au ubia na *TANESCO* kwa mfano, tutawahamasisha kufanya hivyo na tutawaruhusu kufanya hivyo. Kwa hiyo, hawalazimishwi kufanya shughuli hii pamoja na Serikali. Lakini kama ninavyosema,

Halmashauri ambazo ni Serikali za Mitaa au za Wilaya kule walipo wanaweza kabisa kuanzisha miradi hii ikawa ni miradi yao wenyewe, wakaiendeleza na wakazalisha umeme wakawauzia wananchi pale ambapo wanafikiria kuna soko la kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kwamba kuwe na umakini wa usimamizi wa matumizi ya Mfuko wa Nishati unaopendekezwa. Kipengele cha 13 na 16(5) kinaweka bayana uwajibikaji wa Bodi ya Mfuko kwa Waziri na Bunge kuhusu matumizi ya Mfuko wa Nishati Vijijini, utunzaji wa mahesabu, ruzuku inayotolewa na kadhalika. Tumejifunza sasa hivi Serikalini hasa kwa miaka hii kumi ambayo inakwisha sasa ya Awamu ya Tatu jinsi ya kutumia Mifuko hii maalum ambayo inaundwa kwa sababu fulani kama vile Mfuko wa Mbolea, Elimu, Barabara na sasa hivi Mfuko wa Nishati. Tumejifunza sana jinsi ya ku-*manage* Mifuko hii ili itumike vizuri kuwe na uwazi, kusiwe na ubaguzi na tupate manufaa ya Mifuko hiyo.

Vile vile kuwapa imani wale ambao wanachangia ikiwa ni pamoja na walipa kodi wetu maana Mifuko hii fedha zake nyingine zinatokana na kodi zetu, lakini kuna wafadhili vile vile. Kwa hiyo masharti haya yaliyopo hapa ni *standard* kwa Mifuko ya aina hii na inakubalika sehemu nyingi. Kwa mfano, Mfuko huu tumetazama wenzetu wa Zimbabwe, Uganda na kwingine ndivyo wanavyouendesha na umekuwa na manufaa makubwa sana. Kwa hiyo, tutakuwa makini ili fedha hizo zitumike kwa madhumuni yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge vile vile walisema utoaji wa ruzuku uwe wazi pamoja na namna ya kudhibiti bei ya umeme. Hapa ningependa kuongezea tu aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kama mtakavyoona kwenye Muswada huu hasa kwenye jedwali la kwanza, kuna vipengele na vigezo ambavyo vitatumika, tutaviangalia kwa makini sana wakati wa kuchagua miradi. Miradi ikiletwa tutaichambua vizuri, iwe ni miradi ambayo kwa kweli itawasaidia walaji au watumiaji wa umeme na watapata umeme wa nafuu. Pale ambapo tunaona mradi unaletwa unaweza kuwa mzuri kibiashara, lakini hautasaidia katika kuendeleza huduma za jamii katika sehemu fulani basi hautapitishwa na Bodi ya Wakala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wataona kwenye hilo jedwali vigezo gani vitatumika ili kuhakikisha kwamba ruzuku hii inatumika vizuri. Kama alivyosema mwenzangu, tutaangalia kwamba mradi ambao kwa mfano upo mahali fulani umeme wake utakuwa wa bei kubwa kuliko bei ambayo tunalipa *TANESCO*, sasa hivi, tutawaambia wale wawekezaji kwamba huu mradi utawaumiza walaji na sababu ya kutoa ruzuku ni kwamba gharamaza uwekezaji *(capital cost)* zipungue ili aweze kuzalisha kwa bei nafuu na awauzie watumiaji kwa bei nafuu. Kwa hiyo yote hayo tutayaangalia ili watumiaji wa nishati hii hasa huko Vijijini wasije kupatwa na tatizo la kulipa bei kubwa na wakashindwa kuanzisha au kuendesha miradi yao kwa sababu ya nishati ambayo ni ghali sana. Niongezee tu kwamba *EWURA* kazi yake mojawapo ni hiyo. *EWURA* itakuwa inaangalia sana na ipo karibu kuanzishwa sasa, nadhani taratibu za kuanzishwa zipo tayari. Kazi yake kubwa itakuwa ni kuangalia kwamba hakuna ulanguzi au bei ambazo kwa kweli siyo za halali na itasuluhisha. Kwa

mfano, walaji mahali fulani wakiona bei wanayochajiwa na mzalishaji wa umeme ni kubwa wanaweza kuja *EWURA* wakasema, tunaonewa hapa.

Kwa hiyo, *EWURA* atakuwa msuluhishi, ni jicho lingine la Serikali. Kwa hiyo, kwa kweli hawa wawekezaji binafsi hawatatuchukua *for a ride* kwa sababu tumewapa nafasi hiyo ya kuweza kuanzisha miradi kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliulizwa; Je, *TANESCO* imejitoa kusambaza umeme Vijijini? La, hasha! *TANESCO* ipo kushughulikia miundombinu mikubwa mikubwa, kupeleka *Grid* katika ehemu mbalimbali ambazo mwekezaji mmoja labda hataweza kuufikisha. Waheshimiwa Wabunge wengine walisema, kwa nini Vijiji ambavyo viko chini ya waya kubwa visipewe umeme na *TANESCO* sasa hivi.? Sasa hiyo ni aina mojawapo ya miradi ambayo mwekezaji, pale ambapo nguzo kubwa zipo, anaweza akazungumza na *TANESCO* akapewa *step down transformer* ya kupooza umeme ule halafu ukasambazwa kwenye Kijiji pale, ikawa ni mradi mojawapo.Lakini *TANESCO* peke yake labda isingefikiria kufanya hivyo. Ilikuwa inafikiria kupeleka umeme labda kutoka Chalinze kwenda Korogwe, hapa katikati haikufikiria kuwahusisha walaji walioko pale. Ni nafasi hiyo ya Kijiji au mwekezaji binafsi kusema hapa umeme upo tupatie *transformer* tuzalishe umeme Kijiji hiki kipate nishati ambayo inafaa. Kwa hiyo, kwa kweli vinakwenda pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba matawi ya *TANESCO* Mikoani yawe ndiyo Watendaji ili kudhibiti fedha zitakazotolewa kwa wawekezaji. Hakuna fedha ambazo zitakuwa zinatolewa tu ambazo *TANESCO* ingeweza kuzisimamia. Fedha zitapelekwa kwenye mradi na mradi uzalishe. Kwa hiyo, *TANESCO* pamoja na kazi zake zote, hili halitakuwa jukumu lake mojawapo. Fedha za Mfuko zitakuwa zinatolewa na yule *Trust* na nitaelezea baadaye *Trust* maana yake nini? Mtu mwenye mradi akishatimiza masharti fulani, fedha hizo atapewa na yule *Trust Agent* na yule *Trust Agent* analipwa *Commission* yake. Kwa hiyo, gharama zinakuwa ndogo, lakini siyo *TANESCO* itakayohusika kwenye shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge vilevile walisema Serikali iondoe kodi kwenye vifaa vya umeme na vilevile iangalie vipi mtumiaji wa mwisho wa nishati anafaidika kwa kuondolewa *VAT* kwenye vifaa vya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelisikia hili kwa muda mrefu na hivi juzi kodi imefutwa kwenye vifaa vya *solar* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na bado tunaangalia ni wapi ambapo tunaweza kupunguza. Mradi kwa mfano wa kupeleka umeme Ukerewe ulifutiwa kodi. Kwa hiyo, pale ambapo kunastahili, Serikali inasikiliza, maana Serikali ni moja. Sisi Wizara ya Nishati na Madini na wenzetu wa Wizara ya Fedha tuko pamoja na tunafanya kazi ile ile na lengo ni moja la kufanikiwa. Kwa hiyo, kama mahali tunaona kodi ikiondolewa itahuisha au itapunguza gharama ya umeme, basi Serikali inafikiria ikizingatia nia ya kukusanya kodi vilevile kwa sababu ya sekta nyingine. Lakini ni jambo ambalo linazungumzika pale ambapo itahitajika kupunguza gharama za vifaa hivi vya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliulizwa ni jinsi gani uteuzi wa miradi utafanyika na makandarasi wa kuendeleza miradi hiyo watateuliwa. Uteuzi wa miradi utakuwa wa ushindani na pia kwa kuzingatia mahitaji kwenye maeneo yenye uhaba wa vyanzo vya nishati ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo. Hili Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa na wasiwasi kwamba labda walionacho wataongezewa. Kule kwa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ambako anasema *90 percent* wana umeme, kwa kweli ukilinganisha na wenzetu ambao hawajapata miradi ikija, mradi wa kutoka kwake na mradi wa kutoka sehemu ambayo haijapata kama kule Same, basi bila shaka yule wa Same atafikiriwa kwanza kabla ya yule wa Moshi Mjini. Lakini kutakuwa na uwazi na kutakuwa na upendeleo kwa maeneo ambayo hayajapata umeme wa kutosha. Hii tumelisema kwenye Muswada, mtaona na Bodi itakuwa makini sana wakati wa kuchambua miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliulizwa vilevile Bodi itatumia vigezo gani katika kutekeleza miradi, tumevieleza katika Muswada vitatangazwa kila mwanzo wa mwaka kwamba mwaka huu tuna fedha kiasi fulani, tuna bilioni tano labda, bilioni kumi na vigezo vitakavyotumika ni miradi labda ya aina hii, aina hii na miradi hii italetwa na wawekezaji wenyewe. Lakini Wakala wenyewe watafanya utafiti. Hata sasa hivi tunayo orodha ndefu ya sehemu ambazo tunaamini kuna *Potential Projects.* Sehemu zenye maporomoko ya maji kidogo kidogo, lakini hakuna mwekezaji, tutawahamasisha kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu zenye jua zuri la wakati wote, sehemu zenye upepo kama kule Mkumbara kwa Mheshimiwa ndugu yangu Mheshimiwa Lupatu, kuna upepo mwingi, pale Same Makanya kuna upepo mwingi ambao unaweza kuvunwa ukazalisha umeme. Tutawahamasisha wawekezaji kwenda pale ili wazalishe umeme na usambazwe ufike sehemu ambazo unahitajika. *By the way* umeme utakaozalishwa ukiwa mwingi zaidi ya matumizi ya pale utauzwa kwa *TANESCO* kama vile Kiwira wanavyowauzia *TANESCO.* Hata hao wa mashamba ya miwa wakiwa na umeme zaidi wanawauzia *TANESCO*. Kwa hiyo, hii ni biashara ambayo tutaiunganisha na itawafikia wengi na tutakuwa na umeme wa kutosha na kuweza kufikisha katika sehemu nyingi ambazo hazina umeme sasa hivi ikiwa wazalishaji wadogo wadogo tutawahamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko uanze kuweka fedha mapema, hili ni kweli na tumeshalizungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye bajeti ijayo atuwekee tonge moja kubwa kubwa la kuanzia ili tuwe na *impact*. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie wakati ukifika Kamati yetu hasa ile ya Fedha kwamba huu Mfuko upewe kiasi cha kutosha, ukiwa na fedha za kutosha za kuanzia hata wafadhili watasema; ahaa, tuna nia nzuri na watatuongezea fedha na zitakuwa nyingi. Hii ni kabla ya kuanza kutoza ile asilimia ambayo haitazidi tano kwenye uzalishaji wa umeme. Kwa hiyo, tunakubaliana na hoja hiyo kwamba Mfuko upewe fedha za kutosha ili uwe na *impact* kama ule wa barabara ambao una *impact* kubwa kwa sababu una fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala kwamba Bodi itoe kipaumbele kupeleka umeme kwenye Hospitali na Shule. Hili tunakubaliana nalo kabisa. Miradi

itaelekezwa huko na mradi ambao utatoa umeme au nishati kwenye huduma za jamii tutaupa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko midogo midogo maalum itafanya nini? Kwenye Sheria kumetamkwa kwamba kuna *Special Purpose Funds* pamoja na ule Mfuko mkubwa. Mfadhili mwingine anakuja anasema mimi nataka akinamama wahamasishwe kutumia labda majiko ya aina fulani au hospitali ndogo ndogo zihamasishwe kuwa *fridgerator* ndogo ndogo vya kuwekea dawa zao. Huyo Wakala anaweza kuambiwa hebu simamia Mfuko huu. Sasa hiyo ndiyo *Special Purpose Fund* na itakuwa na maana sana kwa Wafadhili ambao wanataka kusaidia *specific purposes.* Ndiyo maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa mazingira uzingatiwe kwa kutoa nishati bora na ya kutosha ili kupunguza tatizo la kukata miti. Tutashirikiana kwa karibu kabisa na wenzetu wa mazingira na hili tutalizingatia kwa sababu tunataka kulinda mazingira yetu na ndiyo dhana hasa ya Muswada huu kupunguza athari kwenye misitu yetu na mazingira kwa ujumla.

Kulikuwa na suala kwamba Wakala au Mwekezaji akija kwenye Kijiji asambaze umeme kwenye Kijiji chote na siyo Kitongoji kimoja akaacha kingine. Hili kwa kweli litategemeana na yule mwekezaji na mahitaji ya umeme pale kwa sababu kama kuna mahitaji makubwa, bila shaka atasambazia wateja wake wote ili apate fedha ya kutosha na mradi wake uweze kulipa mapema. Lakini kama nilivyosema, miradi ya *TANESCO* ambayo sasa hivi inafanya hivyo, wanaweza kufikisha nguzo moja tu kwenye Kitongoji kimoja wakaenda zao. Sasa ni juu ya kile Kitongoji au kile Kijiji au ule Mji kuanzisha mradi waka-*tape* ile *power* iliyoko pale na kuisambaza kama mradi na ikawafikia wengi na wao wakapata faida kama wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliulizwa Taasisi zinazoundwa na Muswada huu ni nyingi mno na labda zitakuwa na wafanyakazi wengi. Kwa nini tuwe na Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini, Mfuko wa Nishati Vijijini *(Trust Agency)*? Majibu yetu ni kwamba kwa kweli hivi siyo vyombo vinavyosimama vyenyewe. Kwa mfano, chombo hasa ni Wakala wa Nishati Vijijini, *Rural Energy Agency* na kama Shirika lolote linakuwa na *Board of Directors* ndiyo hiyo Bodi. *Board of Directors* ni watu wa muda tu wanakutana *three, four times a year*. Kwa hiyo hawana gharama kubwa sana, lakini lazima kuwe na Bodi ambayo itatoa maamuzi kama sheria inavyosema. Mfuko unaitwa Mfuko, lakini ni *account* ambayo iko Benki. Fedha za wafadhili, fedha zetu na zozote zile ambazo zinatumbukizwa pale kwanza ndiyo zitoke sasa kuanza kutumika, lakini ni *fund* ambayo ina madhumuni yake.

Lakini siyo kwamba itaajiri. Wafanyakazi wake, ni wale wale wa *Agency. Director General, Accountant*, Afisa Utawala na kadhalika, hao hao ndiyo wanao-*manage* vyote hivi. Lakini lazima uvitaje ili viwe *separate* kisheria. Kwa mfano, huu Mfuko uwe *separate* na matumizi ya kawaida ya chombo hiki. Usipokuwa na Mfuko maalumu, basi jamaa wanaweza kujinunulia magari, waka-*furnish* Ofisi zao wakafanya mambo ambavyo siyo madhumuni ya ule Mfuko. Kwa hiyo, ndiyo maana tuna Mfuko

maalum na *purpose* zake na matumizi yake yametajwa *specifically.* Fedha zitatokaje, zitakwenda kwa nani na ripoti zitaletwa kila mwaka kwa Waziri na hapa Bungeni kutakuwa na ripoti inayoletwa kila mwisho wa mwaka kuonyesha Mfuko unafanya kazi namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Trust Agency* ni kama Benki. Mradi kwa mfano, uko Tandahimba unamwambia *Exim Bank* pale Mtwara kwamba wewe uko karibu sana *once in while* kama wana uwezo huo, peleka mtu akaone ule mradi unaendelea vizuri. Yule mtu tunayempa ruzuku akisema, msingi nimemaliza, nimeweka mitambo yangu tunaanza kuzalisha *Trust Agent,* ndiye atakayekuwa anasimamia badala ya kupeleka wataalam kutoka Dar es Salaam waende na ndege na posho na nini.

Huyu *Trust Agent* ndiye ambaye atafanya hivyo na ndiye ambaye atakuwa analipa na atawajibika akilipa ovyo ovyo wakati kazi siyo nzuri na ndiyo maana tunataka mtu mwenye uwezo. Huwezi kumweka tu jamaa yeyote hapo ukamwambia wewe ndiye *Trust Agent* ambaye anaweza akafanya mipango na yule mwenye mradi mkapata hasara. Lazima kiwe ni chombo ambacho kina uwezo, kikiharibu kinaweza kulipa. Lakini kina jina lake vilevile, hakiwezi kufanya mchezo kwenye shughuli kama hii. Ndiyo maana tunasema *Financial Institution* kama Benki labda ndiyo wanaweza kuwa *Trust Agent.* Atalipwa *commission and therefore* hatakuwa na gharama kubwa sana. Kama hakuna kazi, basi halipwi chochote.

*REA* imekuwa ni *very skeleton* na tunafikiria hiki chombo chote labda kitakuwa na wafanyakazi 36 hivi, hawatafikia 50 kwa siku hizi za kwanza. Lakini kazi itafanyika kwa kutumia *out sourcing consultant* kama ni miradi kuichambua. Mradi umetoka mahali fulani unachambuliwa na wataalam halafu unapitiwa. Siku hizi ndivyo *Administration* inavyokuwa *lean but efficient,* siyo kama zamani, wafanyakazi wengi na Maofisi wengi na *bureaucracy* kubwa. Kwa hiyo, hakuna wasiwasi hapa kwamba fedha nyingi zitatumika kwenye kuendesha Wakala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mwakilishi wa Wafadhili haruhusiwi kupiga kura? Tunawaheshimu kwa sababu wanatusaidia kifedha na huu ni uwazi na ukweli tu, wasije wakafikiria labda tunachezea hizi fedha. Kwa mfano, Mfuko wa *TASAF* na Mfuko wa *SELF* inasifika sana. Inafanyika kazi nzuri sana kwa sababu ina huo uwazi na *any one can look* na akaona kazi zao ni zipi wanazozifanya, akaona miradi inavyofanyika na mahesabu yao. Sasa huu nao tunasema wafadhili hasa hizi siku za kwanza wakitusaidia tutakuwa na mtu wao pale ambaye anachangia mawazo yake, lakini hapigi kura kwa sababu hatutaki atuingilie kwenye utawala kwa kweli na shughuli zetu, tutaamua wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka ushuru wa asilimia hadi tano kwenye uzalishaji wa umeme kuchangia Mfuko, kutaongeza gharama ya umeme kwa mlaji. Hapa kuna ukweli, lakini kwa kweli hatukuwa na njia nyingine. Hata kwenye barabara anayetumia petroli kila lita analipia kiasi fulani, lakini ndiyo maana tumefika hapa tulipofika kwa sababu hizo Sh.100/= kwenye lita kama unatumia hiyo barabara au hauitumii, lakini unanunua mafuta, basi tunapata fedha tunajenga barabara zetu na

barabara zetu zikijengwa uchumi unaongezeka. Sasa na hii tunasema ni njia mojawapo ya kujenga uchumi wetu hasa huduma za jamii, Shule zipo hazina kompyuta, Hospitali zipo hazina *refridgerator,* hao watu wakichangia umeme ukifika pale tunapata afya na tunapata elimu na tunafanya kazi vizuri na uchumi wetu unaongezeka, tuna-*move forward* kama Taifa.

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nishati na Madini wataangalia waanze na kiasi gani wakiona asilimia tano itawaumiza walaji, basi watashusha na kutafuta vyanzo vingine. Lakini haitakuwa *automatic, five percent* inaweza ikaanza na *three percent, four percent* au *two percent.* Lakini ni jambo la muhimu kwa kweli kuonyesha nia yetu wenyewe na kuwa na chanzo ambacho ni cha kuaminika kwa sababu siku zote watu watatumia umeme na jinsi umeme unavyotumika kwa wingi ikiwa ni pamoja na miradi hii ndiyo fedha hiyo itakapokuwa kubwa na kama vile mafuta tunavyotumia kwa wingi hapa Tanzania magari mengi, basi fedha ya barabara inapatikana na barabara zetu zinajengwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji wa umeme Mikoani na Wilaya hadi Vijijini uwe na uwiano mzuri. Huu ndiyo msingi na tutahakikisha kwamba kunakuwa na uwiano na Waheshimiwa Wabunge wale ambao mtakuwepo na nadhani wengi mtakuwepo au wote karibu mtakuwepo Bunge lijalo, basi mtakuwa mnafuatilia na kuona kwamba kweli hakuna upendeleo na kile kidogo kilichopo kinapelekwa *with fairness* bila kubagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada haujataja vianzio vya nishati vitakavyoendelezwa, ni vianzio vyote. Akija mtu akasema: “Mimi nataka Mradi wa Upepo”, tutautazama kama unakidhi vigezo vyetu tutampa msaada, wa mionzi ya jua, wa *geothermal* kutoka ardhini, wa maji, ni vianzio vyote kwa kweli labda kuni tu kidogo tutasita kuangalia huko. Lakini vile ambavyo haviathiri mazingira yetu na vinakuwa na bei nafuu, basi vitaendelezwa na tutavihamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kwamba gharama za umeme ni kubwa na wananchi hawatafaidika na kwamba Mfuko utoe ruzuku kwa watumiaji wa umeme. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tunatoa ruzuku sasa hivi, *units* 50. Ninayo chati hapa na mtaiona kwenye hotuba yetu ya Bajeti mwaka huu na mwaka jana tuliiweka vilevile. Kwa zile *units* 50 kwa mtumiaji wa chini wa Tanzania ndiye mwenye nafuu kubwa kuliko Kenya, Uganda na naambiwa hata wenzetu wa Zambia na nchi nyingine ambazo zinatuzunguka hapa. Kwa hiyo, tunatoa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu niko kwenye hilo, hata hizi chati kama ninavyosema tutaziweka kwenye hotuba yetu ya mwaka huu, mtaona kwamba kwa sasa watu wanasema Tanzania umeme ni ghali, *this was two years, three years ago,* Kenya wanapandisha umeme, Uganda wanapandisha umeme *all the time* wana matatizo makubwa sana kule. Kwa hiyo, bei yao ya umeme hata viwandani inafanana fanana sana na ya kwetu. Kweli ni sehemu ndogo labda kwenye aina moja tu ndiyo tunawapita, lakini hatuwapiti sana tuko karibu karibu na sehemu nyingi tuko chini. Kwa hiyo, hii hoja au dhana ya kwamba Tanzania umeme wake ni wa juu sana ndiyo maana

viwanda haviji siyo kweli kabisa ukilinganisha na nchi ambazo zinatuzunguka hapa. Lakini mwenzako akiugua na wewe ukiugua huwezi kusema aah, basi siugui.

Kwa kweli umeme wetu ni ghali na jinsi vyanzo vyetu vinavyoboreka vya gesi na kama hivyo tukitumia vingine ambavyo ni vya bei nafuu, basi umeme wetu utakuwa na nafuu zaidi siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilielezwa kwamba nishati ya jua itumike kwenye Zahanati Vijijini. Kama nilivyosema, nishati ya jua ni mojawapo ambayo tunaihamasisha iendelezwe na wale ambao wanataka kujua zaidi kuna Shirika linaitwa *TATEDO* pale Dar es Salaam limeanza kutoa misaada ya nishati ya jua kwenye Zahanati na Shule. *TATEDO* wanakuja wanakujengea kwa bei nafuu kabisa. Shirika hilo linaloitwa *TATEDO* na kule Wizarani tuna anwani yao, tunaweza kuwapa ili mwende mkawaulizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala kwamba; Je, *Qualified Private Developers* watatoka wapi? Vijijini tutawapata wapi? Lakini njia mojawapo ya kuwapata *Qualified Private Developers* Vijijini ni kuitangaza miradi iliyopo na kukaribisha maombi ya kuiendesha kutoka kwa *Private Developers* popote walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hivi Miradi ya *TANESCO* kwa mfano, kutoka Tabora kwenda Urambo inafanywa na *Private Developers,* tena wengine ni *ex-employees* wa *TANESCO* wameanzisha Kampuni zao na wanangojea kazi. Kwa sababu sasa hivi kazi siyo nyingi, hizi zikianza, basi wapo *Developers* ambao wana uwezo, walichokuwa wakitaka ni kuhakikishiwa kwamba kuna soko na kama itakuwa gharama kubwa sana, tunawapa ruzuku na tunawaambia soko lipo.

Kwa hiyo, kwa kweli watapatikana tu na wengine watatoka nchi za jirani ikiwa ni lazima wapatikane kutoka kule waje watujenge, hakuna ubaya anajenga na anaendesha mradi huo. Lakini hasa hasa tunaamini kwamba *developers* watatoka ndani ya nchi na jinsi miradi inavyokuwa mingi, basi shughuli hiyo itakuwa ni moja ambayo inakua na itatoa ajira kwa wingi kwa Kampuni zetu. Sisi hatuna wasiwasi kwamba hakutakuwa *Developers* wa aina hiyo kwa vivutio hivi ambavyo tunavitoa hapa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwa nini Serikali isitumie umeme wa gesi ambao ni rahisi, kweli gesi yetu inatoka ardhini lakini uitoe pale ardhini unatumia fedha nyingi sana. Mradi wa Songosongo uligharimu Dola milioni 250 kuitoa pale ilipo na hizi tulikopa. Tungekuwa na fedha zetu wenyewe mfukoni ile gesi tungeiuza bei rahisi, lakini lazima tulipe lile deni. Sasa baada ya muda, tutaanza kunufaika. Lakini hata hivyo, kwa mfano, *IPTL* tunaanza kubadilisha ile mitambo ili tutumie gesi na ile kidogo itabonyeza gharama. Bei ya umeme kupungua kabisa itategemeana na soko jinsi tutavyotumia wengi, basi utaona lazima bei itashuka tu na wazalishaji kama hivi wakianza kushindana bei nayo itashuka ya umeme. Lakini kwa sasa kwa sababu bado tunalipia vyanzo kama hivyo vya Songosongo kwa kweli ndiyo maana bei haishuki kwa haraka na itachukua muda kidogo kabla haijapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya labda atanisaidia rafiki yangu kuhusu ule mradi wa bei poa. Yeye alikuja nadhani na Mwenyekiti au na Ofisa mwingine mkauleta mkaniona nikawaita Makamishna wangu tukakaa tukazungumza, tukawapa maswali rahisi na machache ili tuweze kuutekeleza, maana nyie ni Wawekezaji bwana, tunawashika kwa mikono miwili. Lakini mlipotoka pale sikuwaona tena wala sikusikia nini kimetokea? Hilo nadhani ukipata nafasi utanijibu. Lakini kwa kweli hilo ndilo lililotokea, hawa jamaa hawakurudi tena na umeme poa umekuwa umeme potea. Hatujasikia habari zake tena. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28 cha Muswada kinachowalinda wafanyakazi wa wakala kiondolewe. Mheshimiwa Ludovick Mwananzila alihoji kifungu hicho na alikuwa na wasiwasi kwamba labda kifungu hicho kinawalinda wazembe au nini. Lakini nadhani kwenye sheria zetu ni *standard.* Ukianzisha chombo kama Shirika hili unawahakikishia wale unaowaajiri kwamba fanyeni kazi bila wasiwasi wowote, mkikosea kwa nia njema kama Daktari vile akikosea kwa nia njema, basi humshtaki. Lakini atakayekuwa mzembe au mwizi au mbadhirifu huyo atachukuliwa hatua na zimesemwa katika Sheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila asiwe na wasiwasi, hilo tutakuwa tumelizingatia. Tulishajibu kuhusu Mheshimiwa Maria Watondoha, alikuwa na wasiwasi na umeme Mikoa Kusini na tulivyokuwa tukitoka Bungeni aliniambia nimwonyeshe *list* ya Vijiji ambavyo vitapata umeme kutoka Songosongo kuja mpaka Dar es Salaam. Tunayo hapa ya Vijiji karibu 49 vitapata umeme na maji. Kwa hiyo, kwa kweli wanavijiji nao watanufaika na mradi huo moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Edward Ndeka, alikuwa na mradi wake pamoja na Wachina. Namuahidi kwamba tutauangalia na huo ni mojawapo ya miradi ambao unaweza kuingia katika kusaidiwa na Mfuko huu, kwa sababu kama Wachina watamletea mitambo yeye au Halmashauri yake au Kampuni yake na wakija kwenye Mfuko huu, wanaweza wakasaidiwa kwa namna fulani wakaanzisha mradi wa kuzalisha umeme pale mahali na msingoje mpaka *TANESCO* ifike. Mheshimiwa Herbert Mntangi na yeye ana Vijiji vyake ambavyo vinahitaji umeme wa jua, kama nilivyosema tunaweza kuiangalia wakati Wakala huu ukishaanza kazi. Nadhani hayo ndiyo ambayo nilitaka kuyaongezea. Kama kuna la zaidi ambalo hatukuligusia, basi tunaweza kutoa maelezo zaidi wakati tukiwa tunatekeleza mradi huu kwa sababu kwa kweli umechelewa, tunachoomba mturuhusu Muswada huu upite uwe sheria na sisi tuko tayari kabisa kuuanza mara moja. Tukikutana mwezi Juni hapa labda tutakuwa na hadithi nyingine ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaanza kuwa tunapokea miradi na kuona kwamba kazi hii inafanyika na umeme unafikishwa kule ambako unahitajika kwa wananchi ambao wanaungoja kwa muda mrefu sana na tunasukuma maendeleo yetu kwa nishati hii ambayo tunaamini itakuwa ya bei nafuu au ya bei ambayo wanaweza kuilipa na ikawa ni kichocheo cha maendeleo Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini wa Mwaka 2005 *(The Rural Energy Bill, 2005)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hapa nilitaka kuuliza tu kwamba watu watakaoweza kutengeneza umeme kidogo kidogo kama watauzia *TANESCO* na ukiwa mwingi; Je, *TANESCO* itafanyaje? Itawaondoa au itasitisha mikataba? Itakuwaje kama wakiweza kuzalisha umeme mwingi kuliko kiwango kinachotakiwa? Itapata wapi fedha za kununua huo umeme na wakati Mkataba wamekwishasaini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naamini kabisa kwamba hao Wawekezaji kwenye miradi hii watakuwa wamefanya pembuzi yakinifu kwa kiasi ambacho watazalisha umeme tu ambao unahitajika kwenye soko lile wanalotaka kulihudumia kwa wakati ule. Kama ikitokea wana umeme zaidi ya ule wanaohitaji, basi watawauzia *TANESCO*. Nchi hii bado ni kubwa sana na *TANESCO* bado inahitaji umeme. Wangepata umeme wa uhakika kama huo wangepunguza matumizi ya *IPTL* ambayo ni mafuta na ni ghali. Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunaunganisha sasa hivi *Grid* yetu na nchi za jirani kwa mfano Kenya ambao wanahitaji umeme sana. Kwa hiyo kama *TANESCO* itakuwa na bahati ya kuwa na umeme wa ziada, basi soko kwa kweli lipo kwa miaka mingi ya usoni, hakuna wasi wasi.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu Na. 14 pale kuna *establishment* ya *Agency*. Lakini *EWURA* ambayo ndiyo *regulator,* sioni kwamba pengine hapa ndiyo imetajwa pamoja na hii *Agency.* Sijui Waziri ana tamko gani kuhusu *EWURA* ili kudhibiti matumizi au ku-*regulate* mambo haya ya umeme!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* atakuwa *regulator* na labda nimsomee Mheshimiwa Mbunge sehemu ndogo ya maelezo yangu ili yaingie kwenye *Hansard* vizuri. "Kwa kuwa gharama ya uwekezaji itakuwa imepungua, bei ya umeme au huduma yoyote ya nishati itabidi iwe nafuu ili kuvutia wateja. Aidha, *EWURA* watakuwa na wajibu wa kutathmini gharama ya uwekezaji na bei ya nishati kabla ya kutoa leseni." *EWURA* kama nilivyosema katika maelezo yangu mwanzoni, itasuluhisha migogoro kati ya wazalishaji na walaji. *EWURA* inahusika wakati wa kutoa leseni kuhakikisha kwamba kwa kweli hakuna uonevu kwa walaji kutokana na mradi ambao mwekezaji ataweka na bei ambazo ataziweka. Lazima *EWURA* iangalie kuona kwamba kuna *fairness* na hakuna uonevu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hapa nimeona kifungu cha 17, *Establishment of funds*. Nimeona kwamba *percentage* hizi asilimia tano na *VAT* zinazidisha gharama ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hizi gharama za asilimia tano halafu *VAT* zinakuwa ni mzigo mno ambapo tungeweza tukaamua kubakiza *VAT* tusiweke tena gharama nyingine na namna ya kupata fedha. Kwa hiyo mifuko ikatafutwa kwa namna nyingine zaidi au ikatoka kwenye hiyo *VAT*. Kwa hiyo nilitaka Waziri atueleze hapo kwa sababu wananchi wanaumia kutokana na bei za umeme.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote na Mheshimiwa Mbunge, kifungu cha 17 hakina aina yoyote ya tozo. Hakina *VAT, Levy,* hakuna! Sasa ni vizuri ataisaidia Kamati yako ielewe ni nini hasa kusudio lililomfanya asimame.

Nadhani kama anataka nimsaidie, aende akasome kifungu cha 19 nadhani anawahisha mambo ambayo hayajafikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, subiri mpaka tufikie kifungu cha 19.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa iko kwenye orodha hiyo hiyo basi tutaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ninauliza tu kuhusu hizi gharama ambazo zinaendelea kuwepo. Mpaka sasa hivi watu

wanapiga kelele kuhusu *VAT* wanataka iondolewe. Sasa tuongeze tena asilimia tano na *VAT* inabaki pale pale. Tunataka Waziri atueleze ni vipi tutafanya hili maana nia ya mradi huo hasa wa Vijijini ni kupunguza matumizi ya nishati za kuni na kadhalika ili misitu yetu isife. Sasa kama tutashikilia tu kwamba lazima tuwanyonye ili tuweze kupata namna ya kuendesha, hatuwezi kufika. Naomba Waziri atueleze Serikali ina mpango gani?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ngawaiya swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *VAT* na hiyo *Levy* kama vingechanganywa tu halafu tukaachia hapo unaweza kusema zinaongeza gharama. Lakini wakati wote Serikali inatafuta njia za kupunguza gharama za nishati. Kama nilivyosema, kila mwaka Waziri wa Fedha anaangalia mapato na matumizi yake na hoja zilizoletwa. Safari hii amepunguza kodi kwenye vifaa vya *solar*. Sasa hapa napo miradi kama hii kila mwaka atakuwa anaangalia. Je, tuweke *levy* kiasi gani ambacho kitatusaidia kufanikisha azma hii ya kupeleka umeme Vijijini? Sio lazima iwe asilimia tano. Sheria inasema *"up to",* isiyozidi asilimia tano. Inaweza ikawa asilimia mbili kama ana vianzio vingine vikubwa vya kutosha akasema iwe asilimia mbili mwaka huu. Kama hakuna vianzio vingine akasema iwe asilimia tatu. Maana nia yetu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tupate uwezo wa kusambaza umeme haraka haraka tuchochee uchumi wetu ili tuweze kulipia hiyo asilimia tano. Kama miradi itaanzishwa, ajira itaanzishwa, mapato yataongezeka, basi asilimia mbili au tatu hapa na pale kwa kweli haitakuwa kubwa sana kwa faida kama hii ambayo tunapata ya kichocheo cha uchumi wetu.

*VAT* itakuwa inaangaliwa mwaka hadi mwaka kutegemeana na mahitaji ya fedha ya Waziri wa Fedha. Kwa hiyo vyote hakuna kilichofungwa kabisa, tutatafuta njia ambayo itahuisha mzigo huu wa gharama za umeme Vijijini. Lakini ni lazima tuwe na chanzo chetu cha kuaminika na ndio wafadhili watakuja kutusaidia. Bila hivyo watasema sasa nyinyi wenyewe hamchangii chochote. Lazima tuwe na njia kama hiyo. Kama ile Sh.100/= kwenye mafuta ambayo tumezoea sasa na tunafurahi barabara zinajengwa.

Ahsante Mwenyekiti.*(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana kwa asilimia 90 ya majibu ya Waziri. Lakini namna ya kupata hizi fedha kule Kijijini kwanza hakuna. Sasa hizi gharama tunazoongeza kweli ana uhakika kuna wanavijiji wenye uwezo wa kulipa huo umeme na kuongeza hizo gharama nyingine?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi natoka Kijijini kama ndugu yangu hapa. Lakini tuseme ukweli, hivi kweli *unit* moja leo ya umeme labda ni Sh.100/= umwambie mtu Kijijini kwamba kama utalipia Sh. 105/= utapata umeme na faida zote za umeme pale Kijijini. Mimi nadhani wengi wangesema nitaacha dengerua yangu na mambo mengine nipate hii Sh.5/= niongeze kwenye *unit* nipate umeme. Ni jambo ambalo kila mtu analingojea kwa hamu sana. Kwa hiyo sidhani kama litakatisha watu tamaa. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja tu kuhusu vyanzo vya Mfuko hasa kile chanzo ambacho kinatokana na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasi wasi kama huu Mfuko utapata fedha za kutosha kwa sababu hakuna kigezo chochote kilichowekwa. Tumeacha tu kwa huruma ya Waziri wa Fedha atakazoamua ndiyo hizo zitakatwa. Je, Waziri wa Fedha akiamua tunawapa Shilingi milioni 200 mwaka huu, hii kweli tutafanikisha mradi huu ama mradi ambao tunataka kupeleka Vijijini wa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifananishe na Mifuko mingine kama ule wa barabara. Wewe ni shahidi kwamba Mfuko wa Barabara umekuwa *packed* kwenye mafuta. Kwa hiyo tuna uhakika wa kupata fedha zile. Huu Mfuko haujawa *packed* kwenye *anything,* uko hewani tu. Waziri wa Fedha atakavyoamua ndivyo utakavyopata. Sasa nataka nijue Waziri wa Nishati ana uhakika gani wa kupata fedha za kutosha kwa kazi hiyo? Isije ikawa kama mradi huu wa *CDA,* hauna fedha unakaa tu ilimradi upo pale. Tutaunda vyombo vile ambavyo tutagharamia kulipa mishahara, lakini hawana kazi ya kufanya kwa sababu tutakuwa hatuna fedha za kutosha. Kama kweli tuna nia nje, ebu aniambie kwamba kwa kuanzia, Waziri wa Fedha ama Serikali itatenga kiasi gani katika bajeti ya kawaida?

Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mpango huu wa Wakala wa Umeme na Mfuko wa Umeme Vijijini ni mpango wa Serikali nzima na Serikali inafanya kazi kwa pamoja. Si mpango wa Wizara peke yake uliobuni ikaja hapa Bungeni. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye nadhani wasiwasi wake unaeleweka kwamba tusubiri wakati wa bajeti utakapofika dhamira ya Serikali itaonekana juu ya uanzishwaji wa Wakala huu na mfuko huu. Napenda nimtoe wasiwasi kwamba ni mpango wa Serikali na utatengewa fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 23

Kifungu cha 24

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 25

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulizie swali moja la ufafanuzi katika sehemu ya 25 ya Muswada huu kuhusu *qualification* ya Mkurugenzi Mkuu na hasa hiyo Sehemu ya Pili.

Nashukuru kwamba amefanya mabadiliko katika kifungu hicho kwa kuondoa neno "*Internationally*" ambayo sasa neno hilo limetokea, kwa hiyo neno halipo sasa hivi nashukuru.

Lakini nilikuwa nafikiria kwamba wangeweka "*nationally*" badala ya kuacha sentensi ina-*hang* namna hiyo. Maana yake mimi nilikuwa nalenga kwamba hawa wataalamu ama Mkurugenzi awe Mtanzania, kwa hiyo tungeweza kuweka neno "*nationally*" pale ingebana ili mtu wa nje asiweze kupata nafasi hiyo. Lakini kama tuko tayari kufungua milango ili tuajiri watu wa nje, sawa lakini wasi wasi wangu ndio huo. Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Degera swali lake kuhusu huyu *Director General* atatoka wapi. Tumeondoa "*Internationally*" anasema labda tungeweka "*Nationally*" au *"National Competitive Selection"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali tunaelewa *sentiment* zake hizo kwamba pale tunapoweza tunawachukua Watanzania wenzetu. Kama ni mradi, kazi ni kitu gani tunaweka upendeleo kwa Watanzania wazalendo. Kwa hiyo tukiondoa hii "*Internationally*" hapa bado hawa watakaochagua huyu *Director General* wakati wa kuchambua, watakuwa wanaangalia kama tuna Mtanzania ambaye anafaa. Kama hakuna kwa kweli katika wale walioomba, basi tutalazimika kwa muda kuchukua mtu wa nje ili chombo chetu kiweze kuendeshwa vizuri. Lakini nia yetu na *sentiments* zetu ni kuchukua Mtanzania mwenzetu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 26

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nazungumzia kifungu Na.26(b) kuhusu *Managing* ya *Budget*.

Mhekshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu kwamba, mwaka jana tulipitisha bajeti hapa tukasema *units* 100 ndiyo hazitachajiwa. Sasa hapa katikati ikabadilika ikawa ni *units* 50. Kwa sababu tulipitisha hapa Bungeni hilo suala la kushusha kutoka *units* 100 kuja kwenye *units* 50 halikupitishwa hapa Bungeni tena. Nilitaka kujua hizi *powers* tukishapitisha hapa Meneja anaweza akabadilisha *time to time*?

**MWENYEKITI:** Mkisoma hii inasema: *"Functions of the Director General." Nothing to do* na hizo *units.*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Hawajaleta bado?

**MWENYEKITI:** Hapana. Hii ni ya Utawala

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

**Jedwali la 1**

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**Jedwali la 2**

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima umeufikiria Muswada wa Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Act)* 2005 kifungu kwa kifungu na umeikubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Act 2005)* sasa ukubaliwe. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Muswada unaofuata utaanza kesho. Kama mnavyoona kwenye *Order Paper* kuna Muswada unaofuata. Kufuatana na Kamati ya Uongozi iliyokubaliana kwamba kila siku tutakuwa na Muswada mmoja. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho Saa Tatu asubuhi.

*(Saa 12.18 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 19 Aprili, 2005 Saa Tatu asubuhi)*